Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Kumi - Tarehe 20 Juni, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, kabla hatujaanza, nieleze ratiba ya leo kwamba tutaendelea na mjadala wa jumla mpaka saa sita. Itakapofika Saa Sita nitawaita Mawaziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu waanze kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa mpaka Saa Saba. Itakapofika Saa Kumi na Moja ndiyo ataitwa mtoa hoja mwenyewe ili aweze kuhitimisha hoja yake kwa muda kama wa Saa moja hivi baada ya hapo ndiyo tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi, kupitia kifungu hadi kifungu. Hiyo ndiyo ratiba ya leo.Sasa tunaanza Kikao cha Kumi cha Mkutano wa Ishirini.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 90

**Mashujaa wa Uhuru**

**MHE. TEDDY KASELLA-BANTU** aliuliza:-

Kwa kuwa, tunao waasisi/mashujaa walioanzisha mikakati ya kudai uhuru na kuanzisha Chama cha *TANU* miaka 50 iliyopita na kwa kuwa ni muhimu kwa watoto na vijukuu na kadhalika kujua historia ya nchi yetu:-

(a) Kwa kuwa walikuwa 17 chini ya uongozi wa Baba waTaifa; Je wale 16 ni akina nani?

(b) Kama Baba wa Taifa alikuwa Mwenyekiti na Mzee John Rupia Makamu Mwenyekiti, nani alikuwa Katibu, Mweka Hazina, Wajumbe wa Kamati ya Utendaji?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIBU)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kwa watoto, wajukuu na taifa kwa ujumla kujua historia ya waasisi na mashujaa walioanzisha mikakati ya kudai uhuru na kuanzisha Chama cha *TANU* kwa Tanganyika na *ASP* huko Zanzibar.

Kazi ya kwanza kabisa ya *TANU* kwa Tanganyika ilikuwa kuwaunganisha wananchi na kuwaongoza katika mapambano ya kupigania uhuru wa kitaifa. Mapambano hayo yalikuwa ni kuendeleza juhudi za wananchi waliopambana na mabeberu na wakoloni tangu karne ya 19.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wajumbe 16 kati ya 17 waliohusika na uundaji wa *TANU* chini ya uongozi wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, tarehe 7 Julai, 1954 ni hawa wafuatao:-

Ndugu S. M. Kitwana, Ndugu C. O. Milinga, Ndugu Kisung'utu Gabara, Ndugu L. M. Bugohe Makaranga, Ndugu Saadani A. Kandoro, Ndugu Dosa A. Azizi, Ndugu Abdalla K. Sykes, Ndugu Joseph Kasella-Bantu, Ndugu Patrick Kunambi, Ndugu Germano Pacha, Ndugu Japhet Kiliro, Ndugu John Rupia, Ndugu Joseph Kimalando, Ndugu Abubakar Iranga, Ndugu Tewa Said Tewa na Ndugu Ali Sykes.

(b) Baba wa Taifa alikuwa Rais wa *TANU* na Ndugu John Rupia Makamu wa Rais wa *TANU.* Mwandishi wa *TANU* siku za awali alikuwa Ali Sykes hadi Januari mwaka 1955 alipochaguliwa Katibu Mkuu wa kwanza wa *TANU* Ndugu Oscar Kambona.

Katika miaka ya awali ya kuundwa kwa *TANU* tunadhani hakukuwa na Kamati ya Utendaji.

**MHE. TEDDY KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba kuongeza swali moja la nyongeza;

Kwa kuwa, hawa waasisi wa *TANU* wengine walifukuzwa kazi wakati ule na wakajitolea kupata maisha ya shida na kutunza watoto wao katika shida kutokana na vipato vyao kuviacha na kwenda katika kazi ya Kudai Uhuru Na kwa kuwa mfano wa *KANU*, Jomo Kenyata alipopata Uhuru aliwapa wengine biashara ya daladala na wengine aliwapeleka kwenye *settlers* kuchukua mashamba. Je, Serikali inayotuongoza inawafikiria nini kuwatunza hawa au kuwapa kifuta jasho na kuwaenzi viongozi walioanza hapo awali na kutufikisha katika matunda haya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIBU):** Mhesimiwa Spika, kwanza ningependa kusema kwamba Chama cha Mapinduzi na Serikali iliyopo Madarakani sasa hivi, inawaenzi na itaendelea kuwaenzi waasisi hawa kwa sababu wamechangia sehemu kubwa ya uhuru wa nchi yetu ya Tanzania.

Pili, Mheshimiwa Spika, wakati wazee hawa walipokuwa wanajiunga kuunda Chama, madhumuni makubwa yao yalikuwa ni kuikomboa nchi yao ya Tanganyika na walifanikiwa sana. Kwa hiyo, fahari yao kwanza kwamba wao wanaona kwamba nchi hii imekomboka na ninaona fahari sana leo kwamba Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu ni mmoja wa wanaofaidi matunda ya uhuru wa Tanganyika na uhuru wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mawazo ya Mheshimiwa Kasella-Bantu nayathamini na Chama cha Mapinduzi kitaendelea kuwathamini waasisi hawa. *(Makofi)*

Na. 91

**Tatizo la barabara za Kapalala - Gua na Kapalala Udinde**

**MHE. PAUL E. NTWINA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara za Kapala - Gua na Kapalala - Udinde ni za Wilaya na kwa kuwa barabara hizo hazijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu, hali inayosababisha kutopitika wakati wote hata kusababisha Tumbaku isichukuliwe; na kwa kuwa barabara hizo zinapita kwenye maeneo ya wananchi ambao wanajishughulisha na kilimo cha Tumbaku huko Gua na Uvuvi huko Udinde:

Je, Serikali Kuu haiwezi kusaidia kutengeneza barabara hizo mbili ili kuondoa tatizo kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul E. Ntwina, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa hali ya barabara ya Kapalala - Gua yenye urefu wa kilomita 35 na Kapalala – Udinde yenye urefu wa kilomita 7 zilizopo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya hazipo katika hali nzuri hivyo kutopitika kwa kipindi kirefu cha mwaka.

Kutokana na hali hiyo Halmashauri ya Wilaya kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara inaendelea na juhudi za kuzifanyia matengenezo barabara hizo ili ziweze

kupitika kwa kipindi kirefu cha mwaka. Juhudi ambazo zimekuwa zikifanywa hadi sasa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

Moja, Kufanya matengenezo ya mara kwa mara kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2003/2004 jumla ya kilomita 35 za barabara ya Kapalala – Gua zimechongwa kwa Greda na mifereji ya maji ya mvua imetengenezwa . Kiasi cha shilingi 34,500,000/= zilitumika kukamilisha kazi hiyo.

Pili, Katika mwaka 2004/2005 madaraja mawili ya Kikamba na Lukwati katika barabara ya Kapalala - Gua yamekarabatiwa kwa kuondoa mbao na kuwekewa deki ya zege na iligharimu shilingi milioni 28.

Vile vile katika kipindi hicho daraja la Manda Juu kwenye barabara ya Kapalala – Udinde limefanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi milioni 3.

Mheshimiwa Spika, ili barabara ya Kapalala – Gua iweze kupitika kwa mwaka mzima, Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kwa mwaka wa fedha 2005/2006 itaifanyia matengenezo ya sehemu korofi kilomita 35 kwa gharama ya shilingi milioni 5.5 kutoka katika mfuko wa barabara.

Mheshimiwa Spika, juhudi hizo zote nilizo zieleza hapa zinatokana na fedha za Serikali na wala siyo Halmashauri kwa maana ya mapato yake yenyewe. Serikali itaendelea kuzifanyia matengenezo barabara hizo hadi ziweze kufikia kiwango ambacho kinaridhisha.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Vijiji vya Gua, Ngwala, Udinde, Some Kapalala na Kininga vinapakana na Mbuga za wanyama za Lukwati, eneo zuri kwa Utalli na eneo ambalo pia linalimwa Tumbaku; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kuwa barabara hizi zitatengenezwa.

Je, anaweza kunihakikishia kuwa kwa baadaye hizi ni vyema kutengeneza kwa kima cha changarawe hizi barabara kwa sababu mara kwa mara zimekuwa zikitengenezwa na mvua inayonyesha maeneo yale imekuwa ikiziharibu?

Swali la pili, kwa kuwa hizi barabara zimeunganishwa na barabara ya Mkoa, Saza – Kapalala kwa maana ya Mbalizi–Saza; na kwa kuwa yapo maeneo ambayo nimeyasema sana huko nyuma ambayo yako na udongo mwekundu na udongo mweusi.

Je, yale maeneo nayo Waziri anaweza kutusaidia kuyaimarisha ili barabara yote sasa mpaka kule Gua na Udinde ipitike?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ningeweza kabisa kuahidi kwa sababu Serikali muda wote ina nia nzuri ya kujaribu kuondoa kero hizi, lakini nachelea kusema hilo kwa sababu ya matatizo tu ya kifedha.

Ninaloweza kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa maeneo yote mawili, tutaendelea kushirikiana na Halmashauri yake kujaribu kutatua matatizo haya kadri uwezo wa fedha utakavyokuwa unapatikana. Dhamira yetu ni nzuri, kikwazo kikubwa ni fedha tu.

**SPIKA:** Swali la msingi linahusu barabara za Chunya, sasa Mheshimiwa Lubeleje uliza swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kutengeneza barabara katika Halmashauri zetu ni kidogo sana, ni asilimia 30 tu ya mfuko wa barabara na Wizara ya Ujenzi inabaki na asilimia 70. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba wakati umefika sasa angalau Halmashauri za Wilaya zipate asilimia 40 au 50 za fedha ili tuweze kutengeneza barabara zetu vizuri?

**SPIKA:** Hilo sawa sawa, Mheshimiwa Naibu Waziri endelea kujibu hilo swali la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lubeleje swali lake ni zuri sana lakini nasema tu kwamba mambo haya ni vizuri tukaenda tunayatazama kwa pande zote mbili. Tunaweza tukapunguza kweli upande wa barabara za Mkoa na Taifa, lakini nina hakika Bunge hili hili mtasema tumebomoa upande ule ambao mlifikiria ni wa maana zaidi.

La msingi hapa ni kujitahidi tuone kama tunaweza tukawa na utaratibu unaotuwezesha kupata mapato zaidi ili tuweze pengine kuwa na utaratibu ambao utatuwezesha kuongeza nguvu za matengenezo pengine kuliko kupunguza kiwango kilichopo hivi sasa kwa sababu kote kwa kweli kunahitajika.

Na. 92

**Kambi ya Wasiojiweza na Wenye Ukoma**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa na utaratibu wa kuhudumia kambi za wasiojiweza na wale wagonjwa wa ukoma; na kwa kuwa kambi hizo ni za miaka mingi kiasi ambacho wale wanaoishi humo wameyazoea sana mazingira hayo na wamezaa watoto ambao wengi wao hawakuathirika na ugonjwa wa ukoma lakini kutokana na mazingira ya kambi

hizo, baadhi ya watoto wanaozaliwa hukataa kwenda shule na kuungana na wazazi wao kwenda kuomba mitaani na wengine kujiunga na watoto wanoishi katika mazingira magumu/wasio na makazi;

(a)Je, Serikali inafahamu kwamba katika kambi hizo kuna idadi kubwa ya watu waliokamilika viungo vyao vyote na hao ni nguvu kazi isiyotumika ipasavyo? Je, Serikali itakuwa tayari kutunga sheria itakayo wabana wale wote wenye viungo vilivyokamilika wajitegemee?

(b)Je, Serikali inawasaidiaje hao watu ili nao waweze kujipatia mahitaji yao kwa kuwapatia pembejeo na mikopo ili wajishughulishe?

(c)Je, Serikali kwa mara ya mwisho ilipeleka lini fedha za kuhudumia kambi hizo, kwa mfano Kambi ya Ipuli – Tabora Mjini, Iduguta – Nzega? Je, kambi hizo zina idadi ya watoto wangapi na watu wazima wangapi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mchemba, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kwamba katika makazi ya wasiojiweza wapo pia wananchi wenye viungo kamili. Ukamilifu wa viungo hata hivyo siyo kigezo pekee cha uwezo wa kujimudu. Wapo wananchi wenye viungo kamili na hata nguvu za kufanya kazi lakini kutokana na mazingira waliyomo wanashindwa kujitegemea.

Kadhalika wapo wananchi wasio na viungo kamili, kwa mfano watu wenye ulemavu lakini wana uwezo mkubwa wa kujimudu, wanajitegemea na wanategemewa na watu wengine.

Watu wenye umri mkubwa, wenye maradhi ya moyo, *TB*, *Sickle cell*, mvurugiko wa akili na kadhalika. Mara nyingi wanahitaji kusaidiwa ili waweze kujimudu. Kwa maana hiyo Serikali haiwatunzi wananchi wenye uwezo wa kujitegemea. Kutokana na ukweli huo Serikali haina mpango wa kutunga sheria ya kuwabana wanaodaiwa kuwa na viungo kamili na wanaishi ndani ya makazi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu wa kuwahudumia watoto wa makazi. Kwanza, watoto hao wanapelekwa shule na wanasoma kwa kadri ya uwezo wao yaani hadi Chuo Kikuu. Watoto wanaomaliza Darasa la Saba hufanyiwa utaratibu wa mafunzo ya kazi za ufundi na hatimaye kuwatafutia namna ya kujitegemea kwa kuwapatia mitaji na nyenzo za kufanyia kazi.

(c) Mheshimiwa Spika, makazi ya Ipuli – Tabora yana jumla ya watu wazima 76. Miongoni mwao 47 ni wanawake na 29 ni wanaume. Kuna watoto 36, wasichana 17 na wavulana 19.

Jumla ya fedha zilizotumwa kwa mwaka huu wa fedha hadi kufikia Machi, 2005 ni shilingi 3,700,000/=. Makazi ya Iduguta – Nzega yana jumla ya wahudumiwa 51, miongoni mwao watoto ni 15. Makazi haya yanaendeshwa na Kanisa la *Pentecost*.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini nina swali dogo moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imekiri kuwepo ongezeko la watoto na kwa kuwa Serikali ilikuwa ikiwahudumia wagonjwa na wasiojiweza ambao wagonjwa hao ni wa ukoma na kwa kuwa Serikali ilikuwa imezingatia upungufu huo kwa wale wenye ukoma ni kwa sababu hawana vidole wala miguu na kuwaweka mahali pamoja kama kambi na kusahau kwamba wana uwezo wa kuzaa. Pamoja na hayo naomba sasa niulize swali dogo la nyongeza. Je, Serikali imewahi kuongeza nyumba au vyumba kufuatana na idadi halisi iliyopo hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mwanne Ismaily kwamba ulemavu walionao watu wa ukoma ni wa vidole na midomo lakini uwezo wa kuongeza watoto wanao. Lakini, lazima tufahamu kwamba watoto hao ili waweze kuishi wakipata mapenzi ya wazazi wao wanahitaji na wao kuendelea kukaa na wazazi wao pale pale walipo. Sasa suala la kuongeza vyumba ni pale watoto hawa wanapofikia kwamba haiwezekani tena kwa umri wao kuishi chumba kimoja na wazazi. Pale ndipo tunapofikiria namna nyingine na wakati huo mara nyingi watoto hawa wanakuwa tayari wameishamaliza au Darasa la saba kwa hiyo tunawapeleka vyuo vya ufundi au wengine wamefanikiwa kwenda sekondari. Kwahiyo, ule uwezekano wa kukaa chumba kimoja na wazazi unakuwa umepotea. Lakini kwa umri ule wa chini bado wanakaa nao. Naomba la msingi kabisa, siyo namna gani tunaweza kuongeza vyumba kwa ajili ya wagonjwa wa ukoma na watoto wao, lakini ni jukumu la sisi Watanzania, kama wazazi, kama wahusika wa wagonjwa hao kuwahudumia badala ya kuwaacha mitaani mpaka Serikali ije iwaokote na kuwaweka kwenye kambi. Kila Mtanzania athamini kumchunga ndugu yake, awe mgonjwa wa ukoma, *TB*, Buba na kadhalika.

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, labda nyongeza kidogo tu kwa majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa. Ni kwamba lile suala la makambi haya kama tulivyokwisha eleza mara kwa mara ndani ya Bunge hili lako Tukufu, tunayalea kwa ushirikiano na Halmashauri za Wilaya. Mheshimiwa Mbunge, hebu atusaidie basi kwa nia ya kuwasaidia watoto hawa kwa kushirikiana na Halmashauri yake ya Wilaya atoe mchango unaoweza kusaidia katika kupambana na tatizo hili. Kama ameliona limejitokeza kwa kasi kubwa zaidi katika kambi ya Ipuli na kambi ya Iduguta – Nzega. Mheshimiwa, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nina swali moja tu la nyongeza kwamba; mwaka jana Mjini Nzega tulianzisha kituo cha walemavu

na tulimwalika Mheshimiwa Waziri wa Kazi kuja kukifungua na alipokifungua aliendesha mchango wa harambee kusaidia hawa Walemavu. Sasa Wizara inawasaidiaje hawa wanaokuwa pale kwenye kituo, mathalani katika yao mwaka jana waliwapa nini kusaidia kituo hicho maana alikisifu kuwa ni cha kwanza Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa sana kumpongeza sana Mheshimiwa Kahumbi kwa jinsi yeye anavyoishirikisha Wizara yetu katika masuala yanayohusu walemavu na wazee ndani ya Jimbo lake, ndiyo maana alimwalika hata Waziri akaone hali halisi ilivyo wakati wa ufunguzi wa chuo kile. Hata hivyo, ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Kahumbi na Wabunge wote kwamba nia yetu ni kusaidia kila palipokuwa na kambi ya wazee, walemavu na hata vyuo, lakini uwezo wetu wa kuchangia fedha hizo unategemea na mapato yetu. Ningeomba Mheshimiwa Kahumbi asubiri hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, aweze kuona ni namna gani safari hii amejiandaa kusaidia vituo hivyo pamoja na vyuo vyetu.

Na.93

**Askari wa Zimamoto Katika Viwanja vya Ndege**

**MHE. DR. AMAN W. A. KABOUROU** aliuliza:-

(a) Je, ni kweli kwamba, Askari wa Zimamoto wanaofanya kazi katika viwanja vya ndege wamehamishwa kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwenda Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi?

(b) Je, Askari hao wanafanya kazi kwa kutumia kanuni/ taratibu za kijeshi au kiraia?

(c) Je, maslahi ya Askari hao, ikiwemo mishahara, marupurupu, kupandishwa/kushushwa vyeo pamoja na pensheni zao yanalipwa kwa utaratibu wa kijeshi au kiraia?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Dr. Aman W. A. Kabourou, napenda kutoa maelezo mafupi kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Zimamoto na uokoaji ni moja ya huduma zinazopaswa kuwepo katika uendeshaji na usimamizi wa shughuli za viwanja vya ndege ili kuhakikisha usalama wa mali na maisha ya binadanu wanaosafiri kwa njia ya anga na wanaotumia au kutoa huduma mabalimbali katika viwanja vya ndege. Utoaji wa huduma za Zimamoto na Uokoaji huzingatia viwango vilivyowekwa na Shirikisho la Kimataifa la Usalama na Usafiri wa Anga *(The International Civil Aviation Organisation)* kwa mujibu wa makubaliano ya Chicago ambayo Tanzania imeridhia na ni mwanachama.

Mfumo wa huduma za Zimamoto na Uokoaji katika viwanja vya ndege duniani hutegemeana na muundo unaokubalika. Katika nchi zingine, huduma hii huwa ni sehemu inayomilikiwa moja kwa moja na Mamlaka inayohusika na uendeshaji wa viwanja vya ndege.

Kwa upande wa Tanzania, huduma ya zimamoto na uokoaji kwenye viwanja ndege vilivyo chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, hutolewa na Kikosi cha Zimamoto ambacho kiutawala kipo chini ya Kamishna wa Zimamoto na Uokoaji, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Aman Kabourou, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Meshimiwa Spika, Ni kweli kwamba mwaka 1996 Serikali iliwahamisha Askari wa Zimamoto na Uokoaji kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwenda Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na hatimaye Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania. Askari hao walihamishiwa viwanja vya ndege ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za kuzimamoto na uokoaji katika viwanja hivyo.

(b) Meshimiwa Spika, Askari hao wanafanya kazi kwa kufuata taratibu za Kijeshi. Kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Utumishi wa Umma *(The Public Service Act)* Na.8 ya 2002 na hivyo kufutwa kwa Sheria ya Zimamoto na Uokoaji Na.3 ya mwaka 1985, Usimamizi pamoja na uongozi wa shughuli zote za zimamoto na uokoaji unafanywa kwa kutumia mwongozo wa sheria hiyo ya Tume ya Utumishi wa Umma.

(c) Mheshimiwa Spika, maslahi ya askari hao yanatolewa kwa msingi na kanuni zilizopo kama ifuatavyo:-

- Mshahara hulipwa kwa mujibu wa muundo wa mishahara ya askari hao *(Tanzania Protective Service Workers)*.

- Marupurupu hulipwa kwa mujibu wa niongozo inayotolewa kuhusiana na kada hiyo.

- Askari hao ni wanachama wa Mfuko wa Pensheni wa Utumishi wa Umma; hivyo masuala ya pensheni zao hushughulikiwa kwa mujibu wa Sheria na kanuni zilizopo.

- Kupandishwa/kushushwa vyeo pamoja na masuala ya nidhamu kwa ujumla hushughulikiwa na mamlaka zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria, kanuni na taratibu zinazohusika na usimamizi wa shughuli za Zimamoto na Uokoaji kama nilivyoeleza hapo awali.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Waziri, nataka nimuulize swali moja kwamba kwa kuwa sasa hivi, maghorofa yanajengwa marefu na hawa watu wanakuwa hawana vifaa vya kuzimia moto kwenye maghorofa marefu na sasa ni muda mrefu toka hali hiyo imetokea. Wizara ina mpango gani au Serikali ina mpango gani wa kusaidia ili waweze kuzima moto huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ingawaje Wizara yangu inashughulika na masuala ya Zimamoto katika Viwanja vya Ndege pahala ambapo hakuna maghorofa, lakini Kiserikali naamini kwamba Wizara zinazohusika ikiwemo na Tawala za Mikoa watashughulikia ipasavyo kupata vitendea kazi kama tulivyoona juzi wakati unazimwa moto katika jengo ambalo lina ghorofa karibu 18.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaamini fika wanaohusika wameliona hilo na watashughulikia.

Na. 94

**Uhitaji wa Mawasiliano ya Simu**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika zama hizi za Sayansi na Teknolojia mawasiliano ni jambo muhimu, nyeti na zuri; na kuwa, sehemu mbalimbali za Jimbo la Nyang'hwale hazifikiwi na mtandao wa mawasiliano ya simu za mkononi kutoka kwenye minara ya *Celtel, Vodacom* na *Mobitel* iliyoko Bugarama (Wilayani Kahama), Sengerema, Sima na ile ya Bukoli na Geita na kwa kuwa katika Jimbo hilo tayari kuna watu wengi, taasisi mbalimbali zikiwemo za Kidini, Kielimu, Wafanyabiashara na Viongozi wa ngazi mbalimbali wa Serikali walio na simu za mikononi ambazo ili kuzitumia inawalazimu kupanda juu ya miti, milimani au kwenye vichuguu ili kupata mawasiliano:-

(a) Je, Serikali imefikia wapi juu ya ombi la Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale na ahadi ya Kampuni ya *Celtel* ya kujenga mnara wa mawasiliano Jimboni kabla ya Julai, 2005?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuwasiliana na Kampuni ya *Vodacom* na *Celtel* ili wajenge minara katika eneo hilo lenye wateja wengi wanaohitaji mawasiliano hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Phillipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali iliwasiliana na Kampuni ya *Celtel* kuhusu kueneza huduma za mawasiliano katika maeneo yaliyomo katika Jimbo la Nyang'hwale. Utafiti ulionyesha kuwa mnara ukijengwa eneo la Kukuluma utafikisha mawasiliano katika maeneo ya Jimbo la Nyang'hwale. Mnara tayari umejengwa. Napenda nimwarifu Mheshimiwa James Musalika kuwa mtambo wa Kukuluma umewashwa wiki iliyopita na tunategemea wataalam watakwenda kufanya tathmini ili kuona kama kazi iliyofanywa au tatizo lililoko limetatuka au kuna hitajika ufumbuzi mwingine. Napenda hapa nimshukuru Mheshimiwa Musalika kwa juhudi zake za kufuatilia huduma za simu katika Jimbo lake.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda nimjulishe kwamba Kampuni ya *Vodacom* wametueleza kuwa maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge yanafanyiwa tathmini hususan yaliyomo katika Jimbo la Nyang'hawale ambayo hayana mawasiliano. Uchambuzi ukikamilika na kuonekana kuwa yana mvuto mkubwa wa kibiashara. Kampuni hiyo ya simu itajenga mitambo ya mawasiliano mapema iwezekanavyo.

Tumjulishe pia kwamba Kampuni ya Simu ya *Mobitel* wametuambia kwamba na wao wana mpango wa kufikisha mawasiliano ya simu kwenye Jimbo la Nyang'hwale. Utafiti utafanywa hivi karibuni ili kutekeleza azma hiyo.

Namwomba Mheshimiwa Musalika na Wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale wavute subira. Lakini waone kwamba juhudi kubwa Mheshimiwa Mbunge wao alizozichukua katika kutatua matatizo ya simu katika Jimbo lake.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Kijiji anachotamka sijakipata vizuri, ana maana ya Kalumwa, Kulumwa, sielewi vizuri na kwa kuwa utafiti uliofanywa na Kampuni ya *Celtel* ilikuwa ni Kalumwa Msalala.

Je, kama ndiyo Kalumwa anasema na mimi nilikuwa kule wiki iliyopita na sikupata taarifa, ni kijiji hicho hicho. Na kama sivyo.

Je, Waziri yuko tayari kuwasiliana na Kampuni hiyo na zingine kama vile *Zantel* ya Zanzibar ambayo sasa hivi inaruhusiwa kufanya kazi Tanzania Bara wapeleke minara huko na *Vodacom* na *Mobitel* haraka sana kabla ya Uchaguzi Mkuu ujao? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Musalika, kama ifuatavyo:-

Mimi naamini na nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba hamu yake ni kuona kijiji cha na Jimbo lake la Nyang'hwale linapata huduma za mawasiliano mapema inavyowezekana. Nia ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kupitia Kampuni za simu Tanzania, ni kuona tunafikisha huduma za mawasiliano ya simu nchini kote Tanzania. Napenda nimhakikishie Mbunge kuwa juhudi hizo zitaendelea na tutaendelea kuwasihi wanaohusika watekeleze wajibu wao. Kama nilivyomjibu wakati wa jibu langu la msingi kwamba tuliwasiliana na *Vodacom* na wameahidi, tumewasiliana na *Celtel* wameahidi na wenzetu wa *Celtel* walituambia wao wameshajenga mnara kwenye eneo la Kukuluma. Sasa Mheshimiwa Mbunge, kama wamekosea wao kutuambia, mimi nitarudi tena kwao niulize ni kijiji hiki Kukuluma au kuna sehemu nyingine zaidi ambayo unaisema Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Mbunge, tukuhakikishie kwamba *Zantel* wameshapata leseni ya kuja Tanzania Bara na wao hivi sasa wanajitayarisha, walituambia mwisho wa mwezi huu au mwanzoni mwa mwezi ujao wataanza kutoa huduma hapa Tanzania Bara. (*Makofi*)

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jimbo la Nyang'hwale liko Wilayani Geita na Wilaya ya Geita ina eneo la ziwa ambapo kuna visiwa kama vya Lubondo, Zumacheli, Butwa na Mesome na eneo lile kumekuwa na tatizo la mawasiliano kwa ajili ya kuhudumia wavuvi na watu wa maeneo yale na Serikali imeonyesha mfano mzuri wa kuweza kupima kwamba wangeweza wakaweka mnara katika Kijiji cha Nkome. Je, Serikali inasemaje kuukamilisha huo mnara? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naamini atakubaliana nami kwamba juhudi kubwa zimefanywa za kupeleka mawasiliano ya simu Geita. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba Vijiji alivyovitaja vya Kibunda, Zumacheli, Butwa wanaohusika na mawasiliano watafanya utafiti na kuona kama kuna uwezekano wa kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo pindi wakiona kuna huduma za kibiashara. Mheshimiwa Mbunge, nadhani sasa wananchi wako wa karibu pale wengi tu wanapata huduma za mawasiliano ya simu na nia ni kufikisha huku ambako umesema. Tunashukuru kwa kuona umuhimu wa mawasiliano katika maeneo yako. (*Makofi*)

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi nimeshaandika mradi wa kusambaza mtandao wa simu katika Jimbo la Kahama na kwa kuwa tayari nimeshawasiliana na baadhi ya Makampuni ya simu za mtandao wa simu za mkononi na kwa kuwa katika Jimbo la Urambo Magharibi, tayari mtandao huu upo. Je, Serikali itatusaidia watu wa Jimbo la Kahama kuhamasisha haya Makampuni ili yaweze kutimiza matarajio ya wananchi wa Kahama? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa tukushukuru Mheshimiwa Raphael kwa juhudi zako unazozifanya napenda nikuambie kwamba tutawasukuma wanaohusika katika huduma za mawasiliano ya simu waone umuhimu na ku-*coordinate* hiyo *project* yako uliyoiandika kwa ajili ya kupeleka mawasiliano katika maeneo yako. (*Makofi*)

Na. 95

**Walimu Wanawajibika Chini ya Wizara Ipi?**

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa Walimu wetu wanafanana na watoto yatima kwa kuwa hawana Wizara ambayo wanawajibika moja kwa moja na kuweza kuwajibishwa kuhusu kero zinazowahusu:-

(a) Je, kwa suala la kutolipwa mafao na stahili zao ni Wizara gani kati ya hizi inawajibika, fedha, Elimu na Utamaduni au Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa?

(b) Je, kushindwa kufaulu mitihani kunakowasibu wanafunzi wetu wa shule za msingi na sekondari kunasababishwa na Wizara gani?

(c) Je, huko kuvuja kwa mitihani kunakotokea kila mara ni Waziri gani alaumiwe?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Mwalimu Stephen Kahumbi, Mbunge wa Bukene, naomba kutoa maelezo ya kiujumla kama ifuatavyo:-

Walimu kama Watumishi wengine wote wa Serikali hulipwa mishahara yao na mafao mengine kutokana na mafungu ya fedha za Serikali ambazo husimamiwa na Wizara ya Fedha, ambayo hufanya malipo ya mishahara na mafao mengine kutokana na mafungu ya Wizara mbalimbali yaliyopitishwa na Bunge.

Mafungu ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, hutumiwa kuwalipa mishahara na mafao mengine Walimu wa Shule za Msingi za Mazoezi na wa Shule za Sekondari na Vyuo vya Ualimu na mafungu ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hutumiwa kuwalipa Walimu wa Shule za Msingi wanaofundisha katika Shule za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu sehemu (a), (b) na (c) ya swali la Mheshimiwa Stephen Kahumbi, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara inayohusika ni ile inayosimamia fungu ambalo mshahara wa mwalimu husika umo kwa kuzingatia maelezo ambayo nimekwisha yatoa.

(b) Mheshimiwa Spika, kushindwa kufaulu mtihani kunakowasibu wanafunzi hutokana na sababu mbalimbali na inawezekana isiwepo Wizara inayohusika na kasoro hiyo. Kwa mfano, kama mwanafunzi ni mtoro, mzembe au mvivu. Ili wanafunzi wafaulu lazima walimu wafundishe kwa ukamilifu na wanafunzi nao wawe na ari ya kujifunza kwa ukamilifu na kuhudhuria shuleni kila siku. Kwa hiyo, ni muhimu uwepo ushirikiano wa walimu, wazazi na wanafunzi wenyewe. Tumekuwa na maendeleo mazuri katika jambo hili. Asilimia ya wanafunzi wanaofaulu mtihani wa darasa la VII imepanda kutoka 14% mwaka 1995 mwanzoni mwa Serikali ya Awamu ya Tatu hadi 20% mwaka 2000 Bunge hili lilipochaguliwa na hadi 49% mwaka jana 2004. Aidha kufaulu katika mtihani wa kidato cha 4 katika madaraja I-III kumeongezeka, kutoka asilimia 25 mwaka 2000 hadi 38.77% mwaka 2004 kwa wanafunzi wa shule zote na 52.99% kwa wanafunzi wa shule za Serikali. Kwa kidato cha 6 kufaulu katika madaraja I-III waliofaulu wameongezeka kutoka 70.7% mwaka 1995 hadi 80.7% mwaka 2004.

(c) Naomba Mheshimiwa Mbunge, atofautishe kati ya kuvuja kwa mtihani na wizi wa mtihani. Katika ya hivi karibuni kuanzia mwaka 1999 hatujawa na tukio lolote la kuvuja kwa mtihani bali tumekuwa na matukio kadhaa ya wizi wa mitihani kama ilivyotokea katika Shule ya Sekondari ya Ngateru Mkoa Arusha, katika mtihani wa kidato cha 4 Novemba 2004, ambapo wahusika wamechukuliwa hatua zinazostahili kwa mujibu wa sheria ya mitihani. Mlinzi na mwanafunzi mmoja wamefikishwa Mahakamani na jumla ya watahiniwa 1,544 wakiwemo wa shule 1,307 na wa binafsi 237 waliogundulika kupata mtihani kabla ya wakati wamefutiwa matokeo yao ya mtihani. Kama kila wizi ukitokea kwenye sekta fulani Waziri wa sekta hiyo atatakiwa kujiuzuru basi sijui nani atabakia katika Baraza la Mawaziri!. Wajibu wa viongozi pamoja na Mawaziri ni kupambana na wezi siyo kujiuzulu kila unapotokea wizi. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. STEPHEM M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu hapo nyuma kidogo tumekuwa na matatizo ya walimu kutolipwa mafao yao, mishahara, posho, matatiba mpaka akalazimika Waziri Mkuu kuunda Tume. Je, ni nani ambaye alisababisha hiyo mishahara isipatikane kwa walimu na kutokana na ripoti ya Tume hiyo, Serikali inasemaje kuhusu hao waliokuwa wanawapa mateso walimu wetu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI**): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Stephen Kahumbi, kama ifuatavyo:-

Kulikuwa na matatizo mengi yaliyosababisha walimu kupata matatizo ya kulipwa mishahara na mafao yao mengine. Lakini tatizo kubwa lilikuwa ni kutokuwa na uhakika na idadi kwanza ya walimu wenyewe wanaodai, lakini la pili uhalali wa malipo kwa hiyo, Serikali ilihakikisha kwamba kwanza inafanya uhakika wa walimu halisi na wale ambao ni hewa, lakini pili kufanya uhakiki wa madai halali na yale yalikuwa hewa na baadaye ndiyo malipo yakaanza kufanyika. Juu ya Tume ambayo iliundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi ningeomba nimwachie Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Olfisi ya Waziri Mkuu, ili aweze kulitolea maelezo ya kina. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika,

napenda kumhakikishia Mheshimiwa Stephen Kahumbi, kwamba kama alivyosema Naibu Waziri matatizo yaliyosababisha walimu kutokupewa fedha zao yamesababishwa katika ngazi mbalimbali. Yapo matatizo yaliyosababishwa na utendaji wa Halmashauri baada ya kufika zile fedha wametumia isivyotakiwa. Yapo matatizo yaliyosababishwa na Wizara mbalimbali kama Wizara na Elimu.

Hatua zilizochukuliwa baada ya ile tathmini na taarifa kutolewa Serikali imewaandikia viongozi wa maeneo yote yaliyohusika katika upotevu wa fedha hizi na kuwapelekea orodha ya watu waliohusika moja kwa moja na kutajwa katika ile taarifa. Kwa sababu zile ni tuhuma tusingeweza kuchukua hatua moja kwa moja, lakini kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma, tunawaomba viongozi katika maeneo yale yote na maeneo ambayo wahusika wametajwa wachunguze ili waweze kubaini wale ambao kweli wamesababisha matatizo haya na kero hizi kwa walimu wawachukulie hatua za nidhamu. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, kwamba baadhi ya Mikoa hivi sasa wameshawachukulia hatua za kinidhamu wale wote waliosababisha upotevu au kero hii kwa walimu. (*Makofi*)

Na. 96

**Serikali Kufadhili Wanafunzi**

**MHE. JOEL N. BENDERA (K.n.y. MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeweka mkakati wa kuwafadhili wanafunzi wanaofaulu kwenda kidato cha kwanza ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwalipia karo:-

(a) Je, ni wanafunzi wangapi wa Wilaya ya Serengeti wamenufaika na mpango huo tangu mwaka 2002 hadi 2005 na umegharimu fedha kiasi gani?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa karo ya wanafunzi wanaosoma katika shule za sekondari nchini ili kuwaondolea kero wananchi wa Tanzania na mpango huo utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI**) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, tangu mpango wa Serikali wa kugharimia elimu ya sekondari kwa wanafunzi wanaofaulu mtihani wa darasa la VII ambao wazazi wao hawana uwezo uanze mwaka 2003, hadi mwaka huu wa 2005 jumla ya wanafunzi 118 wa Wilaya ya Serengeti wamenufaika na mpango huo na jumla ya Shilingi 27,720,000/= zimetumika kugharimia Elimu ya Sekondari kwa wanafunzi hao.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa haina mpango wa kuondoa karo katika shule za sekondari za Serikali kwa sababu inafaa wazazi walio na uwezo wachangie angalau kiasi kidogo katika kugharimia elimu ya watoto wao. Serikali imepunguza kiwango cha karo ya shule za kutwa kutoka shs. 40,000 hadi 20,000 lakini pia Serikali inatoa ruzuku ya uendeshaji wa shule ya shs. 40,000 kwa kila mwanafunzi kwa Sekondari za Serikali zikiwemo shs.20,000/= zinazofidia ada iliyopunguzwa. Aidha ada ya shs. 20,000 inayolipwa inabakia shuleni na kufanya jumla ya fedha za uendeshaji kuwa shs. 60,000 kwa mwanafunzi. Ada ya 20,000 inaweza kulipwa kwa awamu mbili za shs. 10,000/= kila muhula.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka huu ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha alishatoa na alitoa ahadi mwaka jana kwamba fedha hizi zitakuwa zinaongezwa kila mwaka ili kuongeza idadi ya wanafunzi ya kusaidia wanafunzi ambao wazazi hawajiwezi. Je, katika mwaka huu Bajeti hiyo ipo, maana safari sikumwona Mheshimiwa Mramba akijitanua kwa hilo? (*Makofi*)

Katika wanafunzi hao 111 na wengine ambao wamesaidiwa Wilaya ya Serengeti na Wilaya zingine zote, yako matatizo ya wanafunzi hawa kurudishwa majumbani kwa ajili ya kukosa ada na kutoa usumbufu sana kwa wanafunzi hawa. Je, kwa nini hili linatokea na watoto hawa hawana uwezo, wazazi wao hawana uwezo kwa nini inatokea Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba fedha hizi zinafika kwenye shule husika? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI**): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Joel Bendera, kama ifuatavyo:-

Juu ya kama fedha hizi zitaendelea kuwepo katika mwaka huu wa fedha ningemwomba Mheshimiwa Mbunge avute subiri, asubiri siku ya Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Elimu na Utamaduni, aweze kuona mambo yakoje ambayo ni mazuri tu. *(Makofi/Kicheko)*

Juu ya watoto kurejeshwa nyumbani kwa kweli ni tatizo la utendaji. Fedha zinatolewa na Wizara kupelekwa kwenye Halmashauri. Inawezekana zikachelewa hapa au pale, lakini ni suala tu la Halmashauri husika ambayo inasimamia mfuko huo kuwasiliana na shule inayohusika badala ya kuwanyanyasa hawa watoto kuwarejesha nyumbani wanajisikia wanyonge. Halmashauri iwasiliane na shule zinazohusika na mambo haya bila shaka hayana sababu ya kutokea tena. Naomba nitoe wito kupitia Bunge lako Tukufu, kwamba uongozi wa Halmashauri uwasiliane na shule hizi kwamba inapotokea fedha zimechelewa kufika watoto hawa wasibugudhiwe waendelee kusoma iwe ni suala la Halmashauri na uongozi wa shule za sekondari zenyewe. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU):** Mheshimiwa Spika, nyongeza kidogo ni kwamba Serikali imeshatambua udhaifu huo kwa hiyo, kwa maana hiyo, wameshafungua mawasiliano ya moja kwa moja kati ya Wizara ya Elimu na Utamaduni na shule husika. Kwa hiyo, kama

kuna tatizo kama hilo, Mkuu wa Shule ashauriwe awasiliane na Wizara moja kwa moja ili kuhakikisha fedha zinatumwa. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, aidha namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini naomba nimuulize swali moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Elimu ya Sekondari, sasa ndiyo elimu ya kusaidia katika vita dhidi ya umaskini; na kwa kuwa tulipofuta fedha za upe shilingi 2,000 ni kwa sababu wazazi wengi walikuwa hawawezi kulipa shilingi 2000. Je, ili tupate manufaa ya Elimu ya Sekondari, Serikali haioni kwamba wazazi wengi bado wanashindwa kulipa hata shs. 20,000 ambazo zimepunguzwa toka 40,000? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI**): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Slaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tunafahamu kwamba bado sehemu kubwa ya jamii yetu ni maskini lakini kwa yule ambaye amedhamiria kusomesha mtoto wake ada ya Shilingi 20,000 kwa mwaka, ambayo inaweza kulipwa katika awamu mbili kwa kweli kama ana dhamira ya kusomesha mtoto wake atasoma. Lakini kwa yule ambaye hawezi kabisa kuna utaratibu ambao unaanzia kwenye Serikali za Kijiji, wanaohibitisha kwamba huyu hajiwezi ndiyo fedha hizi zilizotengwa kusomesha watoto wasiojiweza zinaingia pale katikati. Kwa hiyo, mimi ningemwomba Mheshimiwa Dr. Slaa na Wabunge wenzangu wote kwamba tuwahimize wazazi wenzetu wote wathamini kusomesha watoto na Shilingi 20,000 nina uhakika mwenye nia anaweza akalifanya jambo hilo. (*Makofi*)

Na. 97

**Kasoro Katika Mfuko wa Bima ya Afya**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa kasoro nyingi kwenye Mfuko wa Bima ya Afya, kama vile Watumishi wengi kutopatiwa vitambulisho pamoja na kwamba wanakatwa fedha kwa ajili ya mfuko huo, baadhi ya wagonjwa kutounganishwa kwenye mfuko huo, uchache wa hospitali na vituo vya afya vilivyochaguliwa kutoa huduma hiyo?

(b) Kwa kuwa fedha ambazo Watumishi wanachangia ni nyingi kuliko huduma zinazotolewa, Je, Serikali inaonaje kutokata mishahara ya watumishi kwa asilimia badala yake iweke kiwango maalum kufuatana na uwezo wa kila mtumishi?

(c) Je, Serikali haioni kuwa ni busara kuharakisha kuziingiza hospitali za Mashirika ya Dini yaliyoko karibu na Watumishi wengi kwenye mpango huo ili kupunguza kero ya kutembea na kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hizo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mpango wa Taifa wa Bima ya Afya tayari imeondoa kasoro nyingi zilizoukabili Mfuko hasa katika hatua zake za awali za utekelezaji. Baadhi ya jitihada zilizofanyika ni pamoja na hizi zifuatazo:-

Moja, utoaji wa Elimu ya dhana ya Bima ya Afya kwa wadau, ambapo mwanzoni kulikuwa na malalamiko kuwa dhana ya Bima ya Afya ilikuwa haieleweki. Baada ya Elimu kutolewa wadau wote sasa wanafaidika dhana hii.

Pili, ufunguzi wa Ofisi saba 7 za kanda umesogeza huduma karibu na wadau. Awali wadau walilalamika kuwa huduma za kiutendaji zilikuwa zinatolewa kutoka Dar es Salaam yalipo Makao Makuu ya Mfuko. Hatua hii imefanyika katika kipindi kifupi cha utekelezaji wa mpango huu.Nne, kuongeza uwigo wa mafao yatolewayo na mfuko ikiwemo, idadi na uwigo wa vipimo, huduma pamoja na bei za dawa zimeendelea kufanyika marekebisho kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la vitambulisho hadi tarehe 31 Desemba 2004 jumla ya wanachama na wategemezi wao wapatao 946,233 walishatengenezewa vitambulisho vya matibabu. Hii ni sawa na asilimia 83 ya lengo. Kati ya vitambulisho vilivyotengenezwa vitambulisho 29,610 vilipelekwa Mkoani Singida. Kwa upande wa Wilaya Iramba, mfuko umekwisha peleka vitambulisho 7,650 kati ya vitambulisho 8,675 vilivyotarajiwa kama wanachama wote wangejaza fomu. Jitihada zinazofanyika sasa ni kuhakikisha kwamba wanachama ambao hawajajaza fomu wanajaza fomu hizo ili watengenezewe vitambulisho na wakati huo huo Wizara tayari imeuagiza uongozi wa Mfuko ufanye zoezi la sensa ili kubaini na kuwatambua wanachama wake, pamoja na kushughulikia suala zima la vitambulisho. Aidha mfuko umesajili jumla ya vituo 3,724 kati ya hivi 3,169 ni vya Serikali na vingine 555 ni vya madhehebu ya dini na Mashirika yasiyo ya Kiserikali pamoja na maduka ya dawa. Vituo hivi ni vingi na Mkoa Singida kuna jumla ya vituo 176 vilivyosajiliwa kati ya hivyo 167 ni vya Serikali 9 ni vya Mashirika na dini na binafsi.

(b) Mheshimiwa Spika, Mifuko wa Bima ya Afya, imejengeka katika misingi ya mshikamano kwa wale wenye vipato vikubwa kuwachangia wenye vipato vidogo, wenye familia ndogo kuwachangia wenye familia kubwa na wenye afya nzuri kuwachangia wale wanaougua mara kwa mara. Serikali inaona utaratibu wa sasa ni mzuri na haina mpango wa kukubali kwa sasa kwa sababu utaratibu wa kuchangia kiwango cha malipo utawapa mzigo mkubwa Watumishi wenye viwango vidogo vya mishahara.

(c)Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana kuwa ni busara kuzishirikisha hospitali za Mashirika ya Dini, ndiyo maana vituo hivi vilianza kujumuisha tangu tarehe 28 Machi, 2002. Mpaka tarehe 31 Desemba, 2004 mfuko ulikuwa umeshasajili vituo 555 vinavyomilikiwa na Mashirika na Dini ili kutoa huduma sambamba na vituo 3,169 vya Serikali vilivyopo katika maeneo husika.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bima ya afya kuna baadhi ya tiba haitoi hasa magonjwa yenye gharama kubwa. Je, Serikali haioni kwamba kutokutoa huduma yote kwa Watumishi kupitia Bima ya Afya haiwatendei haki Watumishi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, magonjwa ambayo Mfuko wa Bima ya Afya haulipii ni yale tu ambayo hayatozwi aina yoyote ya malipo kwa kuwa Serikali inayahudumia. Naomba nitoe mfano wa magonjwa kama Ugonjwa wa Ukimwi, magonjwa ya Kisukari, *TB* magonjwa ya kifua kikuu ambayo tayari kuna mipango ya Serikali ambayo inatoa fursa kwa yoyote anayehitaji tiba kupata matibabu hayo bila malipo. Isingekuwa busara kwa Mfuko wa Bima ya Afya kuendelea kulipa kitu ambacho tayari kimeshalipiwa na Serikali. (*Makofi*)

**MHE. ALI MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa mara ya kwanza kupata kuuliza swali la nyongeza.

**SPIKA:** Tangu lini? *(Kicheko)*

**MHE. ALI MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuuliza swali moja.

Kwa kuwa mfuko huu una dhamira nzuri tu ya kuwasaidia Wafanyakazi wa Serikali ili, waondokane na tatizo la kuweza kuhudumiwa wakati wanapopatwa na maradhi.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anajua kwamba kuna watu ambao wana miaka mitatu wanaumwa mara moja na wanakosa huduma na matokeo yake, fedha zao wanaendelea kukatwa?

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba inaweza ikawa ni jambo la busara wanaolipa fedha hizi wakaweza kuhudumiwa kwanza na baadaye wakalipwa hizo fedha na Wizara?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, dhana ya bima ndiyo hiyo kwamba fedha zinachangwa mwanzo, halafu matibabu yanatolewa pale mtu anapohitaji matibabu. Sasa kama nimeelewa vizuri suala la Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba fedha hizi zinakatwa kutoka kwenye mishahara kiwango cha asilimia 3 kwa kila mfanyakazi na Serikali inachangia asilimia 3, ili baadaye mfanyakazi anapougua yeye au familia yake aweze kupata matatibu bila ya kulazimika kutoa fedha taslimu.

Na. 98

## Tatizo la Maji – Nzega

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:

Kwa kuwa, Wilaya ya Nzega ni miongoni mwa Wilaya zenye ukame nchini na kwa kuwa, katika vijijini vingi bado kuna tatizo kubwa la maji safi na salama:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo?

(b) Je, Serikali iko tayari kuunganisha Wilaya ya Nzega, kwenye mtandao wa Ziwa Victoria?

**NAIBU WAZIRI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Teknolojia inayofaa kutatua tatizo la maji kwenye maeneo kame ikiwemo Wilaya ya Nzega, ni kuchimba visima virefu na kujenga mabwawa.

Serikali kwa kushirikiana na wahisani mbalimbali kama vile,*Oxfam*, *Water Aid*, *World Vision*, *TAHEA,* Makanisa ya *Anglican* na Moravian hadi kufikia Juni, 2004, wameshachimba visima virefu 10, visima vifupi 56 na kufunga pampu za mkono ili kupunguza tatizo la uhaba wa maji katika Vijiji vya Wilaya ya Nzega. Serikali ilitoa kiasi cha Shs 14,880,000/= katika mwaka wa fedha 2002/2003 ambazo zilitumika kuchimba na kujenga kisima katika Vijiji vya Mbongwe, Mwakabilu, Bujulu, Kili Sekondari, *Upungu Mission*, Nkiniziwa, Kipugala Shule ya Msingi na Mwamala.

Jumla ya pampu 18 za mkono zilinunuliwa na kati ya hizo 11 zilifungwa katika visima vilivyochimbwa na 7 zilizobaki zilitumika kufufua visima katika shule mbalimbali za msingi katika Tarafa za Bukene na Puge.

Katika mwaka wa fedha 2004/2005 Serikali imetoa shilingi milioni 20 kwa ajili ya ununuzi wa pampu 11 na ukarabati wa visima 11 katika Vijiji vya Kahama ya Nhalanga, Mbooga, Mhabala, Ululuma, Bukene, Ikindwa, Ntungulu, Mwanzoli, Idudumo, Mbagwa, na Tongi.

Aidha, tangu mwaka 2003 Serikali imekarabati malambo ya Ibako, Kabale, Mwasala, Idugila, Kabanga, Mabisilo na Mwansilo ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa ajili ya binadamu na mifugo katika wilaya ya Nzega.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho Serikali vile vile imefanya upanuzi wa mradi wa maji Nzega kwa kukarabati mabomba, mitambo ya kusukuma maji na vituo vya kuchotea maji. Bomba la maji limelazwa toka bwawa la Kilimi hadi Uchama ambako chujio limepanuliwa pia.

Mheshimiwa Spika, kasi ya kupunguza uhaba wa maji kwa Wilaya Nzega na Wilaya nyingine nchini itategeemea upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maji inayoelekeza wananchi kama walengwa wa miradi hii ya maji kushiriki kikamilifu katika kubuni, kupanga, kujenga na kugharamia uendeshaji wa miradi yao.

Serikali itaendelea kusaidia juhudi za wananchi kulingana na mahitaji yao na upatikanaji wa fedha katika kuondoa kero ya maji. Wananchi wanawajibika kuunda vyombo vyao vya kusimamia miradi ya maji pamoja na kuanzisha mifuko ya maji.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa kati ya vijiji 133 vilivyopo Wilayani Nzega, ni vijiji 47 tu vilivyokwisha unda Kamati za Maji na kuanzisha mifuko 46 ya maji yenye jumla shilingi milioni tano laki tatu na tisini na moja (5,391,000/=).

Namwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwashauri na kuwahamisha wananchi wa Wilaya ya Nzega kuongeza kasi ya kuunda Kamati za Maji na kuanzisha mifuko ya maji.

Na (b) Mheshimiwa Spika, mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya miji ya Kahama na Shinyanga umeanza kutekelezwa na uko katika hatua nzuri ya utekelezaji.

Mradi huu ambao unagharamiwa na Serikali yetu utaweza kupanuliwa katika siku za usoni na kuweza kuzinufaisha Wilaya na Vijiji vingine kama Serikali itapata fedha za kufanya hivyo. Wilaya ya Nzega na Wilaya nyingize jirani zitaweza kuunganishwa kwenye mtandao muda utakapowadia na fedha zitakapopatikana.

Na. 99

**Huduma ya Maji – Vijiji vya Babati Magharibi**

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza:-

Kwa kuwa Sekta ya Maji ni mojawapo ya maeneo yaliyopewa kipaumbele katika kuondoa umaskini na kwa kuwa wananchi wa Gidewari, Birsima na Endadu katika Kata ya Dabil kwa muda mrefu hawana huduma ya maji kutokana na maeneo hayo kuwa na chumvi na hivyo uchimbaji wa visima kutofaa kabisa.

Je, Serikali sasa inawasaidiaje wananchi wa maeneo niliyotaja ili waweze kupatiwa huduma ya maji?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO) **alijibu:-**

**Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Babati Magharibi, kama ifuatavyo:-**

**Ni kweli kwamba maeneo ya Gidewari, Birsima na Endadu ambayo ni vitongoji katika kijiji cha Mandi Kata ya Dabil, Tarafa ya Bashnet, Wilaya ya Babati, vina shida ya maji kutokana na vyanzo vilivyopo kutoa maji yenye chumvi kiasi cha kutofaa kwa matumizi ya nyumbani.**

**Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Babati imekuwa ikifanya tafiti za kupata vyanzo vya maji yanayofaa kwa matumizi ya binadamu katika maeneo hayo. Kadhalika, wananchi wa eneo hilo kwa kushirikiana na asasi ya kidini ya Jimbo Katoliki la Mbulu nao walifanya utafiti wa visima vifupi mwaka 1998, lakini utafiti huo nao haukuzaa matunda makubwa kutokana na chumvi nyingi iliyopatikana kwenye vyanzo hivyo.**

**Chanzo kimoja cha chemchem ndogo kilipatikana na kulifanya Jimbo Katoliki la Mbulu kujenga mradi wa km 3 katika eneo la kitongoji cha Gidewari, mradi ambao unahudumia sehemu ndogo yenye Kaya 55 kati ya Kaya 190.**

**Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi nilizozitaja hapo juu Serikali kwa kushirikiana na wananchi hao na wadau wengine itaendelea kutafuta ufumbuzi wa tatizo la upatikanaji wa majisafi na salama katika vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge. Wananchi wa maeneo hayo wanashauriwa kuendelea kuchangia mifuko yao ya maji ili kuwawezesha kugharamia, kutunza na kuendesha miradi yao ya maji.**

SPIKA: **Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, tunaendelea na matangazo ya vikao vya leo. La kwanza Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Alhaj Shaweji Abdallah, anawatangazia Wajumbe wa Kilimo na Ardhi kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo tarehe 20 saa 5 asubuhi chumba Na. 219 ghorofa ya pili.**

**Kamati nyingine ni ya Miundombinu. Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, kwa niaba ya Mwenyekiti, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kwamba leo tarehe 20 Juni, 2005 saa 7 mchana kutakuwa na Mkutano katika ukumbi Na. 227, ghorofa ya pili, kupitia Taarifa na Maoni ya Kamati ya Miundombinu.**

**Halafu kile chama cha *Amani Forum* cha Wabunge, kwa niaba ya Mwenyekiti Mheshimiwa Ibrahim Marwa, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya *Amani Forum* kuwa leo tarehe 20 saa 5 asubuhi watakutana katika ukumbi Na. 227. Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper.***

## KAULI ZA MAWAZIRI

### KAULI KUHUSU SUALA LA WAKAZI WA KIJIJI CHA RWAMCHANGA ENEO LA NYAMUMA WILAYANI SERENGETI

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: **Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa Kauli ya Serikali kuhusu suala la wakazi wa eneo la Nyamuma iliyobaki au kwa jina lingine *CCM Center* katika Kijiji cha Rwamchanga Wilayani Serengeti. Kama Bunge lako Tukufu linavyofahamu suala hili tayari linashughulikiwa, limeshughulikiwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na sasa limefikishwa Mahakamani.**

**Natambua kuwa moja ya misingi mikubwa ya Katiba yetu na Kanuni za Bunge lako Tukufu ni ule unaotaka kwamba suala ambalo tayari liko Mahakamani lisizungumziwe nje ya Mahakama. Hivyo sina mpango wa kulizungumzia suala hili katika upana wake bali nitaligusia tu kwa kiwango ambacho kinagusa suala zima la amani na utulivu katika eneo hilo la mgogoro na Wilaya ya Serengeti kwa ujumla.**

**Mheshimiwa Spika, Serikali inaona upo umuhimu wa kulitolea ufafanuzi suala hili katika muda huu kutokana na jinsi ambavyo suala lenyewe limekuwa likipotoshwa na baadhi ya Taasisi zikiwemo za Wanaharakati wa Haki za Binadamu, kwa kutoa madai yasiyo na msingi kwamba Serikali inawatesa na kuwadhulumu kwa njia ya kijeuri wananchi wa Wilaya ya Serengeti na hivyo kuleta taswira tofauti na hali halisi ilivyo.**

**Mheshimiwa Spika, historia ya suala hili. Hali ya ulinzi na usalama katika maeneo kadhaa ya Mkoa wa Mara ilianza kuwa na matatizo tangu mwaka 1980 hasa kutokana na kuzagaa kwa wingi wa silaha haramu na wizi wa mifugo**

**ulioambatana na ujambazi wa kutumia silaha hasa baada ya vita ya kumng'oa Nduli Iddi Amini kumalizika. Ingawa ni kweli kwamba tatizo la wizi wa mifugo lilikuwepo hata kabla ya hapo wakati huo tatizo hilo lilikuwa linajikita zaidi kwenye mila ya Sosaro iliyoko katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Mara ambako baadhi ya jamii huamini kuwa mwanaume hawezi aliyekamilika hadi aingie jando na mara baada ya zoezi hilo kufanyika ili kuwathibitishia hilo wahusika huiba ng'ombe wachache wakati wa usiku na wengine kunyemelea machungani na kufunga ng'ombe kinywa ili waweze kuwasafirisha usiku bila kupiga kelele.**

**Lakini katika miaka ya 1980 wizi wa mifugo ulibadilika sura na mbinu. Wizi ulianza kuwa wa kibiashara zaidi na soko kubwa la ng'ombe wa wizi likawa ni nchi jirani. Nitarudia sehemu hiyo, wizi ulianza kuwa wa kibiashara zaidi na soko kubwa la ng'ombe wa wizi likawa ni nchi jirani Kaskazini mwa Mkoa wa Mara. Katika Wilaya ya Tarime na hususan Tarafa ya Ingwe, Imchungu, Imchage na Iwano na kwa upande wa Wilaya ya Serengeti, Kata ya Mgumu Vijijini hali ya usalama ilikuwa ya kutisha sana. Hali hiyo iliyotokana na wimbi la wizi wa mifugo ulioambana na ujambazi lilizusha zogo la uhasama wa koo miongoni mwa koo mbalimbali katika maeneo hayo.**

**Koo hizo zilijiona kama vile nazo ni Serikali na zikaanzisha majeshi yake. Katika kipindi hicho walijitokeza majemedari wa kila ukoo waliokuwa wakiongoza vikundi vya ujambazi vilivyokuwa vikiiba mifugo kutoka ukoo mmoja na kupeleka ukoo mwingine. Kwa bahati mbaya uwezo wa Polisi Mkoani wa kudhibiti hali hiyo ilikuwa ni ndogo kutokana na uchache wa askari wa kukabiliana na matukio ya uhalifu, hali ya usafiri kuwa duni na ukosefu wa mawasiliano. Hali hiyo ilitoa mwanya kwa majambazi kuzidi kutamba na kuitangazia Serikali uwezo wao. Wananchi nao kwa upande wao wakaanza kusema kuwa Serikali ilikuwa imekwenda likizo.**

**Mheshimiwa Spika, machafuko hayo yalitokana na mapigano ya ukoo na ukoo pamoja na wizi wa mifugo ulioambatana na matumizi ya silaha yalileta athari kubwa katika jamii hususan katika Wilaya ya Serengeti. Inakisiwa kuwa watu wasiopungua 250 walipoteza maisha yao. Shule na Zahanati katika maeneo mengi Wilayani humo zilifungwa na kuacha wananchi bila huduma ya afya. Aidha ng'ombe wasiopungua 25,548 walivushwa nje ya Mkoa wa Mara kati ya mwaka 81 na 87. Hivyo, kutokana na hali ya kiulinzi na usalama kuwa mbaya katika Mkoa wa Mara kati ya mwaka 81 na 86 Serikali ililazimika kuendesha Operesheni ya Jeshi la Polisi zisiyopungua 7 ambazo baadhi yake zilishirikisha Jeshi la Wananchi Tanzania.**

**Ooperesheni hizo ambazo zaligharimu fedha nyingi zilifanikisha kupatikana kwa silaha nyingi na risasi pamoja na kukamatwa kwa wezi wazoefu na majambazi maarufu waliokuwa tishio kwa maisha ya raia na mali zao na hivyo kurejesha tena**

**hali ya amani na utulivu katika Mkoa wa Mara hususan Wilaya ya Tarime na Serengeti na pia kurejesha imani ya wananchi kwa Serikali yao.**

**Aidha, kwa kutambua kwamba suala la ulinzi na usalama ni la wananchi wenyewe, mwaka 1986 Jeshi la Polisi lilianza kushirikisha Mabaraza ya Jadi, Ritongo katika utambuzi wa wahalifu kuwakamata na kuwafikisha mbele ya vyombo vya haki.**

**Mheshimiwa Spika, kwa ujumla operesheni mbalimbali za kupambana na uhalifu zilizofanywa na Serikali Mkoani Mara pamoja na ushirikishwaji wa Mabaraza la Jadi na walinzi wa jadi katika Wilaya ya Tarime na Wilaya ya Serengeti ndicho kilichowezesha Serikali kurejesha tena hali ya usalama na utulivu hadi kufikia hatua ya Mkoa wa Mara kutoka katika nafasi ya kwanza kitaifa kwa matukio ya uhalifu hadi kufikia nafasi ya tisa kitaifa mwaka 2003.** ***(Makofi)***

**Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa historia hii fupi kwa sababu inaamini ni muhimu katika kuelewa chimbuko ya malalamiko yaliyofikishwa mbele ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.**

**Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 Serikali Mkoani Mara iliendesha operesheni ya kung'oa na kutekeza zao haramu la bangi. Operesheni hiyo iliwashirikisha pia Sungu Sungu. Wakati wa Operesheni hiyo, ilijitokeza hisia kwamba Sungu Sungu wa ukoo wa Remchoma waling'oa mashamba ya bangi ya ukoo wa Mchari. Hatua hiyo ilianzisha chuki na uhasama mkubwa kati ya koo hizo mbili na kusababisha mwezi Julai, 2001 kuibuka kwa mapigano kati ya ukoo wa Waranchari na ukoo wa Waranchoka. Mapigano hayo yalipoteza maisha ya watu 13, jumla ya nyumba 428 zilichomwa moto sambamba na kusababisha watu 556 kukosa makazi. Ili kukabiliana na ghasia hizo Jeshi la Polisi lilifanya operesheni ndogo ya kumaliza mapigano ya koo hizo mbili, baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kutembelea eneo hilo tarehe 24 Septemba, 2001 Serikali iliagiza kuwa ardhi iliyokuwa ikigombaniwa na koo Wamchari na Waremchoka na Wakira ichukuliwe na Serikali.**

**Baadhi ya familia za ukoo wa Remchoka zilizokumbwa na hatua hiyo ya Serikali zilihama kutoka Wilaya ya Tarime na kwenda kuishi katika Wilaya ya Serengeti katika maeneo yaliyokuwa tayari yanakaliwa na ukoo wa Waranchoka. Hatua za wahamiaji hao ambao baadhi yao walikuwa wamevuka kutoka nchi jirani zilisababisha msongamano mkubwa wa watu katika maeneo waliyohamia huko Wilayani Serengeti. Baadhi yao hata walidiriki kwenda kuishi katika maeneo ambayo tayari yalikwisha tangazwa na Serikali kuwa ni pori la akiba yaani *Game Reserve* kama vile eneo la Ikorongo.**

**Uhamiaji huu wa mwaka wa 2001 wa ukoo wa Waranchoka kutoka Wilaya ya Tarime na kukimbilia Wilaya ya Serengeti ulikuwa ni wa awamu tatu, ukitanguliwa na uhamiaji wa miaka ya 80 na ule uliofanyika mwaka 92 na mwaka 94 ambao nao kiini chake kilikuwa mapigano ya kiukoo. Kutokana na msongamano mkubwa wa watu katika maeneo yaliyovamiwa pamoja na milipuko ya mapigano na mauaji ya mara kwa mara. Serikali ilikitoa maagizo ya kuwataka wavamizi hao waondoke na warejee kwenye maeneo yao ya asili Wilayani Tarime.**

**Lakini nyakati zote maelekezo hayo yalipuuzwa na wananchi hao. Kabla ya zoezi lililolalamikiwa la kuwaondosha wavamizi hao kutoka kwenye eneo la mgogoro kutekelezwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Serengeti iliwasilisha kwenye ngazi ya juu za uongozi Mkoani Mara, taarifa yake kuhusu hali mbaya ya usalama katika eneo hilo. Kutokana na Taarifa hiyo, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa katika kikao chake kilichofanyika tarehe 5 Octoba, 2001 baada ya kujadili kwa undani hali ya usalama iliyokuwa katika eneo la Nyamuma iliyobaki, iliagiza watu wote waliovamia eneo la Kijiji cha Rwamchanga na kuibatiza eneo hilo jina la Nyamuma iliyobaki waondoke na warejee kwenye maeneo yao ya asili.**

**Baada ya muda waliopewa wa kuondoka kwa hiari yao kwisha uamuzi wa Serikali ulitekelezwa kwa operesheni ya kuondoa wananchi hao kutoka katika maeneo ya kijiji cha Rwamchanga au kwa jina lingine Nyamuma iliyobaki au *CCM Center* Wilayani Serengeti ambayo walikuwa wameivamia. Hatua hiyo ya Serikali ndiyo iliyokuwa chimbuko la malalamiko yaliyofikishwa mbele ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na wananchi wapatao 135.**

**Mheshimiwa Spika, ni vema ikakumbukwa kwamba hata kabla ya zoezi hilo la kuwaondoa wavamizi hao kutoka kwenye eneo la mgogoro kuanza kutekelezwa na Serikali tayari kulikuwepo na uamuzi halali wa Mahakama Kuu uliotokana na shauri lililofunguliwa na baadhi ya wananchi hao ya kupinga kuondolewa kwao katika pori la akiba la Gurumeti na Ikolongo. Katika shauri hilo Na. 24 la mwaka 1997 Mahakama Kuu iliagiza yafuayayo:-**

**Mosi, wadai hao walipwe na Serikali fidia ya shilingi milioini 114,085,115 kwa mali zao. Pili, baada ya fidia hiyo kulipwa wadai waondolewe kwenye eneo la mgogoro ndani ya siku 30 ambalo inavijumuisha vijiji vya Nyamuma na Gurumeti ambavyo vimo ndani ya pori la akiba la Gurumeti na Ikolongo.**

**Tatu, wadai, hawa wahamishwe katika vijiji vya Romeo, Kwamchanga, Mashangura, Kwiteta, Machuri, Rungabure na Nyasirori. Nne, wananchi watakaopenda kurejea kwenye maeneo yao asili waruhusiwe kufanya hivyo na**

**mwisho baada ya muda wa siku 30 kwisha wananchi hao waondoshwe kutoka kwenye maeneo ya mgogoro.**

**Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia amri hiyo ya Mahakama na baada ya wananchi wa vijiji vya Nyamuma na Gurumeti kulipwa Serikali ilitoa ilani ya kuwataka wawe wamekwishaondoka katika eneo hilo pindi muda wa siku 30 wa ilani utakapomalizika.**

**Mheshimiwa Spika, baadala ya kwenda kwenye maeneo waliyopangiwa kwa msingi wa amri ya Mahakama Kuu au wao wenyewe kurejea kwenye maeneo yao ya asili baadhi ya walalamikaji katika shauri hilo waliamua kulivamia eneo la kijiji la Rwamchanga na kama ilivyokwishaelezwa na kuliita eneo hilo Nyamuma iliyobaki au *CCM Center.* Hali hii ilisababisha kuzuka tena kwa vurugu na mapigano kati ya wanakijiji wa Rwamchanga na wavamizi hao.**

**Kama ilivyoelezwa hapo awali uvamizi huo wa Waremchoma katika Wilaya ya Serengeti na ukaidi ulioonyeshwa na wananchi hao kwa kudharau uamzi wa Mahakama uliulazimu Serikali Mkoani Mara mnamo tarehe 5 Octoba, 2001 kuagiza wavamizi hao waondolewe mara moja kutoka katika maeneo kwenye eneo hilo la mgogoro.**

**Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inaheshimu sana Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Tume hiyo ni asasi muhimu sana katika kudumisha Utawala Bora na Utawala wa Sheria nchini. Serikali wakati wote inaheshimu sana haki za binadamu na inaizingatia.**

**Aidha, Serikali inatambua na kuheshimu sana haki na uhuru wa raia wa kwenda kuishi popote nchini ili mradi wazingatie Sheria, Kanuni, Taratibu zilizowekwa na waishi kwa amani na utulivu. Hivyo Serikali itafanya kila iwezekanavyo kulinda maslahi ya jamii kwa kuhakikisha watu wake wanaishi kwa amani na utulivu.**

**Baada ya Tume kuwasilisha taarifa yake Serikali yalifanyika mashauriano mapana na ya kina yaliyohusisha uongozi wa Mkoa wa Mara na Mamlaka nyingine za Serikali kuhusu taarifa hiyo.**

**Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati uongozi wa Mkoa wa Mara pamoja na viongozi wa vyombo na Idara mbalimbali za Serikali kwa mchango wao mkubwa ambao umewezesha**

**Serikali kuchambua kwa kina mapendekezo ya Tume na hivyo kuwezesha kutoa msimamo wa Serikali kuhusiana na taarifa hiyo ya Tume.** ***(Makofi)***

**Mheshimiwa Spika, maamuzi ya Tume yaliyotolewa yalikuwa katika sehemu saba tofauti. Kwa kuwa suala hili lipo Mahakamani sitajiekeleza kwa undani katika maamuzi ya Tume. Nitajielekeza tu katika suala zima la amani na utulivu ambayo ndiyo nguzo muhimu katika maendeleo ya nchi yetu hususan nitajielekeza katika eneo moja la mapendekezo ya Tume nalo ni lile la kuelekeza kuwa Serikali ya Kijiji cha Mbomchugu na Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti iwarudishe haraka iwezekanavyo walalamikaji kwenye maeneo yao yaliyoko kwenye eneo la mgogoro.**

**Mheshimiwa Spika, msimamo wa Serikali katika eneo hili ni kuwa pendekezo hilo halitekelezeki na kwamba walalamikaji waliofika mbele ya Tume hawakuwa wakazi halali wa Nyamuma. Walalamikaji hao walikuwa wavamizi wa eneo hilo.**

**Mheshimiwa Spika, tangu wavamizi hao waingie kwenye eneo hilo lenye mgogoro zimejitokeza vurugu na mapigano ya mara kwa mara kati ya wavamizi hao na wakazi halali wa kijiji Rwamchanga ambayo yamesababisha vifo vya watu saba wenyeji wa kijiji hicho. Katika ripoti ya Haki ya Tume imekiri na kuthibitisha kuwepo kwa vurugu na mauaji hayo ya watu saba katika kijiji cha Rwamchanga. Lakini la kushangaza ni kwamba Tume inadai kwamba mauaji hayo si lolote wala si chochote eti kwa sababu hayakuwa mauaji ya halaiki.**

**Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kuwahakikishia wananchi wote kuwa maisha ya binadamu bila kujali idadi ni lulu yenye thamani kubwa isiyopimika na inayostahili kulindwa kwa gharama yoyote ile na hasa kwa kuelewa kuwa kuwarejesha wavamizi katika eneo husika kama inavyopendekezwa na Tume kutasababisha machafuko, vurugu, mapigano na umwagaji wa damu. Serikali inaamini kuwa itakuwa ni Serikali isiyojali wananchi wake, iwapo itawaruhusu wavamizi hao kurejea kwenye eneo la mgogoro kwa sababu amani na utulivu uliyopo hivi sasa utatoweka. Mauaji yanaweza kutokea tena, Serikali isingependa hali hiyo itokee.**

**Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kusisitiza kwamba uamuzi wake wa kuwaondoa wananchi hao kutoka kwenye eneo la kijiji cha Rwamchanga, vijiji vya Nyamuma na Guruneti ulizingatia mambo yafuatayo:-**

**Amri moja ya Mahakama Kuu iliagiza wananchi hao wahamie katika maeneo ya vijiji walivyopangiwa au warejee kwenye vijiji vyao vya asili badala ya**

**kuhamia kwenye vijiji walivyopangiwa wananchi hao walichukua sheria mikononi mwao na kuvamia kijiji cha Rwamchanga pamoja na pori la akiba *Game Reserve* la Ikolongo hali ambayo ilisababisha kuzuka upya vurugu na hivyo kutishia usalama na utulivu wa eneo hilo. *(Makofi)***

**Pili, maagizo ya Serikali yaliyotaka watu wote wasio raia wasakwe na kurudishwa makwao. Baadhi ya watu hao baada ya kurejeshwa katika nchi moja jirani walirejea kimya kimya katika eneo hilo la mgogoro. *(Makofi)***

**Tatu, agizo la Serikali lililotaka watu wote waliovamia maeneo ya vijiji vya Gurumeti, Nyamuma na Rwamchanga waondoshwe kutoka kwenye maeneo hayo ya mgogoro ili kuepusha vurugu, mapigano na mauaji.**

**Mheshimiwa Spika, Tume yenyewe katika ripoti yake imekiri na kuthibitisha kuwa baadhi ya walalamikaji walihamia ndani ya eneo la Kijiji cha Rwamchanga tangu mwaka 1986 wakitokea sehemu mbalimbali kama vile vijiji vya Garawani na Machochowe na Wilaya ya Tarime.**

**Tume pia imebainisha kwamba watu hao waliondoka katika maeneo yao ya asili kutokana na migogoro na mapigano ya kiukoo na kwamba wakati huo eneo hilo la mgogoro lilikuwa chini ya uongozi wa kijiji cha Mwamchanga.**

**Mheshimiwa Spika, Serikali ilitegemea kuwa baada ya kukiri na kuthibitisha hilo Tume ingeona busara kutolitolea pendekezo lolote suala nyeti na tete kama hili la ardhi kwa sababu kama taarifa yake inavyosema vipo vyombo mahususi vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria kushughulikia masuala ya ugawaji wa ardhi. *(Makofi)***

**Mheshimiwa Spika, kwa sababu wananchi waliolalamika mbele ya Tume walikuwa wamekalia maeneo ya kijiji cha Rwamchanga bila kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia uhamiaji katika maeneo ya vijiji, Serikali iliwajibika kuwaondoa.**

**Pia baada ya zoezi la kuwaondoa walalamikaji hao kukamilika, eneo husika liligawiwa kwa wananchi wengine kulingana na mahitaji yao. Hivyo kitendo cha kuwarudisha walalamikaji kwenye eneo hilo kama ilivyopendekezwa na Tume bila shaka kutaibua upya vurugu, ghasia na mapigano na hivyo kuhatarisha amani na utulivu katika kijiji cha Rwamchanga.**

**Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kwa ujumla kwamba Serikali haina nongwa na Tume. Kutotekeleza pendekezo la Tume na kuwarejesha watu hao kwenye maeneo, hilo ni kusimamia maslahi ya umma.** ***(Makofi)***

**Hivyo, Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kuwaasa wananchi wenye nia na matamanio ya kuanzisha makazi mapya katika maeneo ya vijijini na mijini kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo kuhusu makazi.**

**Mheshimiwa Spika,** ni vema tukaendelea kuenzi amani na maendeleo yaliyopatikana kwa gharama kubwa ili kudumisha usalama na utulivu nchini hususan katika Wilaya ya Serengeti na Mkoa wa Mara kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, serikali kama mdau na muhimili mkuu amani na utulivu hapa nchini haiko tayari kuona hali ya usalama, amani, utulivu iliyosheheni kote nchini na hususan Wilayani Serengeti **na Mkoa wa Mara kwa jumla ikivurugwa na kutolewa kafara kwa kisingizio chochote kile, kama alivyotuasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, wakati anawasilisha hotuba yake ya Bajeti juzi, nanunukuu:**

**"Utawala bora unakuwepo kwa sababu kuna amani, hivyo tahadhari yangu kwa Watanzania wote ni kuwa kama tunataka mafanikio yoyote tunayoyaona yayeyuke tuchezee amani yetu. Amani yetu ni mali ya Watanzania wote na siyo mali ya viongozi wala mtu yeyote". Mwisho wa kunukuu.** ***(Makofi)***

Mheshimiwa Spika, napenda niongezee katika nukuu hiyo ya wiki kwa kusema imani yetu sio mtaji binafsi wa mwanaharakati wa haki za binadamu wala wa chombo chochote. Naomba Watanzania wote tuendelee kuenzi amani yetu tuidumishe, tuilinde kwa nguvu zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. KHERI KHATIBU AMEIR:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nitoe shukrani za dhati kunipatia nafasi hii nami kuwa mmoja kati ya wachangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Lakini vilevile naomba kukupongeza Mheshimiwa Spika, kwa muda wote huu miaka kumi iliyokuwa imepita kuongoza Bunge hili na katika hali ya kwamba ya maelewamo kufahamiana na vilevile katika hali ya utulivu ni tofauti labda na Mabunge mengine yanayotokea tunayaona watu wanarushiana viti kama yanavyotokea katika nchi jirani twakupongeza sana Mheshimiwa Spika.

Naomba vile vile kutoa pole kwa vifo vilivyotokea kwa marehemu Abu Kiwanga, wa Jimbo la Kilombero na Mheshimiwa Diria Hassan wa Jimbo la Rahaleo, tunawapa pole wapiga kura wao wote pamoja na familia zao na tunaziombea roho za Marehemu Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema peponi, Amen.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwasilisha hotuba yake hapa alianza na kumsifu Mheshimiwa au kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Tanzania kwa uongozi wake thabitiwa miaka kumi, na mimi naungana naye kumpongeza Mheshimiwa Rais Benjamini Mkapa, kwa ujasiri alionao na uwezo mkubwa Mwenyezi Mungu aliompa wa kuiongoza nchi hii katika hali ya utulivu na hali ya amani na hasa kwa kusimamia uendelevu wa uchumi wan chi hii.

Lakini vilevile nimpongeze kwa kuwa ni mmoja katika kiungo kikubwa cha kuunganisha baina ya Tanzania na ulimwengu tulio nao. Nimpongeze Rais Mkapa kwa kuchaguliwa kama Mwenyekiti wa Tume ya Blair ambayo ni Tume iliyoteuliewa kuweza kusimamia masuala ya umaskini au kwa maendeleo za nchi ya kiafrika.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze vilevile Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Mkapa kama Mwenyekiti, wa Chama cha CCM chama tawala namna walivyokuwa uendeshaji uchaguzi na mchakato ulivyokwenda kwa kuchaguliwa Rais mtegemewa wa Tanzania. Uchaguzi uliokuwa umepita katika miezi miwili iliyopita, na katika mchakato huo huo naomba niwapongeze wale wateuliwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete pamoja na Mheshimiwa Amani Abeid Karume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ulivyozungumza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitoa maelezo mengi sana na kwa bahati nzuri ilichukua muda kama saa mbili hivi, na wewe kwa busara zako ulisema kwamba hotuba hii hukumuwekea mipaka Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hata sisi tukafikiri labda inawezekana itachukua hata saa tatu au saa nne, lakini bahati nzuri ilichukua masaa mawili. Lakini yenyewe ilikuwa ina maudhui ya utendaji wa miaka kumi iliyokuwa imepita tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ile yenye page 85 ilikuwa kama ningejiandaa vizuri hata kueleza ilikuwa mistari mingapi lakini hakukuwa na suala moja la wazi lililokuwa limejitokeza, suala la muungano. Kama watanzania, kama Bunge hili la Tanzania suala la muungano ni suala mama au ni suala muhimu sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema maneno machache tu lakini hakutoa mwelekeo kama vile alivyotoa mwelekeo wa kiuchumi, au hakutoa dira kama vile alitoa maelezo ya usalama na amani katika nchi yetu kama ambavyo tulitegemea angekuwa ametamka maneno mazuri katika suala hilo. Tunamuomba Rais ajaye na Waziri Mkuu ajaye hilo suala nalo hilo awe analijali na analiweka mahali pake.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni moja katika mapungufu yaliyokuwepo lakini si kwamba mapungufu hayo yaliharibu ladha na uhakiki na ukweli wa hotuba yenyewe au na uongozi wenyewe kwa muda huo ulikuwa umepita. Yaliyojitokeza kama ni upungufu vilevile ambayo sisi yalitugusa mfano katika kusherekea miaka 41 ya Muungano, sherehe iliyokuwa imefanyika uwanja wa Jamhuri Dodoma tuliona viongozi kutoka Zanzibar, walikuwa wamefuatana na Mheshimiwa Rais, Mawaziri wakina Shamhuna na wengine walivyokuwa wanababaika pale hata pale mahali pa kuka walikuwa wanatafuta wanababaika hawakutengewa mahali mahsusi.

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba Ofisi ya Waziri Mkuu na Watendaji masuala kama yale kwa masuala ambayo yanakuwa yanaleta dosari katika hali nzima ya uongozi mzuri aliokuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waziri Mkuu vilevile tungemuomba ajaye ajitahidi na dosari zilizokuwa zimejitokeza katika matumizi ya Serikali katika Halmashauri zetu katika wilaya. Tunayoyakuta madosari mengi yanatokea, madhambi mengi yanatokezea lakini baada ya ripoti kutolewa za upungufu unaojitokeza hatusikii taarifa gani au hatua gani zimechukuliwa dhidi yao, inawezekana kwamba zimechukuliwa kimya lakini ni vizuri Bunge lako nayo tukawa tunaelezwa, kwa sababu taarifa zile zinakuja hapa na tunaelezwa matokeo ya hatua hizo. Kwa hiyo, tuelezwe hatua za wale korofi na wale waliokuwa wanachafua utendaji katika wilaya au katika Halmashauri, wale ambao pesa anazivuruga katika Halmashauri, tuelewe ni hatua gani zinachukuliwa dhidi yao. Kama tunavyofahamu kwamba pesa nyingi sasa zimekuwa zinakwenda katika Halmashauri, Bunge hili linahidhinisha pesa nyingi na Bunge hili linategemea kwamba yale yanayoidhinishwa na hali wanategemea kwamba yatatendeka katika mawilaya yanatekelezwa. Kinyume chake Waheshimiwa Mawaziri mara nyingi masuala yanapokuja wanasema kuwa hili suala Halmashauri ndio watakao tekeleza na kweli pesa inapelekwa katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, tunaomba masuala haya nayo tuzingatie katika miongo na siku za baadaye zinazokuja. Nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikutaja maendeleo makubwa yaliyokuwa yamepatikana katika masuala ya barabara, mawasiliano, maji, elimu na mengi mengineyo, na haya yalitekeleza. Mafanikio haya yametokana kutokana na usimamizi mzuri uliokuwa umefanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo tuliyokuwa tumeyazungumza ya uchumi, tunampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba nchi yetu miaka kumi iliyopita, ukusanyaji wa mapato umekuwa kutoka kutoka bilioni 26 mpaka sasa kufikia bilioni 160 kwa mwezi. Lakini tumpongeze vilevile kwa usimamizi wake wakati wote muda ulikuwa mmepita huo kwamba vilevile imeonekana kwamba uchumi umekuwa kwa kiasi cha kupigiwa mfano katika Afrika na wa kuigwa katika dunia. Kwa hiyo nayo tunampa

hongera sana na tunamtakia Mheshimiwa Waziri Mkuu anakokwenda aende salama na inshallah tuko pamoja naye.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi uliyonipa ya kuchangia Hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami ya kuweza kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote naomba kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri, pili kuwashukuru Mawaziri wote wa SERA ambao wako katika Wizara yake na kuwaweza kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Pili naweza kumshukuru Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuweza kufanya kazi yake vizuri na watendaji wake kuleta Miswada. Naweza kumshukuru pia Mheshimiwa Waziri kaka yangu Lukuvi kwa kazi nzuri ambayo ameifanya. Namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Andrew Chenge kwa miaka mitano yote ambayo tumeshirikiana naye kwa kuweza kuleta Miswada kwa muda muafaka na kwa kazi nzuri ambayo ameifanya yeye na watendaji wake kwa kutokupata usingizi usiku na mchana ili kuweza kufanikisha shughuli za Serikali katika Bunge.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuweza kuchangia katika hotuba hii katika nafasi ya *TASAF*, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Benjamini Mkapa, kwa kuweza kuleta utaratibu wa *TASAF* ili kuweza kuwasaidia wananchi maeneo husika. Lakini utaratibu huu ni mzuri kuweza kuwasaidia wananchi inahitajika iweze kupatikana elimu kwa wananchi ili waweze kuelewa *TASAF* ni nini ambacho kinatakiwa wafanye wao na Serikali imeamua kuwapa madaraka wao wenyewe kuamua zile kero ambazo wanaona zinawakera maeneo husika. Itakuwa ni vizuri zaidi kama Serikali itatumia vyombo vya habari ili kuweza kuwaelimisha wananchi. Nilipata tabu sana kuweza kusikia katika Bunge hili kuna mmoja akichagia au akijibu hoja katika Bunge akisema kuwa *TASAF* ni utaratibu ambao unawasaidia kuwakopesha wananchi, nikasema kama sisi wenyewe inatukwaza kuelewa *TASAF* si mkopo sasa je wananchi wetu watapata kuelewa kwa namna gani? Laiti wakielewa kuwa *TASAF* si mkopo ila ni utaratibu ambao unawasaidia itawasaidia zaidi kwa kuweza kupata elimu wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ni suala la Tume ya Madini, uliandaliwa Tume ya Madini ambayo inayoshughulikia utaratibu mzima wa kubadilisha sera ambazo tumeziona sera zinakuwa zina upungufu. Tume hii imeundwa na karibu sasa ni miezi sita toka imeundwa, lakini je, nini ambacho kilichofanyika katika Tume hii mpaka sasa, mpaka sasa hakuna majibu yoyote ambayo yaliyoletwa katika Bunge au Serikali inajibu nini kuhusu suala la Tume hii kubadilisha sera. Matokeo yake napata kigugumizi sana kwa kupata tabu kuona wale walioiandaa sera mara ya kwanza, ndio hao ambao unajikuta ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume hii. Sasa huyu Mwenyekiti ambaye wakati anaandaa sera aliziandaa na kuelewa kuwa kile alichokiandaa ni sahihi na hakitohitaji kuletewa mabadiliko, na sisi tumekiona kuwa si sahihi kinahitaji kubadilishwa. Lakini katika kubadilishwa kwake yule yule aliyekiandaa ndiyo anakuwa Mwenyekiti, sasa yeye mwenyewe ni mhalifu, na yeye mwenyewe ni jaji na yeye mwenyewe ni hakimu. Kwa hiyo, hii mimi inanisumbua sana kuelewa je tukishaletewa zile sera sisi tutazipokeaje.

Pengine zinaweza zikawa ni nzuri lakini kutokana na kukwaza tu katika sehemu moja ambayo ya Mwenyekiti hiyo inakuwa ni kitu ambacho kitakuwa ni kigumu kidogo. (*Makofi*)

Lakini la pili, katika kuandaa sera lazima tuwe tunashirikisha maeneo husika au watendaji, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya au Wabunge. Lakini katika sera hii alishirikishwa Mkuu wa Mkoa mmoja je, sisi ambao watu wa Tabora tunamadini pale, viongozi wetu wa Bunge, Mkuu wa Mkoa wetu hajaweza kushiriki kule hii inakuwa ni sera ya aina gani ambayo ya kushirikisha Tume tu bila kuweza kushirikisha wale watu wa maeneo husika. Hiyo ni mojawapo ambayo inaonekana kuwa hizi sera zinazoundwa zinakuwa ni sera za mficho ambazo haziweki wazi kuwapa uhuru wale washiriki ili na wao waweze kutoa mawazo yao. Mfano kuna Tume ambayo tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu baada ya kumshauri na mimi mwenyewe ninakumbuka nilizungumza kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu katika muda wako huu wote wa miaka mitano au kumi uweze kuunda Tume ambayo itashughulikia mishahara ya walimu, na alifuata mawazo hayo kwa Wabunge wengi ambao walitoa mawazo na baadaye Tume hiyo ikaundwa.

Sasa toka Tume hiyo imeundwa nini ambacho kilichofanyika mpaka sasa, yako maeneo ambayo yaliyofanyika katika Mikoa lakini kwenye Bunge hili haijaletwa Tume imetoa maamuzi gani na ushauri gani katika Bunge au imetoa maamuzi gani, ushauri gani na mahojiano ya namna gani, ili kuweza kuwashughulikia wale ambao wameweza kuonekana wabadilifu na wamefanyiwa kitu gani, mimi napata shida kuelewa kuwa zinaundwa Tume, Tume maana yake ni nini na kwa nini zinaundwa, zinaundwa ili baadaye ziweze kuleta majibu kwetu hapa Bungeni au kwa wananchi waelewe Tume imeundwa matokeo yake ni nini na utekelezaji wake ni wa aina gani. Lakini zikiundwa Tume zikawa Tume zilizokuwa katika kifurushi kilichofungwa bila kufunguliwa hizo zinakuwa ni Tume ambazo zinatutia wasi wasi zaidi kwa kuundwa Tume. Ni bora msiwe mtangaza kuwa tunaunda Tume, bora muwe mnasema kuwa tunaandaa utaratibu wa kuweza kufuatilia, bila kusema Tume, Tume maana yake mtuletee majibu tuweze kuelewa nini ambacho mmekifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mawasiliano, katika mkoa wetu wa Tabora tunashukuru mawasiliano tumepata, lakini kuna wilaya moja ya Sikonge, mwaka jana walituambia mwaka jana walituambia mwezi wa tisa msiwe na wasi wasi. Mimi Mbunge wa Viti maalum wa Vijana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo tukaenda kwa kifua mbele kabisa kuitisha mkutano wa wananchi, tukawaambia nyie jiandaeni kununua simu, mwezi wa tisa simu zenu zitaanza kufanya kazi.

Lakini sasa tunaona haya hata kwenda kwa wale wananchi tena kusimama kwa sababu hizo simu bado nafasi za kuweka mitambo yao tunasema kuwa zipo ni nafasi kubwa tu, lakini sasa mnatupa nafasi ngumu sisi ya kusema uwongo kule, bora msiwe mnatuambia lakini tumeitisha mkutano mimi na Mheshimiwa Mbunge kwa kifua mbele kujidai msiwe na wasiwasi, lakini simu zenyewe ziko wapi.

Kwa hiyo, tunaomba jamani ule utekelezaji ambao mnatupa ahadi, basi muweze kukamilisha au kusema kweli kama inakuwa ni mwezi wa tisa haiwezekani mnatupa hata

moyo wakusema mwezi wa kumi kwa hiyo naomba liweze kushughulikiwa kabla ya uchaguzi kule Sikonge angalau mawasiliano yaweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la MKUKUTA na wakimbizi, mimi napata shida sana kusikia MKUKUTA maeneo ambayo wanaishi wakimbizi, maeneo wanayoishi wakimbizi ni maeneo ambayo yanaleta shida sana, hata suala la silaha majambazi ni maeneo ambayo wao wanaotusababishia nchi yetu hii kuweza kupata matatizo ya uharifu zaidi. Kwa sababu maeneo haya hata tukisema ni suala la MKUKUTA, suala la MKUKUTA mfano Tabora, Rukwa, Kigoma na Kagera, ni watu ambao wamejichimbia sana wamezagaa katika maeneo yetu hata wale wananchi wetu tunaposema kutaka kuwaondolea umaskini, hawa wameingia katika maeneo hayo na kuweza kuleta uharibifu mkubwa wa mazingira katika maeneo yetu. Mfano naweza kusemea maeneo ya Rukwa wameingia kule wakimbizi na wanajichukulia majukumu wenyewe ya kufyeka ile miti kwa kiwango kikubwa sana au kufyeka misitu yetu kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Sasa hapa wao itakapofikia muda wa kusema, sisi tunaweza kuwasaidia wananchi wetu, je, tunawasaidia hawa wakipinzi tunawaweka wapi na wanakero zaidi kwa sababu hata kuna vikao vikubwa ambazo vinawashirikisha wakipinzi nchi za Tanzania na nchi nyingine ambazo zinazoleta wakimbizi wao. Viongozi wetu wa mikoa hawashiriki kwenye hivyo vikao sasa hayo matatizo ambayo wale wananchi wanaoishi pale na viongozi wetu wa mikoa wanaoishi pale watapata wapi matatizo au majukumu ya kuweza kuamua kufafanua kuwa katika mkoa wetu kuna tatizo la wakimbizi linatusumbua kwa namna fulani.

Kwa hiyo, mimi ningekuwa naomba wanapokaa vikao vyao vya kuweza kuwa na maamuzi ya masuala ya wakimbizi viongozi wetu wa mikoa lazima washirikishwe. Kwa sababu ni wengi sana ambao wanaotusumbua katika maeneo haya na hata huu MKUKUTA wetu, utakuwa hauna maana katika maeneo wanaishi hawa wakimbizi kwa sababu sisi wenyewe tunaoishi maeneo hayo wanatukwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna suala lingine, suala la ajira kwa vijana, hii ni mara ya pili au ya tatu nazungumzia katika Bunge hili kuhusu suala la ajira la vijana ingawa Mheshimiwa amezungumza kuwa atashughulikia masuala ya ajira.

Lakini ajira hizi vijana wengi wanapata shida, vijana wengi wanapata shida kwa sababu mimi ningetoa ombi moja la kusema kipengele cha kusema uzoefu wa miaka mitano, kumi, kumi na tano, hicho kipengele kwa kweli kifanyiwe kazi zaidi ili kiweze kuondolewa. Unaenda kwenye udereva anakwambaia umeshaendesha gari uzoefu wa miaka kumi na tano? sasa mimi mwenyewe nina miaka thelathini ukiniambia kumi na tano, inamaana mimi nimeaza kuzoea kuendesha gari kwa miaka mingapi? Kwa hiyo hiki kipengele kwanza kinawakwaza sana vijana wengi kuweza kupata kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine, suala la Mkataba, katika Bunge letu tumepitisha kuwa kustaafu ni mwisho miaka sitini, na kama kustaafu ni miaka sitini kuna wale ambao tunawapitishia mikataba anaomba mkataba na kuweza kuendelea. Anaomba

mkataba wa miaka mitano, atakuwa na miaka sitini na tano, miaka mitano tena atakuwa na miaka sabini kijana huyu ambaye anayemaliza shule ataingia kwenye nafasi ile kwa miaka mingapi? Kama yule babu yake anaendelea kuwa na miaka sitini yeye mwenyewe ametoka shule mpaka ule mkataba ukaendelea miaka kumi.

Kwa hiyo, nafasi hizi za mikataba ni kweli ni nzuri ambako kuna wengine tunaowahitaji waweze kutusaidia, lakini zingefutwa au zingetungiwa utaratibu wa kuangalia, kuna wale wengine wanafaa kuendelea ili kuweza kusaidia nchi yetu kwa maamuzi yao yaliyomazuri. Lakini kuna wengine kwa kweli muweze kuliangalia kwa sababu vijana wetu watazidi kuzagaa na kukosa kazi baadaye mtasema vijana wanaleta matatizo wanatusumbua, lakini kusumbua kunatokana na ninyi wenyewe kuandaa utaratibu ambao unaowakwaza vijana kuweza kukosa nafasi ya kuweza kuwa uwakilishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ni suala la UKIMWI ambalo linanikwaza. Suala la UKIMWI tunalizungumzia kwa upana na urefu na kwa semina kuweza kuwapatia madawa walioathirika. Lakini tunajisahau kuwa wale waathirika wanakuwa na watoto wao. Je, wale watoto katika vituo vile tunawaangaliaje, kwa sababu mtoto mdogo akiwa na miaka mitano au kumi akiwa ameshaachwa na virusi vya ukimwi basi yule mtoto anaumia zaidi.

Sasa kuna utaratibu gani kuweza kuwasaidia watoto ambao wameachwa na wazazi wao wakiwa ni waathirika. Tunapoangalia upande mmoja tu wa mzazi lakini mtoto tukamwacha, hiyo inakuwa haitokuwa imewatendea haki wale watoto, na bado wale watoto wanakuwa ni waathirika zaidi. Kwa sababu hata wale wanaowalea watoto yatima wao pia wanapata shida zaidi, kwa sababu yule mtoto ni yatima anamlea lakini anamlea katika mazingira magumu zaidi kwa sababu hana dawa wala hana msaada wa aina yeyote. Kwa hiyo, tuliangalie suala hili kuweza kuwasaidia watoto yatima ambao wanaachwa na wazazi wao.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kinipa nafasi na kuweza kukushukuru wewe kwa muda wote wa miaka mitano ambayo tumeishi na wewe hapa Bungeni kwa kuongoza vizuri na hasa ikiwa kipindi cha asubhi ukikaa hapo bila kuinuka mpaka saa saba nakushukuru sana..

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii adimu ili nami niweze kuzungumza. Sintakuwa na mengi sana ya kuzungumza kwa sababu mimi nastaafu lakini nitakuwa naomba kupitia kwako niwaage Wabunge wenzangu, nikuage wewe Mheshimiwa Spika na Mawaziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijafanya hayo niliomba kutoa rambi rambi kwa kifo cha Mbunge mwenzetu, wananchi wa Kilombero wapate moyo mzito kwa machungu yaliyowapata amina.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningeliomba niompongeze Rais mteule wetu Jakaya Kikwete, kwa kuteuliwa kwake kushika Bendera ya CCM ili awe mshindani

mzuri. Naamini na nina hakika atapita na atakuwa Rais wa nchi hii, lakini nitakuwa nimepungukiwa kidogo kama sintawapongeza vilevile wale wanachama wenzetu kumi wa CCM, ambao hawakupata bahati ya uteuzi kule Chimwaga.

Hawa wametoa mafunzo makubwa mawili. Funzo la kwanza wametoa kwa watu na kwa dunia kwamba CCM imeandaa makada wazuri wengi. Kwa sababu hakuna aliyeachwa kule Chimwaga ambaye ni legelege, yoyote tulipata tabu sana ya kuchagua kwa sababu wote walikuwa ni fedha tupu, almasi. Sasa kwa hilo nawapa pole sana na pongezi na kwa kuionyesha dunia kwamba tunao makada wengi.

Lakini vilevile niwapongeze hawa hawa kwamba wameonyesha nchi kwamba Tanzania kuna demokrasi, wenzetu vyama vya upinzani walikaa wakitegemea mmoja kutoka kundi hili atachepuka akajiunge nao ili nao wapate mgombea madhubuti. Lakini hakuna aliyefanya hivyo wana CCM wenzetu hao wamejipanga upya na tunaendelea. Kwa hiyo pole sana kwa vyama vya upinzani.

Vilevile napenda sasa niwaage rasmi kupitia kwako Mheshimiwa Spika, wana Bukene ambao wamenichagua kwa vipindi vitatu nikiwa hapa Bungeni, watu hawa kwanza nawashukuru sana kwa kuniamini kuwawakilisha katika chombo hiki kwa miaka kumi na tano.

Pili, ninawaomba radhi kwa sababu walihitaji mambo mengi lakini nina moja kubwa ambalo walilitaka na ambalo hawakulipata nalo ni umeme. Miaka yote tangu 1985 nilipokuwa hapa Bungeni nimelilia umeme mpaka leo natoka umeme bado. Wananchi wa Jimbo la Bukene ninawaomba radhi sana sikuwa mzembe lakini Wizara hii ilishindwa kushirikiana na mimi.

Mheshimiwa Spika, siku moja tulipokuwa tumekaa kwenye Kamati ya Siasa ya Wilaya, Mjumbe mmoja alisema nyie Wabunge wa Nzega labda mngeomba msaada kwa Wabunge wenzenu. Mimi liliniuma sana, kuomba msaada, nikaanza kuwaza kwamba kwani mimi hawa Mawaziri wananibagua, kwa nini iko hivi? Nikasema mbona Naibu Waziri wa Nishati na Madini ananikaribisha mpaka kwake, sasa vipi leo niseme ananibagua? Nikashindwa, lakini likabaki linaniuma kwa nini huyu amewaza kwamba tuombe msaada?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu shida zote na maelekezo yote wanayoyatoa watu wa Wizara ya Nishati wanasema watapeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya Mkoa, watapeleka umeme kwenye viwanda vinavyosindika mazao. Hiyo ndiyo sera, tunakubali na wanasema wakati wanapeleka umeme kwenye viwanda au Makao Makuu ya Wilaya au Mkoa wao watateremsha umeme kwenye vijiji vya njiani.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa hapa Bungeni nikiuliza hivi, hivi vijiji vya njiani ni kilometa ngapi kutoka *line?* Jibu silipati, lakini ninayoyaona nafikiria ile sera haifuatwi kwa sababu Wilaya ya Nzega ndio Wilaya ya zamani na imezaa Igunga. Lakini ukiona Igunga vijiji vingi vina umeme, Nzega tangu nilipokuwa Mbunge mwaka 1985

nilitoa malalamiko kwa kijiji kimoja cha Nata ambao umeme ulikuwa unapita juu, wanapitwa tu umeme unatoka Shinyanga unakimbia kwenda Nzega.

Mheshimiwa Soika, nikalalamika kwenye Bunge na watu wa Nzega wakanisaidia kwa sababu watu waliokuwa wanajenga nguzo za umeme wa gridi kutoka Shinyanga kuupeleka Tabora, wananchi wakawa wanafungua zile *bolt* na *nut* wanatumia kutengenezea mikokoteni. Nikamkuta *OCD* kakamata mikokoteni yao mingi ameirundika pale, nikamwambia huna haki hawa wamechukua hizo *nuts* wakazitumie, kwa sababu hizi nguzo zinajengwa hazitawafaa, basi waachie.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati wakawaachia na wakateremsha umeme, lakini bado kitu cha kusikitisha sisi tunaonekana Wabunge wa Nzega hatufanyi kazi. Umeme waliu-*step down* katika kijiji cha Nzega Ndogo ili waupeleke Chomachankola kwenye kiwanda, kwenye *ginnery* na kutoka kule uende Igunga. Pale walipouteremsha hawakuuweka umeme kwenye kijiji kile na pale pana Kituo cha Afya, kuna shule, kuna mgodi mdogo wa Isungangwanda. Lakini waliteremsha wakauchukua kupeleka Chomachankola, nimelalamika nashukuru Mheshimiwa Omar Kwaang', alikuja kutembea kuona miradi ya umwagiliaji, nikampeleka kwenye kijiji hicho. Tukaja tukalalamika hapa na Mheshimiwa Omar Kwaang', akatoa ushuhuda kwamba ni kweli na ameona naye kwa macho watu hawa wakaona haya wakateremsha pale. *(Makofi)*

Sasa Nzega pamoja na kuachwa na wakoloni kama Wilaya ina vijiji viwili tu vyenye umeme na Nzega yenyewe. Sasa unabaki unajiuliza hivi vijiji vya kando ya njia ya umeme ni kilometa ngapi? Maana tunashangaa wameutoa Chomachankola wamepeleka kijiji kimoja kule Igunga cha Ziba. Wakatoka Ziba wakapeleka Nkinga kama maili nane, tukajiuliza swali sisi pale Nkinga ni hospitali kubwa tunakwenda hata sisi, lakini wameutoa pale wanapeleka Simbo kilometa 42.

Sasa na sisi tunajiuliza kutoka Nzega kwenda Bukeni ni kilometa 42, kutoka Ziba kwenda Simbo ni kilometa 42. Hivi kilometa 42 zinazoonekana ziko kando ya njia ya umeme ni zipi? Sisi tuna kilometa za majini hawa wana kilometa za nchi kavu, unabaki unashangaa. Basi ndio maana mimi nasema wameshindwa kushirikiana nasi, nawaomba basi sina kinyongo nao, nawaomba Mbunge atakayekuja kushika Jimbo la Bukene wamsaidie, washirikiane naye. Kama walishindwa kushirikiana na mimi labda kwa sababu ni mzee huyo atakuja kijana, washirikiane naye. Pamoja na hayo nawaomba sana watu wa Jimbo la Bukene wanisamehe kwamba hilo sikuweza.

Mheshimiwa Spika, nilijaribu kubadili mbinu nikasema labda niombe Bukene iwe Wilaya kusudi niweze kuuwa ndege wawili kwa jiwe moja, na yenyewe hakuna. Nikiuliza maswali naambiwa sifa zote za Bukene kuwa Wilaya zipo, lakini kuwa Wilaya fedha hazipo sasa hizi fedha huwa zinakosa kwetu tu kwingine mnapeleka.

Mheshimiwa Spika, kitu cha muhimu ambacho nataka kusema hapa cha mwisho kabisa sitaki kukupotezea muda, ni kwamba mimi nimekwishaonja yote. Nimekwishaonja kuanguka Ubunge nikakaa mstari wa nyuma huko na nimekwishaonja kuushinda Ubunge. Mimi kitu ambacho kilikuwa kinanikera ambacho nasema na

ninawaomba na wenzengu ambao tunastaafu nao tusikifanye kwani kinaleta kero sana kwa viongozi wa zamani kuwa walalamishi kulaumu viongozi wapya kama mimi nikakae pale kijijini kwangu Mbunge atakayekuja niwe nam-*criticize,* nalaumu laumu tu, si afadhali kumsaidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba sisi turudi mstari wa nyuma lakini tuwasaidie Wabunge watakaokuja, nimeyapata haya ya kulaumiwa kila wakati, wanaokulaumu wanajiita waasisi, sisi waasisi sasa kama muasisi kama wewe uliweza yote mbona tumekuta hayapo haya?

Mimi nisiweze kujivuna kwamba mimi ndio Mbunge wa kwanza wa Bukene, huyu anazitizama, maana yake nini? Ni lazima tushirikiane na uongozi unaoendesha madaraka sasa hivi. Ukiondoka, ukitaka kupata taabu, na imetuletea taabu, mimi nilipoanguka uchaguzi nilikwenda kwenye mikutano miwili, mmoja ulikuwa wa Diwani wa Kata yangu nikahudhuria maana na mimi ni raia, nikahudhuria kwenye kikao hicho.

Mheshimiwa Spika, Diwani alikuwa na mawazo ya kujenga Sekondari, akasema vizuri na mimi nikaomba nitoe ushauri nikasema Mheshimiwa Diwani tunashukuru sana kwa mawazo mazuri ya kujenga Sekondari, lakini mbona tuna Sekondari nyingine hapa hapa haijai wanafunzi? Tulikuwa na Sekondari waliiomba wazazi wakapewa wazazi ilikuwa *Middle School* wakaigeuza kuwa Sekindari, Sekondari ya ajabu. Mwalimu wa Sekondari mmoja tu na wengine wa *Primary* waliofukuzwa kule wamekusanywa wakawekwa pale. Sasa kwa nini tusiimarishe hii halafu tuwaze kujenga nyingine? Hisia zilizotokea pale zikawa za aina mbalimbali. Akinamama wakapiga vigelegele, lakini hawakupiga vigelegele kwamba nimetoa mawazo mazuri, walipiga vigelegele kwa sababu wanasema huyu anatuokoa tusichangishwe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Diwani wangu naye akatoka pale akasema Stephen Kahumbi sasa ameanza kulilia Udiwani, nikashangaa sana nikasema sasa mimi nisiwe naenda kwenye mikutano? Mkutano wa pili, alikuja Mheshimiwa Joseph Warioba wakati huo alikuwa Waziri Mkuu, alikuja kuweka jiwe la msingi kwenye Kituo cha Afya cha kijijini kwangu, amekuja Mkuu wa Mkoa Gama ndiyo alikuwa Mkuu wa Mkoa, kaja pale sasa mimi nikashiriki na Serikali ya kijiji kwamba huwa tunaweka jukwaa hapa. Mwisho akakumbuka akanitazama, mbona wewe umekwenda vyama vingi? Nimekwenda vyama vingi kuanguka ndio kwenda vyama vingi? Mimi nilimuuliza tu Gama.

Mheshimiwa Spika, hivi huu umri wangu leo niende *NCCR - Mageuzi* mpaka nitakapopata Uenyekiti wa tawi mwaka gani? Nina miaka 74 niende sasa kuanza upya darasa la kwanza *UDP* nitapata cheo gani, nimefika umri gani? *(Kicheko/Makofi)*

Nilimwambia Gama bwana ushike adabu, mimi siwezi kufanya hivyo. Siku nyingine nilikwenda kwenye mkutano wa Waziri ametembelea Bukene na mimi nikaenda, Mungu alininusuri nilichelewa, kwa hiyo, nikafika nikakaa pembezoni kule nasikiliza kikao. Kilipomalizika kikao wakaulizwa wananchi, mmoja akasimama tena ndio wa kwanza, akasema Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana umekuja, lakini sisi

tuna bahati mbaya sana Mbunge hatumjui na Mbunge yupo, hatujamuona sisi huku hatuna Mbunge.

Sasa mimi nikaanza kufikiri nikilinganisha haya mawili, ya kwanza kwamba kama wangeniona wangeniita *high table* wasingeniacha. Kama ningekuwa *high table* swali hilo linatolewa kwa Mbunge aliyenitoa mimi si angepata mawazo kwamba mimi nimeanza kutumia watu kuuliza maswali dhidi yake? Lakini bahati hakuniona.

Mheshimiwa Spika, nashukuru mimi naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu, hoja zote zitakazokuja nitaziunga mkono. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze na mimi kuchangia hii hoja ya Waziri Mkuu. Awali ya yote ningependa nitoe pole na rambirambi zangu kwa wananchi wenzangu wa Jimbo la Kilombero kwa kufiwa na Mbunge wao mpenzi Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mungu ailaze mahali pema peponi roho yake. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kutoa pongezi nyingi na hongera kwa Chama cha Mapinduzi kwa kuweza kuteuwa wagombea wa nafasi za juu katika uongozi wa nchi hii. Ningependa nimpongeze aliyeteuliwa kwa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Ningependa pia kuchukua nafasi hii kumpongeza mgombea mwenza, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuteuliwa kugombea nafasi ya Makamu wa Rais na pia nimpongeze sana aliyeteuliwa kugombea nafasi ya Urais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume. Namwomba Mwenyezi Mungu aweze kutujalia Chama cha Mapinduzi kiweze kupata ushindi wa kishindo katika uchaguzi unaokuja mwezi Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa nimpongeze Waziri Mkuu. Waziri Mkuu amekuwa ni kiongozi bora kwa sababu ameteuliwa mara mbili kuchukua nafasi ya Uwaziri Mkuu kwa awamu mbili. Maana yake ni kwamba amekuwa msaidizi mzuri kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri Mkuu imeonyesha jinsi ambavyo anaweza akaweka kumbukumbu za kazi ya maendeleo ya Serikali ya Awamu ya Tatu na ameweza kufanya kazi nzuri na kutoa hotuba nzuri kwa sababu kasaidiwa na wasaidizi wake wakiwa ni Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, bila kumsahau Katibu Mkuu, Bibi Rose Lugembe, mimi ninaamini kwamba penye mama ambaye anafanya kazi kwa bidii mambo yanakwenda vizuri, ninampongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi hizi bila kuwasahau wataalam wote katika Ofisi ya Waziri Mkuu ambao wamechangia kwa njia moja au nyingine kumsaidia na kumpa ushauri mzuri ndio sababu kazi nzuri imeonekana na hii hotuba imeonekana ni nzuri ambayo ni *very comprehensive.*

Mheshimiwa Spika, tumesema kwamba hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imezungumzia mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu. Hii Serikali ya Awamu ya Tatu imekuwa chini ya uongozi wa Rais Benjamin William Mkapa. Amekuwa ni dereva wa gari ambalo limekweda vizuri, gari ambalo halijawahi kupata ajali ndio sababu tumepata mafanikio mazuri kwa namna hii. Naomba nimpongeze sana na ningependa kusema kwamba uongozi wake umebadilisha sura ya nchi tukawa na utawala bora, tukapata mafanikio ya maendeleo ya kiuchumi na ndio sababu hata Jumuiya ya Kimataifa imemtambua kwamba ni kiongozi mwenye busara, mwenye hekima na ambaye ana uwezo mkubwa hivyo akaweza kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti Mwenza katika Tume ya Utandawazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia akateuliwa na Waziri Mkuu wa Uingereza kuwa mshauri katika ile Tume ya Maendeleo ya Afrika na matunda ya kazi yake tumeona juzi tarehe 9 Juni, 2005 walipokuja kuzindua ile *report* hapa. Kwa kweli imekuwa ni heshima kubwa sana kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mimi nina amini pamoja na kwamba anastaafu, mimi nasema kwamba Tanzania bado tunahitaji busara zake na hekima zake, na tunasema kwamba yeye ni hazina ya kuweza kuendelea kutoa ushauri wa kuisaidia Serikali inayofuata, pamoja na mwananchi mmoja, mmoja au mwingine ambaye atahitaji ushauri wake kwa nia njema tu katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunasema kwamba penye ngoma nzuri basi kuna wachezaji wengi na walioandaa na wachezaji wengi walioandaa ngoma yetu ni Mawaziri wake ambao alipowateua mara ya kwanza aliwapa jina zuri sana akawaita askari wa miamvuli. Kweli hawa maaskari wamekuwa ni *sharp,* hakuna aliyedondoka akaachia mwamvuli wake hewani. Wamefanya kazi nzuri na ndiyo sababu kila mmoja ametembea na mwamvuli wake mpaka tukafikia kwenye awamu hii ya mwisho. Ningependa kuwapongeza sana na nina amini kwamba wataendelea kuwepo katika kushauri katika suala lote la mchakato wa maendeleo wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kukuambia kwamba wewe umekuwa ni hazina nzuri sana katika kuliongoza Bunge hili kwa busara na hekima. Bunge letu linatambulika ulimwenguni kama Bunge la kistaarabu. Mimi nasema kwa muda wa miaka mitano niliyokuja hapa sijawahi kumwona Mbunge anamnyooshea Mbunge mwenzake kidole huku ndani, sijawahi kumwona Mbunge anayemtukana mwingine wala mtafaruku wa aina nyingine yoyote kama inavyotokea kwenye Mabunge mengine tunayaona kwenye *television* na kwenye magazeti.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu umekuwa unatuongoza hapa Bungeni kwa busara na hekima pamoja na kuzingatia misingi ya demokrasia. Mimi nina amini kwamba Mwenyezi Mungu ataendelea kukupa hekima, ataendelea kukupa afya njema uweze kuwa hazina ya busara na hekima katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo ningependa sasa nirudi kwenye hotuba ambayo iko mbele yetu. Hotuba ambayo iko mbele ni ya Waziri Mkuu, imetoa

muhtasari wa maendeleo ya nchi hii kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita na ametoa kwa njia ambayo ni ya ufasaha na umahiri mkubwa ambao umeonyesha wazi wazi kabisa kwamba maendeleo ya nchi ni pale ambapo unaona kwamba Serikali imeweza kuweka mazingira ya kumletea mwananchi maendeleo na Serikali yetu ya awamu ya tatu imeweka mazingira ya miundombinu na miundombinu hiyo tunaiona barabara zipo.

Nakumbuka nilikwenda Arusha siku moja nikawasikiliza wananchi wakizungumza wanasema bwana siku hizi mtu anakuwa hapa Arusha asubuhi, unaweza ukaenda Dar es Salaam ukaenda kula chakula cha mchana, jambo ambalo lilikuwa halipo. Wananchi wengi wanazungumza wanasema kwamba siku hizi tunaweza tukapata mazao mengine katika masoko yetu siyo kwa sababu wananchi wa Tanzania walikuwa wavivu zile nyakati nyingine, ni kwa sababu sasa hivi uwezekano wa kukusanya yale mazao kutoka kule vijijini kwenda mijini upo kwa sababu kuna barabara.

Mheshimiwa Spika, ningependa nizungumzie pia kwamba Serikali yetu imeboresha sana huduma za jamii. Huduma za Jamii ambazo kweli tunajivunia nchi hii na kila mtu anazungumza hata majirani zetu ni elimu.

Mheshimiwa Spika, kuweza kutoa elimu kwa watoto na kuongeza idadi ya watoto wanaoandikishwa katika elimu ya msingi, maana yake ni kwamba tumeweza kumpiga adui mmoja mkubwa nyundo kubwa ambaye ni ujinga. Ujinga umekuwa ni baba wa umaskini, ujinga umekuwa ni baba wa vurugu na matatizo mengine mengi ya kijamii.

Kwa hiyo, nina amini kwamba kwa sababu sasa tumeshaweka miundombinu ya elimu, watoto wetu watasoma hata pale ambapo tutazungumzia mchakato mzima wa maendeleo tutakuwa na wananchi wenye uelewa, kwa hiyo, wataweza wakayatekeleza na kila mmoja akaelewa kwa nini ajiondolee umaskini peke yake kwa sababu ana uelewa mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa niseme basi kwamba pamoja na kwamba Serikali yetu imesema kwamba tunatoa elimu kwa watoto wenye umri wa kuandikishwa shule bure. Ningependa nitoe rai yangu kwamba kuna watoto wengi ambao kwa bahati mbaya bado umri wao unakuwa ni mkubwa kuliko umri wa kwenda shuleni. Serikali yetu ilizungumzia kuwepo na programu moja mpango wa MEMKWA.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi huu mpango wa MEMKWA bado naona kwamba unasua sua na unalega lega. MEMKWA pia itakuwa ndio jibu ambalo litasaidia kuwaondoa watoto ambao wako mitaani ambao hawasomi shule, kuwaondoa watoto ambao wako vijijini wanamangamanga, hawasomi shule ili na wao wawe darasani waweze kupata mwanga wa elimu.

Mheshimiwa Spika, hivyo pamoja na kazi nzuri ambayo imefanyika katika mpango wa Elimu ya Msingi, basi Elimu ya Msingi pia iangalie namna ambavyo wanaweza wakaboresha kwamba kila penye Elimu ya Msingi basi kuwepo na darasa la MEMKWA. Kwa sababu tunaamini kwamba kila Mtanzania ana haki ya kuweza kupata elimu, itatusaidia itaongeza uelewa na itapunguza ule tunasema mlundikano wa vijana ambao hawana uelewa kwamba dunia inakwendaje.

Mheshimiwa Spika, tunakuja kwenye Elimu ya Sekondari, nashukuru kwamba tumekuwa na mpango wa MMES, mpango wa MMES utasaidia. Lakini tutafika mahali kwa sababu mfumo wetu wa kuwa na elimu ya juu bado haujaboreka tutashindwa kuwapeleka wananchi wetu pale ambako tumekusudia. Sasa kwa sababu pia tunazungumzia kwamba kuna tatizo la kukosekana kwa ajira, ningependa basi Tanzania tuwe na mpango badala ya kuzungumzia *VETA* tu, basi tuseme kwamba tuwe na mpango wa elimu ya ufundi. Maana yake ni kwamba kila ambapo panajengwa Shule ya Sekondari kule kijijini basi kuwepo pia na madarasa ambayo yatakuwa na mpango wa kutoa elimu ya ufundi kusudi watoto wetu wanaomaliza darasa la saba na wale ambao wanamaliza form four hawawezi kuendelea zaidi na elimu, waweze kupata elimu ya ufundi ili waweze kujenga mazingira ya kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi naomba nizungumzie sasa kero yetu wananchi wa Morogoro. Wananchi wa Morogoro tunashukuru kwamba tuna barabara, lakini katika Mto Kilombero kumeshatokea ajali na baada ya ile ajali ya Kivuko kukatokea tena mtikisiko mwingine ambao ulikuwa karibu ungekuwa ni ajali na kwa bahati mbaya mle ndani kulikuwa pia na wageni waliotoka kwenye Ubalozi wa Uswiss.

Naomba kwamba ili tuweze tukafungua na kuchochea maendeleo katika Wilaya ya Ulanga, Serikali yetu iangalie uwezekano wa kutujengea daraja katika Mto Kilombero. Naomba hilo ni ombi la wanawake kwa sababu akinamama wanasema tunalima, lakini hatuwezi kuvusha naomba Serikali iangalie, wale ni wapiga kura na wale wanachangia sana katika pato la maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Malinyi ni kubwa sana kama Wilaya, lakini haiko mbali na Kihansi. Umeme unaanzia Kihansi unatoka katika Mkoa wa Morogoro lakini wale wananchi wanapenda maendeleo wamejenga nyumba nzuri, shule zinajengwa hakuna umeme. Kwa hiyo, tunaomba kwamba ule umeme usitupite pale, basi katika mpango wa miaka mitano unaokuja waangalie uwezekano wa kutueletea umeme katika eneo la Malinyi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uboreshaji mzuri wa huduma za afya, wanawake wa Tarafa ya Matombo, Tarafa ya Kisaki na Mngazi bado wanakufa kwa sababu yakutokuweza kufika hospitalini mapema kwa sababu ya umbali wa kwenda hospitali na kukosa usafiri. Naomba Serikali yetu isisubiri tu kwamba Serikali za Mitaa ndizo zenye jukumu za kujenga hospitali. Lakini pale ambapo tatizo ni kubwa hawa ni wananchi wanalia matatizo ni mengi vijijini, lakini naomba kwamba hilo tatizo la kujenga hospitali ambayo inaweza ikafanya angalau *ceasaream section* kwa akinamama ambao wamepata *obstructed labour* basi uangaliwe ili tuweze kujengewa hospitali katika Tarafa ya Mngazi.

Mheshimiwa Spika, ningependa nizungumzie dawa ya kulevya, nashukuru Serikali yetu imeona kwamba ni kero na imeona kwamba ichukue hatua kuwa na kitengo. Lakini kuwa na kitengo bila kuwa na sehemu za kutolea ushauri nasaha kwa sababu hawa watoto ni wetu wemeshaharibika hata ukimkamata ukampeleka Isanga, Isanga itafurika,

Magereza yatafurika na mtu anayetumia dawa za kulevya siyo kwamba yeye amekuwa ni hatari kwa mtu mwingine, ila ni hatari kwake mwenyewe. Lakini tunahitaji kumkarabati kitabia, naomba Serikali yetu iangalie namna ya kuweza kufungua vituo katika kila Mkoa kwa sababu hawa watoto wapo na wanaendelea kuongezeka, wanatumia dawa za kulevya, wavuta bangi, wanaongeza kuwa *congestion* kubwa sana katika hospitali zetu za wagonjwa wa akili.

Mheshimiwa Spika, wengine siyo wagonjwa wa akili, sasa unapokwenda kumweka na mgonjwa wa akili na yeye anaanza kuwa na tabia kama ya mgonjwa wa akili. Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuweza kujenga vituo vya kukarabati kitabia watu ambao wanatumia dawa za kulevya, pamoja na sehemu za kukarabati pia au kuwawezesha na kutoa ushauri nasaha kwa watu ambao wamekuwa na ulevi wa kupindukia, wanataka kubadili tabia lakini hawajui wamwendee nani. Mimi naona hilo tatizo lipo na tumekuwa kama tumelifumbia macho. Naomba hilo liangaliwe kwa undani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa mimi ningependa kusema kwamba ni mara nyingi sisi wanawake tunatambulika kwamba tunachangia sana katika pato la nchi hii. Lakini hatutambuliwi, nimeangalia Bajeti ya Mheshimiwa Basil Mramba, nimeangalia hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, pamoja na kusema kwamba maendeleo yamekuwepo, lakini mimi najua kwamba wanaolima kilimo ambacho kinachangia asilimia 48 ni wanawake wengi kule kijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba tutambuliwe, tutambuliwe kwa njia moja. Nashukuru kwa kunipa nafasi na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika hotuba ya Waziri Mkuu. Kabla ya kuchangia niungane na Wabunge wenzangu waliotoa rambirambi kwa kifo cha marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kigoma Kusini tunaiombea roho ya marehemu Mungu aiweke mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu ningependa niwapongeze wana-CCM wenzetu ambao wamepitishwa na Chama cha Mapinduzi kubeba bendera ya Chama chetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, mgombea mwenza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kugombea nafasi ya Uraia wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliisoma hotuba ya Waziri Mkuu baada ya kusikiliza kwa makini na baada ya kuisoma nikaielewa vizuri. Naipongeza hotuba hiyo na nampongeza yeye Waziri Mkuu, Mawaziri wawili katika Ofisi yake Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib. Nampongeza pia Katibu Mkuu na timu ya Maafisa katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuandaa Bajeti nzuri, lakini pia maelezo ya kina ambayo yamejumuisha utekelezaji wa Serikali katika kipindi cha miaka 10. Napongeza kazi iliyofanyika ni nzuri kama ilivyoainishwa katika hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna jambo moja ambalo liko bayana katika hotuba hiyo nalo ni ushirikiano kati ya mihimili mikubwa mitatu ya uongozi wa Taifa letu. Katika hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 97 hadi 102, zimeonyeshwa sheria ama zilizofanyiwa marekebisho au zilizotungwa zipatazo 209. Hizi ni sheria ambazo zilipitishwa katika kipindi hicho cha miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu uongozi na utawala bora, msingi wake mkubwa ni utawala wa sheria. Kwa hiyo, mihimili hii mitatu yaani Serikali kuweza kuleta sheria hizo, Bunge ikazipitisha na Mahakama ikazitumia, ndio siri ya mafanikio ya mabadiliko tunayoyaona katika maendeleo ya uchumi wetu. Naipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu na nguzo hizi tatu ambazo zimeshirikiana kufanikisha hayo, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuthibitisha ukweli huo, ipo pia hali ambayo viongozi wa Kitaifa wamekuwa karibu sana na wananchi, mfano ni katika Mkoa wetu wa Kigoma na hasa katika Jimbo langu la Kigoma Kusini. Katika kipindi kisichozidi miezi 24 tangu nimeingia Bungeni, Rais, Makamu wake, Waziri Mkuu, Mawaziri 14 na Manaibu Waziri watano wametembelea Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kufanya hivyo, wametoa hamasa kubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma na kuhimiza utekelezaji wa miradi. Kila aliyekuja, upo mradi mkubwa ambao ameupa hamasa na wananchi wamehamasika sana. Mfano ni alipokuja Mheshimiwa Rais kuzindua kivuko kwenye Mto Malagarasi na baadaye kuhamasisha ujenzi wa barabara mwambao wa Ziwa Tanganyika jambo ambalo limetia hamasa kubwa. Barabara hii itakapojengwa itafungua Ukanda wa Ziwa ambao una fursa kubwa za kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, alipokuja Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, alihamasisha sana kilimo na sasa hivi kuna miradi ya umwagiliaji katika kijiji cha Nkokwa na Mgambazi ambapo miundombinu inaandaliwa kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, alipokuja Mheshimiwa Waziri wa Elimu, naye alihamasisha ujenzi wa sekondari. Kwa mfano, katika Jimbo langu nilipoanza tulikuwa na shule moja ya sekondari, sasa hivi zipo shule za sekondari sita katika kipindi kisichozidi miezi 24. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Ulinzi, Waziri wa Maliasili na Utalii, Waziri wa Ujenzi, wote walihamasisha maendeleo katika sekta zao. Kwa hiyo, naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kueleza kinaganaga mafanikio ambayo yamefanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa wale Watanzania, awe ni Mtanzania wa kawaida au kiongozi anayebeza mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu, tatizo lake ni kwamba hana uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo napenda nilizungumzie, ni eneo linahusiana na uwezeshaji wananchi kiuchumi kama ilivyo katika ukurasa wa 58 chini ya mfumo huu wa Mfuko wa Umoja.

Mheshimiwa Spika, hapa kuna maelezo kidogo ambayo nadhani ni vema nikayachangia kwa jinsi ninavyoliona. Shabaha ya Mfuko huu wa Umoja ambao unatokana na ubinafsishaji wa mashirika na Serikali kwa kutaka wananchi wawe na uwezo wa kimaendeleo, imeanzisha mfuko huu kwa kutenga asilimia ya hisa zake katika makampuni yaliyobinafsishwa, Kampuni ya Sigara na Kampuni ya Bia kiasi cha shilingi bilioni 10.9 zimeonyeshwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika hili, ningependa nishauri kwamba ingekuwa vyema thamani ya hisa ikatamkwa katika dola za Kimarekani kwa sababu inabadilika badilika kama ikitajwa katika shilingi. Katika kijitabu hiki ambacho ni taarifa kwa umma *(Public Information),* tarehe 8/3/2005, thamani ya hisa hizo ilionyeshwa kwamba ni shilingi 11,571,609,600. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu ya kuitamka kwa shilingi thamani ya hisa hizo inaonekana ni shilingi 10.9bil hapa kuna tofauti ya shilingi milioni 600. Hiki ni kiasi kikubwa sana na naamini wawekezaji katika makampuni hayo wanatambua thamani ya hisa zao katika dola za Kimarekani. Sasa ili mfuko huu tuweze kujua thamani yake isiyo na mabadiliko ingekuwa vema kuitambua thamani hiyo katika pesa ambazo hazipungui badala zake zinaongezeka na hivyo tutaweza kuwawezesha wananchi kwa uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lipo tatizo moja zaidi katika hilo ambalo ningependa Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie, nalo ni kuhusu vipande hivi wanavyouziwa wananchi. Kwanza muda uliotolewa ni mfupi sana mwezi wa tano hadi wa saba. Kwa kuwa ni mpango ambao unapaswa uende kwa watu ambao hawana uzoefu wa kuwekeza. Makampuni yaliyotajwa ambayo watu wananunua hisa hizo ni *NMB,* Benki ya Posta, Shirika la Posta, *Biashara Commercial Bank* na mawakala wa soko la hisa. Kwa kuwa katika Halmashauri ya Kigoma hakuna chombo chochote cha namna hiyo, sasa wananchi watawezaje kununua hisa hizo?

Mheshimiwa Spika, mimi ningetarajia kwanza muda uwe mrefu kwa sababu hapa tunataka kujenga utamaduni wa kuwekeza na haiwezekani jambo hilo lifanywe kwa muda mfupi hasa kwa watu wa vijijini ambapo taasisi hizi ambazo tumezitaja hazipo.

Mimi ningetarajia kwamba kwa sababu ni mpango wa muda mrefu wa kuwewezesha, ungechukua hata mwaka mzima kwa sababu kama Serikali katika kutumia mashirika haya yaliyobinafsishwa imechukua muda mrefu karibu miaka kumi na zaidi kwa nini fursa ya kuwawezesha wananchi kwa njia hii itolewe kwa muda mfupi? Nadhani suala hili linapaswa liangaliwe kwamba uwe muda wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, ningetarajia kwamba hizo shilingi 5,000 ambapo ndio kiwango cha chini ambacho mtu anaweza kununua basi zingeelekezwa katika mfumo wa kaya vijijini. Kwa sababu ukichukua kaya moja ikawekeza hicho kiwango cha chini cha

shilingi 5,000 ambapo itapata ruzuku ya Serikali ya shilingi 1,500 yenyewe ikalipa 3,500 ingewezekana, huo ndio uwezo wa kaya zetu zinavyoweza kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa njia hiyo ukichukua vijiji vinavyokadiriwa kuwa 10,000 katika nchi yetu kiasi cha pesa ya mtaji iliyotolewa shilingi bilioni 10.9 zingeweza kutosheleza vijiji vyote hivi kwa sababu itakuwa ni shilingi 15,500,000,000 na wananchi katika vijiji vyote vipatavyo 10,000 wangekuwa wamechangia shilingi bilioni 35. Kwa hiyo, kwa mfuko huu katika kipindi chote ungeweza kuwa na hisa za wawekezaji vijiji vyote shilingi bilioni 50 ambapo ndio tungesema sasa tunawaweza wananchi katika Taifa lote kwa umoja wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani hilo ndio linapaswa lifanyike kwa sababu hapa tunaanzisha utamaduni ambao wananchi wetu hawajauzoea na hatuwezi kuleta mabadiliko katika muda mfupi kama vile tungekuwa tunazungumzia kuuza hisa za Kiwanda cha Bia, *TATEPA* katika masoko ya kawaida, huu nadhani ni mkakati ambao utawawezesha wananchi katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa rai hiyo, naomba niunge mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika mjadala huu wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kama wenzangu, naomba na mimi nianze kutoa shukrani, pongezi na rambirambi kwa haraka iwezekanavyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa kifupi, nikupe wewe pongezi kwa kuliongoza Bunge hili vizuri kwa kipindi chote. Niliwahi kuwa Mbunge hapa katika Bunge la kwanza. Wakati tunaanza mimi binafsi nakumbuka hali ya Wabunge humu maelewano hayakuwa mazuri lakini kutokana na busara za Mheshimiwa Spika pamoja na mafunzo nimerudi tena hapa hali ya uchangiaji ni nzuri na hali ya uelewano ni nzuri sana, mimi naamini ni kwa sababu yake, hongera sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe rambirambi kwa familia na ndugu wa Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, Mbunge wa Rahaleo, familia na ndugu wa mzee Paul Bomani, mzee wetu wa Kanda ya Ziwa, naomba niungane na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi zangu za dhati kwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero. Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi, *amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kwa haraka nitoe pongezi kwa vyama vyote ambavyo vimekwishapata viongozi wao wa kugombea Urais. Lakini kwa kuwa mimi niko Chama cha Mapinduzi, naomba nirudi hapo kwenye Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si nia yangu kuwakatisha tamaa ambao wanadhamiria kuingia katika kinyang’anyiro cha kugombea Urais, lakini ndugu zangu safari hii wa Chama cha Mapinduzi kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, sisi ndio tuna dume la

shupaza bwana. Nina hakika kabisa Mheshimiwa Jakaya Kikwete atawagaragaza kweli na wananchi wana imani na wanamsubiri. *(Makofi)*

Naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kuwa mgombea mwenza. Naomba pia nitoe pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kupewa nafasi hii tena na Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Amani Abeid Karume katika miaka hii mitano ameonyesha yeye ni mchapakazi kiasi gani, ameonyesha yeye anapenda Watanzania wenzake kiasi gani, ameonyesha anapenda Zanzibar ishirikiane na wananchi wote kwa pamoja pasipo ubaguzi na kwa amani. Katika hali hiyo kama anavyoitwa Amani wananchi wa Zanzibar kwa kuwa wanajua, mimi nina hakika safari hii watampitisha kwa kura nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo nimeomba nitoe pongezi kwa kifupi kwa sababu Wabunge wenzangu wote wameongea na wametoa sifa vizuri zaidi, nimeona nisipoteze muda hapo ila kuna moja ambalo nadhani wenzangu wamelisahau kidogo. Napenda sana kuwapongeza washiriki wote 11 ambao walichukua fomu ya kugombea nafasi ya kupata tiketi ya kugombea Urais kupitia Chama cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo zoezi lao walilichukua kwa ustaarabu wa hali ya juu sana. Shughuli yao wameshamaliza, wameshapongezana na wameshavunja kambi zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita wakati wa kipindi cha maswali na majibu, kuna Mbunge mwenzetu aliuliza swali kwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu mnyama mmoja anayeitwa Kakakuona na alikuwa anataka kufahamu uwezekano wa mnyama huyo kutoweka hapa Tanzania kutokana na umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, mimi nitatoa mfano kwa mnyama mwingine na siku nyingine nikipata nafasi nitamuuliza Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu uwezekano wa mnyama huyu kutoweka kwa sababu kuna mafunzo tunaweza kuyapata kutoka kwake.

Mheshimiwa Spika, kumradhi lakini mnyama ninayemzungumzia mimi, ni fisi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, fisi wanaishi katika ukoo, kuna fisi wa Serengeti, fisi wa Ngorongoro, fisi wa Dodoma na kuna maeneo mengine fisi hawaishi ukienda huko kama wewe ni fisi watu watakuuliza fisi hapa umefuata nini hapa sio kwako.

Mheshimiwa Spika, kama wewe ni fisi sifa yako kubwa kama fisi ni saa mfupa ukitokea wewe unatakiwa uugombanie mfupa, ukitokea mfupa huugombei fisi wenzako watakushangaa, huyu fisi katoka wapi? *(Kicheko)*

Kwa wenzetu fisi kwa hilo halina ubaguzi huhitaji hata kuchukua fomu kwamba hii fomu ya Urais *jackpot bingo* yake shilingi 1,000,000 ya Ubunge *jackpot bingo* yake shilingi 100,000 aah, hakuna wewe njoo tu hata kama mwili wako mdogo, afya yako sio nzuri, hata kama una afya kubwa, saa ya kugombea mfupa, msimu ukifika wewe si fisi eeh, karibu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, niliwahi kuona Serengeti, wakati fisi wanagombea mfupa utadhani kwamba na huu ukoo baada ya mfupa huu utavunjika, hauvunjiki bwana si ni ufisi tu bwana? Ni shughuli ya ufisi tu inafanyika, akishapata mfupa fisi mmoja basi mambo yamekwisha, undugu unabakia, kambi zote zinakwisha inabakia kambi ya fisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisemi kwamba Waheshimiwa 11 waliochukua fomu kugombea Urais ni fisi, hapana, wao ni wanadamu lakini wamefanya mambo yao vizuri na kistaarabu kama fisi wa Serengeti. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, walipokuwa 11 ingekuwa wao ni fisi, natoa mfano tu Mheshimiwa Spika, kuna fisi sita walisema aah bwana hapa pagumu wakawaachia fisi watano bora. Baadaye fisi wawili wakasema aah, bwana sasa sisi wawili tutoke tuwaachie fisi watatu bora na baadaye akabaki mmoja, wamepongezana na yamekwisha.

Mheshimiwa Spika, nikizingatia kwamba hili ni Bunge la mwisho na huenda nisipate nafasi, nakuja kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, msimu umefika. Huko tunakokwenda kwenye Majimbo ni sawa sawa na mfano huu kwamba mifupa imekuwa michache fisi tumekuwa wengi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuna fisi watakaourudi na kuna fisi wengine hawatarudi. Sasa tusizuiane, tukaribishane, mradi ni fisi tukaribishane, halafu akibaki fisi mmoja inakwisha inabakia kambi ya fisi tu basi. Kambi nyingine zote tunafunga kama walivyofanya wenzetu Kitaifa. *(Kicheko/Makofi)*

Baada ya hayo machache, naomba sasa niseme kwamba msimamo wangu, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naiunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda. *(Makofi)*

Mimi nimetumwa na watu wa maeneo mawili, lakini wale wa upande mmoja wa *East African Community,* hotuba ya Waziri wa Fedha imejibu vizuri sana na mimi kwa maoni yangu nawashauri kwamba ni vizuri wakaenda wakachukua fedha zilizokuwepo na kama kuna madai mengine kwanza si unapata chochote halafu unakuwa na nguvu ya kwenda kushughulikia masuala mengine kama hiyo nia bado ipo? Ushauri huo ni mzuri, waende wakachukue kwanza kilichopo halafu kama kuna nia nyingine ya kudai zaidi, majibu yalikuwa ni mazuri wafanye hivyo mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna ndugu zangu wa kiwanda kimoja Arusha kinaitwa Kiwanda cha *Fiberboard.* Kiwanda cha *Fiberboard* kimebinafsishwa na baada ya kubinafsishwa kuna wafanyakazi wa zamani 354. Wafanyakazi hao katika madai wanayodai wamekwishalipwa *pension* yao lakini kuna mafao yao mengine yanayotokana na Mkataba Na.3 wa mwaka 1995 ambapo unadai kwamba kama kuna faida fulani ambayo itatokana na kazi waliyoifanya basi wao wanastahili kiasi fulani. Taarifa nilizonazo wanadai sio pungufu ya shilingi bilioni 1.5 kama nimezidisha sijazidisha sana na kama nimepunguza sijapunguza sana. Wanadai, ni haki yao.

Mheshimiwa Spika, ninayo nia ya kuwasifu sana Baraza...

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. CHARLES M. NYERERE:** Eeeh! *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Ya kwanza.

**MHE. CHARLES M. NYERERE:** Ninayo nia ya kuwasifu Baraza la Mawaziri kwa kazi yao nzuri lakini hawa ndugu zangu wanadai hizi fedha wapo na kwa haraka nitataja baadhi yao ambao wanawawakilisha wenzao katika kesi ambayo tayari iko Mahakamani na kesi hiyo imekwishaamuliwa na Mahakama kwamba walipwe. Mzee Herieli Andrew Lyimo, Mama Mwajuma Waziri, Bwana Estomii Ndesisho, Mama Judith Mlela, Bwana Badi Tengisa, Mama Edith Mrisho, Dr. Abdisalaam Koka na wengine wengi jumla yao ni 354 hawa kwa kutolipwa mapema iwezekanavyo wanaadhirika, wanateseka, wanadhalilika kwa kitu ambacho ni haki yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri wa bure kwa Serikali yangu ya Tanzania, kama ambavyo tunapata faida kwa kulipa madeni ya nje, zipo pia faida nyingi sana tutazipata ikiwa tutawalipa hawa wa kwetu hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba wakati wa majibu ya kufunga mjadala huu, Serikali leo katika kikao hiki ijibu fedha hizo ziko wapi, kuna tatizo gani, anazo nani, anazifanyia nini, kwa nini hawapi wenyewe na atawapa lini?

Mheshimiwa Spika, mimi kama nitarudi hapa, sina uhakika, maana mambo haya inabidi fisi wote mkutane halafu muamue fisi mmoja abaki, kama nitarudi mimi nina dhamira ya kufuatilia suala hili mpaka tuone ufumbuzi wake na kama itawezekana basi Serikali ione ufumbuzi wa suala hili unapatikana kabla ya Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba ili na mimi sababu za kutaka kurudi huku ziwe zimepungua. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, nakutakia kila la kheri wewe na familia yako. Wabunge wenzangu nakutakie kila la kheri, tuelewe tu kwamba kuna kurudi au kutokurudi, Mungu atusaidie, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** *Amin!*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wadogo kwa kazi zao nzuri kwenye Wizara hii. Napongeza pia Ujenzi wa Ofisi ya Bunge Zanzibar. Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar wataweza kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi kwani watapata Ofisi zao kwenye jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Elimu ya Juu ni Muungano. Kwa nini Mpango wa MMES sio wa Muungano? Zanzibar tutawapata wapi vijana wengi wenye sifa za juu wa kuingia Vyuo Vikuu kwa idadi kubwa kama hawajaandaliwa sawa sawa na wenzao walio chini ya mpango wa MMES?

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya huduma za kiuchumi, naipongeza Serikali kwa kuandaa mpango wa MKUKUTA ili kupunguza umaskini hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kuwa utafiti ulishafanywa kwa muda mrefu kuhusu ujenzi wa daraja *(Bridge)* la kutuunganisha Zanzibar na Bagamoyo ili tuweze kusafiri kwa barabara kutoka Zanzibar hadi Tanzania Bara, je, kwa nini kwa mwaka huu 2005/2006 haijatengwa fedha? Umaskini unazidi Zanzibar na njia nzuri ni kupata nafasi zaidi ya kuweza kuuza samaki na matunda kwa wingi na wakiweza kusafiri na barabara kwa wakati wote kuja Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi, kwanza, elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi kuhusu uwezo wa kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kiuchumi.

Ombi langu kwa Idara ya Elimu ya Watu Wazima ni kuwa ingepewa jukumu la kuelimisha wananchi kuandaa miradi yao ambayo wataweza kupata mikopo. Tatizo, kubwa ni hizo *write ups,* wananchi hawawezi kulipwa.

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Spika, naomba awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Frederick Sumaye, Waziri Mkuu kwa kusimamia kwa umakini mkubwa shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge kwa kipindi cha miaka 10 mfululizo. Nampongeza yeye na Mawaziri wa Nchi katika Ofisi yake, Katibu Mkuu na wataalamu mbalimbali kwa matayarisho mazuri ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2004/2005 na mwelekeo wa bajeti ya mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, nitachangia maeneo matatu katika hotuba hii ya bajeti. Eneo la kwanza linahusu Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini. Pili, ni uwezeshaji wananchi kiuchumi na tatu sekta ya uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA kama ilivyoelezwa, Mkakati huu umelenga kukuza uchumi, kuimarisha na kuiwezesha Tanzania kufikia malengo ya Dira ya mwaka 2025. Katika eneo hili nashauri Serikali iongeze mkazo kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula kwa kuhakikisha kuwa eneo linalolimwa linaongezeka kwa kutumia zana bora na za kisasa na kuongeza tija kwa matumizi bora ya utaalam, mbegu bora, mbolea na dawa za kuzuia magonjwa ya mimea na hifadhi ya mazao. Lakini kipato cha wananchi kitaongezeka kama usindikaji wa mazao utawekewa mkakati badala ya kuendelea kutamka tu, kuwa tusindike mazao. Uwekezaji katika kilimo na usindikaji unahitaji fedha nyingi, hivyo Serikali haina budi kuingia kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi, eneo hili ni muhimu sana kuwapa fursa wananchi kumiliki uchumi ikiwa ni njia ya kuondoa umaskini. Nashauri Serikali itazame maeneo mawili hapa. Katika kurasimisha mali za

wananchi hasa nyumba zilizoko katika maeneo yasiyopimwa mijini Serikali isije ikahalalisha uendelezaji na uimarishaji wa maeneo yasiyopimwa na kuifanya miji yetu ibaki kama *squater*. Pili, Mashirika yaliyouzwa, ihakikishwe yanaendeleza biashara ilivyodhamiriwa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uzalishaji mali katika sekta hii Serikali iwe na mikakati thabiti kuhakikisha kuwa wazalishaji katika nyanja mbalimbali wanapewa msukumo wa kuzalisha bidhaa za ubora na ushindani katika soko huria badala ya kutilia mkazo bidhaa za *SIDO* ambazo nyingi haziuziki katika soko la ushindani. Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha viwanda vya kukodisha kwa wananchi wenye nia, ujasirimali na ujenzi wa kuendesha biashara za namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimechagua haya matatu kwa nia ya kuongeza msisitizo juu ya kukuza uchumi na kuongezea wananchi kipato.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu ambayo imesheheni maelekezo yanayotoa misingi ya Bajeti za Wizara moja moja.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima nachukua nafasi hii ya kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri, pia nawapongeza Mawaziri wote wawili katika Wizara hii, Katibu Mkuu pamoja na Menejimenti yote ya ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nataka niuelekeze katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu kilimo. Kwa kuwa wananchi walio wengi wanategemea kilimo, naiomba Serikali iongeze wataalam na wataalam hao waende vijijini ili wawafahamishe wakulima kulima kwa utaalam, wakulima wengi wanajilimia tu na ndio maana mazao yanayopatikana huwa hayatoshi. Lingine Serikali ipunguze bei ya mbolea ili wakulima waweze kuinunua rai yangu nyingine naiomba Serikali ichukue hatua ya kuwafahamisha wakulima kutumia mbolea ya asili kama vile mbolea ya samadi na mbolea ya mboji, iwapo wakulima watafahamishwa vizuri namna ya kutumia mbolea hizo za asili, wakulima walio wengi ambao hawana uwezo wa kununua mbolea ya Serikali watapata nafasi ya kutumia mbolea hiyo ambayo haina gharama ya kifedha.

Mheshimiwa Spika, faida nyingine itakayopatikana wakati wa kutumia mbolea ya asili mbolea hiyo inasaidia kutunza ardhi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kuondoa Umaskini, pia naipongeza Serikali kwa hatua nzuri inayofanya ya kupunguza umaskini na hatimaye kuondoa kabisa. Pamoja na hatua ambazo Serikali imechukua kuhusu kusimamia vizuri kuhusu kuondoa umaskini, mimi nitoe rai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijana wahamasishwe wajiunge katika vikundi vya ushirika ili Serikali itoe fedha za mkopo na baadae waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, yawepo mafunzo maalum kwenye Vyama vya Ushirika, kwa sababu vyama vingi vya Ushirika hawajapewa mafunzo na kwa maana hiyo ndio maana baada ya uzalishaji, hawajui wauze wapi. Hivyo ni vizuri uwepo utaratibu wa soko ili baada ya uzalishaji wanaushirika wajue sehemu ya kuuza bidhaa zao.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu Fredereick Sumaye, kwa hotuba yake nzuri na yenye uchambuzi wa kina ambao ulitupitisha katika kipindi chote cha miaka 10 ambayo amekuwa msimamizi wa shughuli zote za Serikali katika Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chote tulichokaa naye, Mheshimiwa Frederick Sumaye ametoa ushirikiano wa hali ya juu kwangu binafsi na Wabunge wengine wote jambo ambalo limeonyesha mfano wa kuigwa kwa viongozi wengine wote katika ngazi mbalimbali.

Katika kipindi chake cha uongozi tumeona mafanikio makubwa katika nyanja zote za huduma muhimu kama afya, elimu, maji, kilimo, mifugo, barabara, umeme, simu, vyombo vya habari na kadhalika. Ninao wajibu mkubwa wa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuonyesha utumishi na uongozi wa kutukuka.

Si hivyo tu, katika kipindi hicho tumeona amani na utulivu ambao usingekuja tu hivi hivi kama isingekuwa ni jitihada na uwezo alio nao Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Benjamin William Mkapa, kwa kumteua kwa vipindi vyote viwili mfululizo jambo ambalo limetupa fursa ya kuchuma hazina kubwa aliyokuwa nayo Mheshimiwa Waziri Mkuu katika masuala ya uongozi na maendeleo kwa ujumla. Ni wajibu wangu pia kumpongeza Rais Benjamin Mkapa kwa kutupitisha vizuri katika mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi bila ya msukosuko wa aina yoyote ile.

Hata hivyo naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu itusaidie kupata ufumbuzi na pia kutoa msukumo kwa ombi la wananchi wote wa jimbo la Siha hususan wale waishio *West Kilimanjaro* ambao wote ni Maskota ambao waliomba kupewa shamba la *Journey Send* ambalo watalitumia kwa ajili ya kupata makazi ya kudumu.

Ni maoni yangu kuwa kama ubinafsishaji wa mashamba ya *NAFCO* utafanyika bila kujali ombi hilo, zoezi hilo linaweza kuingia dosari, kitu ambacho kwa kweli hatutarajii kwani wananchi wameiwezesha vizuri sera ya ubinafsiahaji na hawana Upinzani wowote ule kuhusu sera hiyo. Ombi hilo lilipitishwa kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, wakati alipofanya ziara katika jimbo la Siha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Mkoa wa Rukwa una tatizo la muda mrefu la uwanja wa ndege. Hadi sasa hatuna ndege

hata moja inayofanya kazi zake za kawaida Mkoani humo. Ndege zinazokuja Rukwa ni zile ambazo zimekodishwa au za viongozi wanaokuja kufanya ziara mkoani kwetu.

Mheshimiwa Spika, imezoeleka kuwa wananchi kuona ndege inakwenda kwenye tope na viongozi walioko kwenye ndege kulazimika kuteremka na mfano kamili wa suala hili ni Waziri wetu Mkuu wa sasa alipokwama katika uwanja ule na kuchelewesha safari yake ya kwenda Mwanza kwa takriban saa mbili.

Mheshimiwa Spika, tangu wakati huo hadi sasa hali ya uwanja huo haijaboreka vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba wananchi wa Mkoa wa Rukwa kupitia Bunge hili Tukufu wapate majibu ya mambo yafuatayo:-

(i) Ni lini Serikali itaufanyia matengenezo fasaha uwanja huo ili kuwaondolea wananchi hofu ya kukwamakwama kwa ndege zijapo Sumbawanga?

(ii) Ni lini Serikali itatuwekea ratiba maalum ya mawasiliano ya ndege katika Mkoa wa Rukwa japo mara moja kwa wiki?

Mheshimiwa Spika, naomba jibu na naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri Mkuu Mheshimiwa Frederick Sumaye na Mawaziri wote wawili wanaomsaidia Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatibu, kwa kazi nzuri walizozifanya kwa kipindi hiki kinachoishia mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze kwa hatua nzuri ya kuhakikisha kuwapimia wananchi wa maeneo ya Oysterbay, Chang'ombe na Mailimbili, hatua nzuri imefikia lakini naomba sana, fedha zile shilingi 30,000 isiishie zoezi la kuweka namba tu katika milango, watu wanahitaji hati miliki za nyumba zao. Watu hawa wana imani na Serikali yao kuwa zoezi hili litakamilishwa kabla ya Waziri Mkuu kung'atuka.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Serikali kwa kusimamia suala zima la amani na utulivu. Nazidi kusisitiza, Waziri Mkuu asimamie vurugu zinazofanywa na Vyama vya Upinzani kwa kuwa wamejua hawatapata kura, sasa wanaendeleza chuki kati ya wananchi na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, tumeshukuru sana, chombo cha *TVT* ambacho ni cha Serikali kinakidhi haja ya wananchi maeneo mengi palipo na umeme hongera *TVT*. Naomba sana ili Watanzania wote wanufaike na matangazo yanayotolewa *live* Bungeni tena Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru vyombo vya habari vimetenga vipindi kwa ajili ya kutoa Elimu ya Mbio za Uchaguzi, kipindi hiki hakipendelei chama chochote.

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki, kinawapa nafasi wananchi ya kujua ni gari lipi linawafaa wapande. Nitashangaa wakisema *TVT* au *ITV* vinapendelea CCM. Si kweli, nawaomba wale wote wanaotaka kupata maelezo ya vyama vya siasa kupitia televisheni tajwa, ombi langu ni kuwa muda uongezwe zaidi wa vipindi hivyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM imefanya mema mengi sana, maendeleo yanaonekana kama barabara, vituo vya afya, maji, elimu na kadhalika vimeboreshwa na barabara zinaendelea kutengenezwa. Naipongeza sana Serikali ya CCM

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana kwa ushirikiano mzuri kati yangu na ofisi hii ya Waziri Mkuu. Niwatakie kheri kwa wale Mawaziri wawili uchaguzi mwema. Aidha, nimtakie maisha mema Mheshimiwa Frederick Sumaye, maana ametuaga hatagombea tena.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono asilimia mia kwa mia.

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nianze kutoa pole kwa wananchi wa Kilombero kwa kufiwa na Mbunge wao mpendwa Mungu ailaze roho ya marehemu peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wake wote pamoja na wataalamu wao kwa kuandaa hotuba nzuri kama hii iliyoweka wazi pande zote na kueleweka vizuri wenye kutupa matumani pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nichangie sehemu mbili upande wa kisiasa na pili upande wa *TASAF.*

Mheshimiwa Spika, upande wa kisiasa mimi nataka nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa hapa tulipofikia.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa ukilinganisha na huku nyuma tulikotoka mimi ninaamini kwamba wananchi wameshaelewa nini makusudi ya baadhi ya vyama vya siasa hususan *CUF* kwamba lengo lao ni kuwasambaratisha na wanadanganya kwa maslahi yao wenyewe viongozi si kwa wanachama wao, wanachama wao wengi sasa wanarudi CCM wakiamini ndicho chama pekee kinawapenda wanyonge na ndicho kinacholeta maendeleo nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, mimi sikubaliani kusema kwamba Chama Tawala ndicho kinachotaka kuvunja muafaka si kweli. Wao *CUF* ndio wanaotaka kuvunja muafaka kwa vitendo vyao wanavyofanya vya vurugu na vitisho hata kuwafanyia vitendo vya kupinga na kuua watu wangapi wamewadhulumu maisha yao leo wanasingizia CCM. Lakini tunasema *CUF* hawana ubavu wa kutawala kwenye nchi hii watabakia kufuata mdundiko wala hawaujui wa nini.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa upande wa *TASAF* nataka nimshukuru Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, kwa kuanzisha mradi huu wa *TASAF* kwa sababu

umetuokoa Watanzania wengi. Namwomba na Awamu ya Pili ifuate nyayo hizo hizo ili tupate kufaidika Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nataka niongezee kuhusu televisheni zetu hasa hii ya Kitaifa *TVT* na *ITV* iongeze mitandao yake ili ifaidike nchi nzima. Kwa sisi tulioko vijijini kwa mfano kama kwenye jimbo langu la Kiwani hatufaidiki na vyombo hivi kwani hatupati. Naomba Serikali itilie mkazo ili sisi tufaidike na vyombo hivi kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo kuhusu UKIMWI kwa kweli bado UKIMWI umetuvaa pamoja na Serikali imechukua juhudi kwamba kwa mgonjwa lakini bado linazidi kuathiri. Mimi ningeishauri Serikali badala ya kufanya semina mbalimbali sasa ichukue hatua zaidi kutilia mkazo ya kwenda kwa kupimwa zaidi kwa wananchi wote kwa kila Kijiji na yule atakayebainika ana virusi basi wapewe alama maalum kwamba yeye ni mwathirika ili watu wapate kumtambua kwa sababu waathirika wengine ni wakorofi sana wanajijua wao ni waathirika lakini wanafanya kwa makusudi tendo la ngono ili apate kumwambikiza na mwingine lakini kama watapewa alama maalum basi pengine mtu ataweza kumfahamu, hatakubali tendo la ngono.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo napenda niungane na wenzangu kwa kuwapongeza Wagombea wetu wote CCM tulio wachagua kwenye Mkutano Mkuu kuanzia mgombea wa Rais wa Tanzania Bara na Rais wa Zanzibar na mgombea mwenza, Makamu wa Rais. Awape ushindi wa juu zaidi ili tuiendeleze Tanzania yetu kwa ujumla na sisi atupe ushindi wa juu kwenye majimbo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wake wote wawili, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Ofisi hiyo kwa jinsi walivyotekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa hali ya juu. Naunga mkono hoja hii kwa dhati.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo kadhaa ambayo naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu iyashughulikie na kuyatolea maagizo.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu *NGO's* zinazoshughulikia UKIMWI nyingi zinafanya kazi kwa ajili ya faida ya wajumbe wenye *NGO's* zenyewe. Haziendi sehemu ambazo hazitawaletea maslahi ya albaki kwa shughuli zao. Mfano, Mkoa wa Rukwa, pamoja na miradi tuliyoiandaa kusaidia waathirika, lakini bado kuna kigugumizi cha utoaji wa fedha hizo. Nashauri mgao uwe unawekwa bayana. Utashangaa kuona jinsi maeneo fulani yalivyopokea fedha nyingi ambazo hazilingani na kazi iliyofanywa. Fanyeni utafiti huo.

Mheshimiwa Spika, pili, mwaka huu wa uchaguzi utakuwa na upungufu mkubwa wa chakula nchini, naelewa tathmini ya kwanza imeonyesha hilo. Kwa kuzingatia tatizo la kuchelewa kuagiza chakula toka nje na kutokana na kuletewa chakula ambacho wakati mwingine hufika huku na kikiwa kimeharibika na ukizingatia hasara tuliyoipata miaka

michache iliyopita na kulazimika kuingia hasara ya mamilioni ya fedha, je, si ingekuwa wakati muafaka kwa sasa mahindi yote yaliyoko Mkoani Rukwa (tani 32,000) yakasafirishwa hadi Shinyanga na Makambako kabla ya msimu mpya wa ununuzi na kabla ya mvua kuanza, nini azma ya Serikali kuhusu hali hii?

Mheshimiwa Spika, tatu, ningemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu asaidie kuangalia upya Sera ya Madaraka Wilayani na uhusiano wa wataalamu wa Makao Makuu ya Wizara na wale wa Wilayani. Kumeanza kutokea *(vacuum)* kati yao kwa kudhani kuwa kila mmoja hawajibiki kwa mwingine. Hatari ya utaalamu kuanza kuporomoka na kufanya kuwepo na tabaka la Makao Makuu na Halmashauri ya Wilaya kwa upande mwingine. Uwajibikaji huu upewe uzito unaostahili *(Long term programme).*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Bunge hili ndilo linamaliza muda wake, lakini yapo mambo mengi ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyasimamia vizuri na kuyachukulia hatua, wakati mwingine hata Bunge kufahamu. Je, isingekuwa jambo zuri wakati wa *wind up* ya Waziri Mkuu akasemea hata kidogo hatua zilizochukuliwa na Serikali kuhusu tuhuma za *TVT* na mkandarasi aliyohusika amechukuliwa hatua zipi. *TVT* bado vifaa vyake vinaendeshwa kwa matatizo, naelewa wahusika wanajua tatizo ni nini pia.

Mheshimiwa Spika, dawa za kulevya na uvutaji bangi, unywaji pombe usio na mipaka, lazima viende sambamba na vita dhidi ya UKIMWI. Fedha zinazotengwa kwa ajili hii ni ndogo sana ukilinganisha na madhara yake kwa Taifa. Huu ni ugonjwa mwingine hatari kama UKIMWI. Ipo *NGO* moja hapa nchini ambayo imeanza kazi nzuri ya kushirikisha vijana wa rika mbalimbali katika kusaidia Taifa lisiingie katika janga hili hatari. *SOBER TANZANIA* ndilo jina la *NGO* hiyo ambayo inafanya kazi nzuri kwa watu kujitolea bila hata kujali maslahi yao binafsi. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu anaweza kuwasaidia vipi ili washirikiane na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya?

Mheshimiwa Spika, nami kwa kuwa ni kipindi cha kumaliza muda wa Bunge, nitumie nafasi kumshukuru na kumtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ndugu yetu Frederick Sumaye, kwa jinsi alivyotuongoza kwa hekima, busara na mshikamano kwa vipindi vyote viwili akiwa Waziri Mkuu wetu. Amefanya yale yote aliyotakiwa kuyafanya kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi.

Mimi binafsi nampongeza kwa utulivu aliouonyesha kwa muda wote huu, pamoja na kutupiwa madongo huku na kule, lakini alisimama kidete kutetea Serikali hadi leo hii. Nitaendelea kumwombea azidi kwa njia moja au nyingine kutoa ushauri, uzoefu kwa Serikali ya Awamu ya Nne na chama chake cha CCM. Naunga mkono hoja.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Katibu Mkuu pole na kazi. Ninayo maombi rasmi kwenye hotuba yangu ya ukamilishwaji wa umeme - Mkwajuni/Kanga, maji visima vitano, upatikanaji wa Kata Mwambani na Magamba na upatikanani wa Vijiji Ilasilo na Ndanga. Hayo ni kero kubwa sana kule kwangu ahsante nisaidie.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia hoja hii ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Fredereick Sumaye, naiunga mkono hoja hii. Ingawa ninayo machache ambayo ningependa Serikali iyajue na iyafanyie kazi upande wa jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kuboresha hali ya jimbo la Songwe baada ya kuanzishwa katika hali hiyo pia yapo mapungufu kama ifuatavyo. Lipo tatizo la kusimamisha kupeleka nguzo na umeme kwenda Kijiji cha Kanga na Galula. Kama wao *TANESCO* walivyoahidi, inashangaza muda waliousema sasa umepitwa na wakati. Hili litaleta upinzani mkubwa kwa sababu mradi ule umekwishaanza na umezoroteshwa tu na viongozi wa *TANESCO* pengine kisiasa. Naomba Waziri Mkuu afuatilie suala hili lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni juu ya Wizara ya TAMISEMI. Wilaya tuliomba kuwa tupate Kata mpya mbili, Kata ya Mwambani kwa maana Kata ya Mkwajuni ni kubwa sana, Kata ya Mwambani tuliomba iwe na vijiji vya Mwambani, Mawombwe, Chikombe, Mbala na Iseche. Kata ya Mkwajuni iwe na vijiji vya Mkwajuni, Saza, Kaloleni, Miembeni na Patamela.

Pili, ni Kata ya Magamba ambayo nayo inatoka kwenye Kata kubwa ya Galula, kata ya Magamba inakuwa na Vijiji vifuatavyo Magamba, Nahalyongo, Ilembo na Isita. Galula yenyewe ina vijiji vya Galula , Ilasila, Iwombwe, Sawi na Itindi. Pia bado tunasubiri kiblali cha kupewa vijiji ambavyo maombi yapo TAMISEMI ni kama ifuatavyo:-

1. Kijiji cha Ilasilo toka Kata ya Galula;
2. Kijiji cha Ndanga Kata ya Mbuyuni.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi naomba Kata mpya mbili za Mwambani toka Kata ya Mkwajuni na Magamba - toka Kata ya Galula. Pia naomba vijiji viwili vya Kijiji cha Ilasilo - toka Kata ya Galula na Kijiji cha Ndaga toka Kata ya Mbuyuni.

Naomba Waziri Mkuu utoe majibu kwa nini hili halikufanyika ingawa kumekuwa na maelezo tofauti. Wananchi wanalalamika sana Waziri Mkuu na sisi tunawakilisha watu wanapotutuma wanapenda wapewe majibu au haki yao, sio kutoa sababu zisizo na msingi.

Mheshimiwa Spika, maombi haya yalipelekwa TAMISEMI tangu walipohamia hapa Dodoma. Naomba nipewe majibu au vibali vya muda kwa suala hili.

Suala la tatu ambalo ni tatizo ni juu ya maji katika vijiji vya Galula, Mbuyuni, Mkwajuni, Mbangala, Kapalala. Wizara ilishachimba visima viwili katika Galula, viwili Mbuyuni na kimoja Mbangala, jumla vitano. Baada ya kazi nzuri ya Wizara bado visima vipo hapo hapo, havitoi maji wakati huu wa uchaguzi imekuwa kebehi kubwa kwangu na Chama cha CCM. Mara kwa mara nimewaona wafanyakazi wa Wizara ya Maji na wametoa ahadi kuwa wametenga shilingi milioni 20 kukamilisha suala lile la maji. Nalo lina mtazamo wa kisiasa kuwa wapo wafanyakazi wasiopenda visima vile vikamilike

kwani tatizo ni nini? Upo mradi wa maji wa *CARITAS* naomba nayo Serikali ichangie. Naomba majibu juu ya suala hili la visima vitano kutokamilika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Shule za Sekondari unaendelea vizuri kati ya Kata kumi sasa tunajenga shule Kata sita na hasa kuzingatia *catchment areas* kufika Jimboni Songwe kwa Waziri Mkuu kumehamasisha sana, kuanza ujenzi wa shule tatu kwa mpigo za Sekondari. Bila shaka tutamalizia Kata zilizobaki kwani hizi zinazojengwa kwa kasi tutazifungua mwaka kesho 2006.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Waziri Mkuu kwa kututembelea kule Songwe yeye pamoja na Mama Esther Sumaye. Nampongeza katika uongozi wake chini ya Rais Benjamin Mkapa. Naomba vikamilishwe hivi nilivyovisema kwa wakati huu ili isiwe hoja ya Wapinzani. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza mtoa hoja Mheshimiwa Frederick Sumaye, Waziri Mkuu, aliyoitoa kwa ufasaha mkubwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naleta maandishi haya kuunga mkono hoja asilimia mia moja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Serikali Bungeni na majukumu yake mengine alivyopewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mawazo yangu yafuatayo:-

Kwanza, wagonjwa na waathirika wa virusi vya UKIMWI. Napendekeza vituo vya kutoa dawa za kurefusha maisha viteremshwe zaidi ili kila Kituo cha Afya nchini kitoe dawa hizi. Aidha, ushauri nasaha uwe ni sehemu ya tiba na wagonjwa kila wanapopewa dawa wapewe ushauri wa kutoambukiza wengine na kutojiongezea virusi zaidi.

Katika kutoa dawa hizi, siku moja tu imetengwa mfano Hospitali ya Mkoa Dodoma, ni kila Jumatano. Siku hii moja haitoshi, zingatia hawa ni wagonjwa, anayeshindwa kufika siku hiyo moja anaumia maana ataishi wiki moja bila dawa.

Napendekeza, sehemu ya kliniki ya kutoa dawa za kurefusha maisha iwe wazi kila siku kwa siku zote za kazi kwa wiki na maelekezo yatolewe mwenye dharura amwone nani?

Mheshimiwa Spika, hii ni bajeti ya uchaguzi na pia haina budi kuzingatia mtazamo wa kijinsia kwamba wagonjwa wa UKIMWI wanawaelemea zaidi wanawake. Kwa hiyo, nafuu ya wagonjwa ni heri ya wanawake.

Naomba wanawake wasaidiwe kwa kupata dawa za wagonjwa wa UKIMWI karibu. Pia iwe kila siku kwa siku za kazi kwa wiki.

Pili, napenda nichangie kuhusu uboreshaji wa elimu nchini hususan Elimu ya Sekondari. Tumefungua shule nyingi na jimbo langu ni mojawapo. Nashukuru juhudi zote zilizofanyika sasa naleta maombi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, badala ya fedha za MMES kuanza kupelekwa Shule za Sekondari kubwa na za zamani, macho yaangalie kwanza kule kwenye shule changa. Shule changa bado zina kazi kubwa ya ukamilishaji majengo ya shule hizo, ikiwa ni pamoja na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, napendekeza shule changa ziwe za kwanza kupewa fedha za MMES. Wananchi wako tayari kuchangia, msaada huu usicheleweshwe.

Mheshimiwa Spika, tatu naomba huduma ya afya ienezwe zaidi. Wananchi wanaishi maeneo mengine ni magumu kufika eneo la huduma. Katika juhudi za kupunguza umaskini na kujenga uchumi, afya ni mtaji. Kwa hiyo, ni bora kabisa huduma hizi ziwe katika kila eneo wanakohitaji na wako tayari kuchangia. Kwa hiyo, natoa wito kwa Taifa, kwamba Serikali iongeze nafasi za mafunzo na ajira kwa wataalamu wa afya wa ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, nne na mwisho kwa mchango wangu ni kuiomba Serikali iziangalie barabara zinazopita katika vikosi vya Jeshi, iwe lami. Naomba barabara inayokwenda na kupita kikosi cha Jeshi 21 KJ Kaboya, Muleba Kaskazini, inayoanzia Ntungamo Kanyinya iwekewe lami. Hii inapita kwenye shamba la Mashujaa, naomba iangaliwe ili iwekewe lami.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ni kuomba Serikali iweke utaratibu mzuri sana na unaoeleweka kushughulika na sekta ya kilimo. Kilimo ni sekta msingi, lakini tumebaki kutegemea mvua tu. Hili ni hatari. Umwagiliaji maji katika mashamba makubwa ya kilimo unatarajiwa kuanza lini? Ipo mikopo ya wanawake, vijana na *SACCOS* na *SACAS.* Je, lini msaada utaelekezwa katika kilimo ili, kilimo kichangie kupeleka mazao ya Tanzania nje.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya Serikali kwa hoja nilizowasilisha. Nakushukuru sana.

**MHE. SIJAMINI MOHAMMED SHAAME:** Mheshimiwa Spika, na mimi kwa niaba ya wananchi wapiga kura wa jimbo la Kitope naanza kwa kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa kmia.

Aidha, sasa napenda kuungana na Wabunge wenzangu waliotangulia kutoa mkono wa pole kwa wananchi wa Kilombero kwa mara nyingine kumpoteza Mbunge wao kipenzi marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, kwa kuacha dunia na Mungu kwa kumhitaji. *Ya Allah* amlaze malezi mema peponi. *Amin.*

Hotuba iliyotolewa kwa Bunge hili na Mheshimiwa Waziri Mkuu Frederick Sumaye, imeandaliwa kama kawaida kisayansi ambayo kama alivyosema mwenyewe imeeleza utekelezaji wa Serikali yetu kwa kipindi chake chote cha Serikali ya Awamu ya

Tatu cha miaka kumi. Hotuba hii haikusaza wala kuficha kitu chochote na kwa ukweli huo na uadilifu wake, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote wa Wizara yake pamoja na Makatibu Wakuu wake pia na Watendaji wake wote. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipongeza hotuba hii mimi ninasisitiza tena kumwomba Waziri Mkuu kuangalia uwezekano wa kushauriana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu mwenendo wa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ (Zanzibar).

Mimi binafsi napata taabu kuona nchi moja yenye chama kimoja viongozi wake wa Mikoa hawatambuani na wala *geography* ya nchi yao hawaitambui ingawa hili suala si la Muungano lakini kutakuwa na ubaya gani viongozi hawa kutambuana, kutembeleana na hata kuwa na tabia ya mkutano wa pamoja kuzungumzia mambo yao. Mimi nina hakika wakiwa na utaratibu wa kujuana na kupata fursa ya kuzungumzia mazingira yao basi Tanzania itazidi kupanuka na kusaidiana.

Mheshimiwa Spika, ujirani mwema ni asili yetu kwani sababu ya Muungano wa Tanzania imetokana na tabia hiyo na ndiyo chombo ambacho kitaimarisha zaidi imani miongoni mwetu na kuaminiana zaidi. Aidha, mfumo huu utaua na kuondosha imani potofu za hawa Wapinzani wanafiki na wazushi wanaopanda mbegu nyaufu ya Wazanzibara kwani mimi ulipobuniwa mfumo wa vyama vingi nilidhani kuna lengo la kuipa changamoto Serikali na katu sikudhania mfarakano.

Mheshimiwa Spika, mimi sikudhania hata mara moja kuwa Zanzibar itakuwa mandhari nzuri kwa Upinzani mpotofu na uchochezi miongoni mwetu na pahali pa maandalizi ya mapambano miongomi mwetu, pahali pa kuwakashifu viongozi wetu wakuu wa nchi hii. Nilitarajia wao wanaojiita wasemaji wa wanaowawakilisha wanyonge na wanaodai haki zao basi wangalikuwa wanaifanya kazi hiyo Tanzania nzima. Bara na Visiwani badala ya kuitumia Zanzibar kisiwa cha amani na utulivu peke yake.

Mheshimiwa Spika, Upinzani maana yake si vurugu kwa Serikali ambazo zinawahifadhi na kuwastiri wao wenyewe kwani huo si uungwana wa Kitanzania hasa kwa kuzingatia kuwa Waswahili wa Tanzania wanasema; *"Huwa fadhlaka huwa saidaka."* Na kwa maana hiyo sasa Serikali imefikia kuamini kuwa sisi kule Zanzibar tumeshachoshwa na bughudha zao. Sasa huyu Mheshimiwa ambaye anasajili vyama eti haoni kuwa kuna chama ambacho kina kila dalili na kuendeleza maadili ya kigaidi kinaachiwa huru kuwa siku moja wananchi wanaweza kuchoka nacho na kuamua kwa kufuata sheria ya nchi ya vyama vingi? Namshauri *Registrar* atupumzishe kwa kufumbua macho kwa hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Frederick Sumaye kama Waziri Mkuu ameeleza nia yake ya kutogombea nafasi ya Ubunge lakini bado ni mwanachama mahiri wa CCM. Bado namwombea afya njema katika maisha yake yote na pia namwomba asisitize kwa Mawaziri wa Serikali zetu mbili wawe wanaendeleza utaratibu wa mikutano

ya Serikali zetu mbili kwa kutumia mazungumzo kwa yale mambo ambayo tunadhani yanaleta bughudha kwa Muungano wetu, badala ya utaratibu ambao unafanywa na baadhi ya Mawaziri wa Serikali zetu kutumia vyombo vya habari mfano *Radio, TV* na magazeti kusema mambo ambayo hayasaidii kuleta masikilizano katika kuendesha Serikali zetu na kuimarisha Muungano wetu mzuri sana na imara zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kuunga mkono hotuba hii.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ya bajeti. Ninayo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Kwanza ni upungufu wa chakula katika jimbo langu la Nanyumbu kutokana na sababu mbalimbali. Zipo sehemu za jimbo ambazo zilikumbwa na balaa la panya ambao walishambulia mbegu wakati wa kupanda mashambani. Juhudi za wananchi wengine kurudia kupanda mbegu hazikusaidia kwa vile kila walipopanda mbegu zingine zilishambuliwa zote na panya. Kwa wananchi waliobahatika mbegu zao kuota mazao yake yalishambuliwa na panya hao. Mazao mengine yalishambuliwa baada ya kuvunwa na kuhifadhiwa ghalani.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mengine yaliyokumbwa na wanyama waharibifu. Maeneo kuzunguka hifadhi ya Pori la Akiba la Lukiwika Lumesula limeathirika sana na wanyama hao hivyo kupelekea mazao kushambuliwa mashambani. Uharibifu huo umetokea zaidi katika vijiji vilivyomo katika Kata za Napacho, Chipuputa, Nanyumbu na Masuguru.

Nashauri Serikali ifanye tathmini ya kina ya hali ya chakula Jimboni Nanyumbu kwa kushirikisha Serikali za Vijiji vyote. Hii itapunguza lawama zilizotolewa huko nyuma ambapo tathmini hufanywa katika maeneo machache na msaada wa chakula kufuata nyayo hizo hizo hivyo kuzua malalamiko kutoka kwa wananchi waliokosa misaada ya chakula ilihali nao walikuwa wanahitaji misaada hiyo kutokana na kukabiliwa na njaa.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine sugu katika jimbo la Nanyumbu ni kukosekana kwa maji. Maeneo mengi yana upungufu mkubwa wa maji. Vijiji vingi havina maji hasa majira ya kiangazi. Ni kawaida kwa akinamama kutembea kilometa nyingi kufuata maji au kutumia saa nyingi kisimani kungojea zamu ya kupata maji. Kuna miradi michache ya maji ambayo imeanza kujengwa kupitia miradi ya *TASAF.* Karibu miradi yote imekwama kutokana na sababu mbalimbali. Mradi wa maji wa Ndwika - Mangaka umekwama baada ya kuishiwa mabomba na fedha za mradi kwisha kutokana na makadirio mabaya ya watalamu Wilayani. Mradi wa Bwawa la Nangomba umekwama baada ya fedha kumalizika kutokana na usimamizi mbaya wa mradi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Bwawa la Manene nao umekwama kama ule wa Nangomba. Miradi mingine ambayo imesimama katika hatua mbalimbali ni miradi ya

mabwawa ya Maratani, Namasogo, Mpwahia na Mpombe. Ni vizuri miradi hiyo ikakamilishwa ili wananchi waondokane na adha ya kukosa maji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kuhakikisha huduma ya maji inaboreka katika jimbo la Nanyumbu kwa kupeleka miradi mingi zaidi ya maji.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa Serikali itayafanyia kazi haya yote. Mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza wewe binafsi kwa moyo na uwezo wako mkubwa kuliongoza Bunge lako hili Tukufu kwa vipindi vyote ulivyojaliwa kuongoza, Mungu akupe umri mrefu wenye kheri na baraka.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mkono wa pole kwa wananchi wa Majimbo yale yaliopoteza Wabunge wao yaani Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria na Marehemu Abu Kiwanga. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Aidha, nina heshima kubwa kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kuwateua Mheshimiwa Jakaya Kikwete kuwa mgombea wa Urais wa Tanzania na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kuwa mgombea mwenza. Vile vile ninampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume kuwa mgombea Urais wa Zanzibar kupitia chama chetu cha CCM. Mwenyezi Mungu *Inshallah* atajaalia kupatikana ushindi mkubwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wake na Watendaji wake wote kwa hotuba nzuri iliyogusa maeneo yote ya Jamhuri yetu ya Tanzania kimaendeleo, naamini hotuba yake ni dira kuu kwa maendeleo ya Taifa hili. Naomba sana tuithamini na tuitekeleze kama dira ya maendeleo ya nchi yetu. Aidha, Mheshimiwa Waziri Mkuu nakupongeza sana kwa nia yako kwa kutaka kupumzika, nakutakia kila la kheri na mafanikio mema.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwenye suala la kupanda kwa uchumi wetu Tanzania. Mimi nakubali kupanda kwa uchumi wetu, lakini naomba sana tuiangalie Hali ya Uchumi katika sehemu yetu ya pili ya Muungano wetu ya Zanzibar. Zanzibar bado iko chini kidogo kiuchumi. Biashara imeshuka sana kiuchumi, Uwanja wa Ndege umepungua mapato yake. Katika hali hiyo naomba sana tusaidiane kuhusu Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hali ya Zanzibar juu ya mawasiliano bado yanahitaji msaada, barabara zake nyingi hali yake mbaya, hali ya usafiri wa bahari na anga unahitaji kuangaliwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, narejea kusema tena naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninaiunga mkono hotuba hiyo kwa asilimia kwa mia. Ahsante.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia kwa mia hotuba ya bajeti ya mwaka 2005/2006 kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu.

Nina hoja mbili ambazo naomba sana zifikiriwe, kwanza kipo Chuo cha Serikali za Mitaa huko Hombolo, Wilayani Dodoma Mjini. Chuo hicho kilijengwa kwa dhumuni la kuboresha utendaji wa watumishi wa Serikali za Mitaa Kitaifa. Uzoefu uliopo hadi sasa wanaosoma hapo ni watumishi wa kada ya chini ya Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na Miji. Hivi kwa nini chuo hiki hakitumiki kutoa mafunzo ya *Orientation* na *Refresher Courses* kwa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri Kitaifa? Kwa kufanya hivyo mimi naamini Wakurugenzi watakuwa wameandaliwa vizuri zaidi kufanikisha shughuli za maendeleo kwa Wilaya/Miji husika.

Pili kwa miaka minne hadi sasa Halmashauri za Ulanga na Namtumbo tumekuwa tukikutana kwa lengo la kuunganisha barabara mbili za Mkoa, Lupilo - Kilosa kwa Mpepo (Mkoani Morogoro) na Lumecha - Kitanda (Mkaoni Ruvuma). Kiungo chenyewe ni barabara ya Wilaya kati ya Kijiji cha Kilosa kwa Mpepo hadi Kitanda kwa kuvuka Mto Ilondo (ambao ni mpaka kati ya Mkoa wa Ruvuma na Morogoro). Tutashukuru sana iwapo Waziri wa Ujenzi ataendelea kusaidia kujenga Daraja la Mwatisi na Daraja la Furua pia barabara ya kuunganisha (Kwa Mpepo hadi Kitanda Kijijini) na Daraja la Mto Ilondo pia barabara ya kuunganisha vijiji vya Kitanda na Kilosa kwa Mpepo.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kitanda hadi Kilosa kwa Mpepo Lupilo itakuwa na faida zifuatazo, kuunganisha Mikoa ya Ruvuma na Morogoro, kufupisha usafiri baina ya Kijiji Kitanda na Mikumi, kufanikisha Utalii katika hifadhi ya *Selous Game Reserve,* kuharakisha kilimo kati ya Lupilo na Kijiji cha Kitanda, kurahisisha Uchukuzi wa mazao ya biashara na kilimo baina ya Mikoa ya Ruvuma na Morogoro na kurahisisha shughuli za *Irrigation* katika bonde zuri la Kitanda (Mawanga) ambako zipo hekta zaidi ya 6,000 zilizoainishwa kwa kilimo cha mpunga.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2005/2006. Ahsante.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata maoni hii ili niweze kuchangia katika hoja ya Waziri Mkuu. Naomba nianze kwa kutoa rambirambi kwa familia na ndugu wa Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero. Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuchaguliwa kwake kupeperusha bendera ya CCM katika Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Oktoba, 2005. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza wa Mheshimiwa Jakaya Kikwete na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kuwa mgombea wa urais wa Zanzibar kutoka CCM.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara yake ambayo imekuwa ya kina na ya matumaini kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali kwa kazi nzuri ambayo imekuwa inafanya. Nianze kwa matokeo ya Kamati aliyoiteua Waziri Mkuu kuchunguza madai ya walimu. Kamati hiyo imefanya kazi nzuri sana. Ushauri wangu ni kwamba Serikali basi imalizie malipo haya kwa walimu hawa.

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu Jimboni Tabora Mjini. Mwaka 2000 Tabora kulikuwa hakuna Kampuni za simu za mkononi, hivi sasa kuna Kampuni tatu, *Vodacom, Celtel* na *Mobitel.* Mwaka 2000 Tabora hakukuwa na Kampuni za Redio zinazotangaza kwa masafa ya *FM,* hivi sasa kuna Redio tatu, *CG FM Radio, Radio Free Africa* na *Voice of Tabora.* Mwaka 2000, barabara ya Manyoni-Itigi-Kigwa-Tabora ilikuwa inapitika kwa shida na wakati wa masika haipitiki kabisa, hivi sasa inapitika mwaka mzima na mabasi yanaenda mpaka Dar es Salaam. Mwaka 2000 madarasa ya Shule za Msingi nyingi yalikuwa hoi kabisa, hivi sasa tumejenga madarasa ya kudumu mengi katika mpango wa MMEM kwa msaada wa Serikali na nguvu za wananchi. Mwaka 2000 uwanja wa ndege wa Tabora ulikuwa hautumiki ikinyesha mvua kidogo tu, jambo ambalo limerekebishwa kwa ukarabati. Mwaka 2000 Kiwanda cha Nyuzi cha *TABOTEX* kilikuwa kimefungwa, hivi sasa kimeanza kufanya kazi. Mwaka 2000 kulikuwa na shida ya madawa katika hospitali zetu Tabora, hivi sasa dawa zimeongezwa.

Mwaka 2000 Mjini Tabora hakukuwa na *x-ray* katika hospitali zetu, hivi sasa kuna mashine za *x-ray* mbili katika Hospitali ya Mkoa ya Kitete na nyingine aliyoleta Mbunge itasimikwa Isevya. Mwaka 2000 hakukuwa na stendi ya mabasi ambayo hivi sasa ipo. Mwaka 2000 kulikuwa na kituo kimoja cha *CG Television,* ambapo hivi sasa matangazo ya televisheni ya Taifa yataanza muda si mrefu kutoka katika kituo kilichoko *Kazeh Hill.*

Mheshimiwa Spika, orodha ya mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2000 jimboni Tabora Mjini ni ndefu sana. Hongera Serikali ya Chama cha Mapinduzi!

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Manispaa ya Tabora wanaiomba Serikali iwe mbia nao katika kuufungua Mkoa wa Tabora. Ombi la kwanza ni kwamba barabara zifuatazo zijengwe kwa kiwango cha lami, Manyoni - Itigi- Tabora- Urambo- Kigoma, Nzega - Tabora, Tabora- Sikonge-Ipole-Ruangwa-Mbeya na Tabora- Sikonge- Ipole - Koga - Mpanda - Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuendeleza ukarabati wa Reli ya Kati ili iweze kubeba mizigo mingi.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu katika jimbo la Tabora Mjini mvua hazikuwa za kutosha hivyo kuna uwezekano wa njaa. Naomba Serikali ijiandae vya kutosha ili pindi

njaa ikaitokea wananchi waweze kusaidiwa haraka. Sisi huko Tabora tumeshaambiana kuhifadhi chakula tulichonacho.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza tena Serikali kwa kuanzisha mradi wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), mradi huu ni muhimu sana kwetu Tabora kwa maana tumeazimia kuanzisha Shule za Sekondari nyingi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu mia kwa mia.

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri iliyokamilika kwani amefanikiwa kuyatolea taarifa mambo yote aliyoyasimamia kwa mafanikio makubwa katika miaka yake kumi na kuwa Waziri Mkuu. Nampongeza na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kutoa rambirambi kwa jamaa, ndugu na familia za Waheshimiwa Wabunge wenzetu wanne waliotutangulia mbele ya haki. Marehemu Kepteni Theodos Kasapira, Marehemu Frank Mussati, Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria na Marehemu Abu Towegale Kiwanga, aliyekuwa Mjumbe mwenzetu katika Kamati ya Uwekezaji na Biashara.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa mchango wangu wa mawazo katika kuijadili hotuba ya Waziri Mkuu napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, mwana CCM, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuchaguliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea wa kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nina hakika kiti hicho atakichukua.

Vile vile niwapongeze Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa na CCM kuwa mgombea wa Urais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2005. Sote tuna hakika kwamba CCM itapata ushindi wa kishindo.

Mheshimiwa Spika, kama Waziri Mkuu alivyobainisha katika hotuba yake ametueleza kwa uwazi hali tuliyokuwa nayo katika nyanja mbalimbali mwaka 1995 hali tuliyonayo sasa baada ya miaka 10 na huko tunakoelekea. Miaka 10 ya Awamu ya Tatu chini ya uongozi shupavu wa jemadari hodari Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, yamepatikana mafanikio makubwa ya maendeleo ya kusifika, siyo tu hapa kwetu nchini bali hata katika Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu hapa nchini tangu wakati wa Azimio la Arusha, kauli mbiu ya maendeleo ilikuwa watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora wa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, akaongoza mtaji. Ukioanisha hayo na maeneo matatu ya kipaumbele katika MKUKUTA ni kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato, kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii na kuimarisha utawala bora na uwajibikaji utapata msingi imara wa kujenga Tanzania kiuchumi, kijamii na

kisiasa. Mwongozo ni Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 na msingi wa utekelezaji ni MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini tukizitumia hotuba za Mheshimiwa Rais wetu ambazo amewahi kuzitoa hapa Bungeni kwa nyakati mbalimbali na hotuba ambazo amekuwa akitutolea wananchi kila mwisho wa mwezi, tukizitumia kama rejea *(reference)* zitatusaidia sana kupata uelewa jinsi tunavyoweza kusukuma gurudumu la maendeleo katika nchi yetu kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, tutakuwa tumetimiza wajibu wetu kuitolea tafsiri sahihi kwa vitendo hotuba ya Waziri Mkuu kwenye majimbo yetu ya uchaguzi katika muda mfupi uliobaki kwa kutegemea kuwa mawazo yake ya busara yataendelezwa hata baada ya Bunge hili kumaliza muda wake.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie machache yenye kuhusika na MKUKUTA. Kwanza ni kuhusu Menejimenti ya Rasilimali Ardhi. Ardhi ni rasilimali ya msingi katika shughuli zote za binadamu na kwa Watanzania walio wengi vijijini ndiyo chanzo kikuu cha kipato chao. Bado hatujaitumia ardhi vilivyo. Wananchi vijiji wanastahili kuelimishwa, watambue kuwa ardhi kwao ni msingi wa kuwainua kiuchumi na kuwaondoa kwenye umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Spika, pili ni kilimo cha kisasa na ufugaji wa kisasa, wananchi waelimishwe kwa mifano iliyo wazi juu ya kilimo cha kisasa na ufugaji wa kisasa. Huduma za ugani vijiji ziimarishwe. Inafaa kila Kata iwe na shamba la mfano wa kilimo cha kisasa na wanyama waliofugwa kwa njia za kisasa na wananchi wote katika Kata na Vijiji wasimamiwe na waagizwe watekeleze ufugaji wa kisasa na kilimo cha kisasa bila kukosa.

Kuhusu ushirika, lazima juhudi za ziada zichukuliwe kuendeleza na kuboresha ushirika vijijini. Ushirika ni sera ya msingi ya CCM na wana CCM, tunatambua kwamba ushirika ni chombo cha kuleta maendeleo ya wananchi na kukuza nguvu za uchumi. Wananchi wanahitaji kuelimishwa, kuhamasishwa na kuondolewa woga walio nao juu ya suala zima la ushirika. Uundwaji wa vikundi vya uzalishaji mali vijijini utumike kama hatua ya kwenda kwenye ushirika kamili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukuza huduma za mitaji vijijini, tatizo kubwa lililopo ni kwamba utamaduni wa kujiwekea akiba na kukopa bado haujachangamkiwa na kushamiri vijijini. Wananchi vijijini wanahitaji kuelezwa kuwa kuingia katika utamaduni wa kujiwekea akiba wataweza kujilimbikizia mitaji ya kuwawezesha kujikwamua kiuchumi. Njia mbalimbali zilizoanzishwa na Serikali za Mikopo ziwekewe msukumo wa kutosha na kuwaeleza wananchi jinsi watakavyofaidika, *SACCOS* ni kielelezo cha wazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imebuni njia mbalimbali za kuwainua wananchi kiuchumi ambazo zimeelezwa katika hotuba ya Waziri Mkuu. Viongozi wa Serikali wa ngazi zote wachukulie kuwa ni wajibu wao kufikisha ujumbe huo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala la UKIMWI bado linatuhangaisha. Kila takwimu zinazotolewa mwaka hadi mwaka zinaonyesha kuongezeka kwa maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Pamoja na kwamba zipo sasa dawa za kurefusha maisha, lakini utoaji na utumiaji wa dawa hizo unahitaji utaalamu wa hali ya juu na kusimamiwa kwa makini kabisa ama sivyo baada ya miaka machache kama dawa hizo zitatolewa holela zitakuwa hazifai na kushindwa kurefusha maisha. Tusiwape matumaini makubwa wananchi kiasi kwamba kila muathirika anadai apatiwe dawa hizo. Utoaji wa dawa hizo taratibu zake za kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba Kamati zimeundwa katika ngazi za Vijiji, Kata na Wilaya bado Kamati hizo hazipewi nyenzo za kufanyia kazi na hata fedha. Iko haja ya kuweka utaratibu unaoeleweka wa kufuatilia na kusimamia kazi zinazofanya na Kamati hizo.

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumzie juu ya utawala bora na uwajibikaji. Natoa ombi maalum kuwa Wilaya 24 zilizobainika kuwa zinastahili kugawanywa baada ya uchambuzi wa kina kama ilivyoelezwa na Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wakati wa kujibu swali Na. 11 la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, ziwekewe *time table* ya utekelezaji na Wilaya ya Kilosa kama ilivyoorodheshwa iwemo ikiwezekana katika mwaka huu wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika,naunga mkono hoja na pongezi sana Waziri Mkuu na Watendaji wa Ofisi yake. Mafanikio yaliyopatikana kwa Serikali ya Awamu ya Tatu ya Rais Benjamin Mkapa yamesimamia kwa kiasi kikubwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye. Nampongeza sana!

Mheshimiwa Spika, Hospitali yetu ya Mkoa wa Shinyanga ilipata pigo kwa kufiwa na Madaktari wake wawili. Hadi sasa Serikali imeletewa Daktari mmoja tu Dr. Nyawawa. Pamoja na kwamba hata wale Madaktari kabla hawajafariki kulikuwepo na upungufu mkubwa wa Madaktari. Huduma ya upasuaji hata kwa wazee walioshindwa kukojoa wanateseka sana ni vyema tupatiwe Madaktari haraka sana. Naomba nipate majibu, Serikali imechukua hatua gani kusaidia suala hili la mahangaiko.

Suala la UKIMWI halipewi fedha za kutosha. Hadi leo *NGO* zote zilizoomba fedha kwa kupitia Manispaa na kukabiliwa hata senti moja haijatolewa na fedha za kwenda Manispaa hazijatolewa. Hivi hii vita kweli tutashinda kwa mtindo huu wa kubania fedha. Watu wetu wanakufa kwa wingi sana katika maeneo ya mjini kama Shinyanga maambukizi ni asilimia 10.7. Hivi ni kitu gani kimetokea kupewa maaneo tu badala ya kupatikana fedha za kupambana na vita hii. Kama uwezo wa upatikanaji wa fedha ndio huu basi tutaishia kufariki. Nitapenda kuelewa nini kimekwamisha suala hili.

Mimi nimekuwepo Bungeni kwa muda wa miaka 10 sasa na ajenda yangu imekuwa kufuatilia ubinafsishaji wa Kiwanda hiki cha nyama. Hadi leo pamoja na maelekezo ya Waziri Mkuu kwa Waziri mhusika na idara husika hadi leo kazi hii haitajekelezwa. Hivi kuna tatizo gani kuhusiana na jimbo hili. Kwa nini hasa uzembe huu ni wa nani. Naomba nipate majibu wakati kwa kujumuika kwa hoja za Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa nini kiwanda hiki kimeshindwa kuuzwa. Wafanyabiashara wa Shinyanga wameomba lakini hakuna lolote. Nitashukuru kupata majibu ya mkwamo huu!

Mheshimiwa Spika, nyumba na ofisi ya Mahakama ya Mwanzo iliungua moto. Nawaomba mara kwa mara nimeomba ofisi hiyo ijengwe lakini hadi leo hamna kinachoendelea! Pamoja na Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba aliagiza Mahakama hii ijengwe maana imeleta athari sana. Naomba suala hili lipatiwe ufumbuzi

Mheshimiwa Spika,tuliahidiwa Mahakama Kuu Mkoani kwetu, naomba sana tuonewe huruma kuwepo na Mahakama Kuu kushughulikia kesi za mauaji ya vikongwe na kadhalika. Naomba suala hili lishughulikiwe mapema maana Mkoa uko tayari kutoa ardhi ama hata majumba ya kununua.

Pamoja na kazi nzuri ya Awamu ya Tatu hivi suala hili la mauaji ya vikongwe kweli Serikali imeshindwa kulikabili? Nchi nyingi hata mtu mmoja akiuawa ni *issue* Serikali yote inalishughulikia, hivi inakuaje watu zaidi 30 kuuawa tunaona ni suala la kawaida na amani tuliyonayo na tunayojidai kuitangaza mbona hawa vikongwe hawana msaada.

Naomba suala hili Serikali ilivamie na kupatikana utatuzi wa suala hilo la siku nyingi, kweli Serikali imeshindwa kutatua hili suala? Kwa nini Serikali na utaalamu ilivyo nayo Jeshi la Polisi na kwingineko imeshindwa kupata fedha mahsusi za kushughulikia janga hili?

Kuhusu usafiri wa Reli, kukolombwezeka kwa *TRC* na *TAZARA* kwa Serikali kutoa fedha za kutosha kununua *rolling stock, locomotive,* kwa sasa hali mbaya sana mizigo inapakiliwa Dodoma kutoka Dar es Salaam na kutoka Bara. Hivi mpango wa kujenga reli kutoka Isaka hadi Kigali (Rwanda) itasaidia nini? *TAZARA* yenyewe imekolombwezwa hakuna mizigo. Reli ni muhimu sana kwa uchumi kinachotakiwa ni kuweka umeme kwa reli. *Electrify the rail* na kuboresha *permanent way.* Kwa kuwa nchi nyingi zinazopakana na Tanzania ni nyingi naamini tukiwa na reli imara uchumi wetu utaboreka sana. Reli hudumu ya miaka mingi kuliko barabara tukiboresha reli uchumi wetu utakuwa imara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini ni hafifu sana, kwa kifupi tunaibiwa! Maana *factors of production* ziko tatu. Ardhi, Mitaji na Utumishi. Kwa nini wawekezaji hawatoi *share* kwa ardhi yetu. Mapato ya mchanga kwa miaka mitano *US$ 286 million,* Serikali imepewa *US$ 4. million!* Asilimia 0.025? Kwa nini Serikali imeamua kuwapa wawekezaji mali yetu bure pamoja na kwamba hatuna mtaji amba ni Ardhi yetu? Je, hivi mtu anaweza kuwekeza hewani? Serikali irekebishe dhuluma hii.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kazi nzuri ya Mheshimiwa Frederick Sumaye (Mbunge), Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri iliyoandaliwa vizuri. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala bora, hongera sana kwa utawala bora. Yapo matatizo yanayojitokeza hivi sasa kama yatazoeleka yataleta mitafaruku kwa jamii. Nayo ni kutumia nguvu za kupita kiasi kwa *FFU,* Polisi, virungu hata kuchoma moto makazi ya wazee, vijana wachuuzi na wanavijiji wanaotaka kuhamishwa, mtindo huo naomba ufe mara moja. Kama kuna Mkuu wa Mkoa au Wilaya ana hamu ya vita, naomba aombe nafasi ya Ukuu wa Mikoa ya Burundi, Zaire hata Darfur. Nchi yetu ni ya amani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TVT* naomba maelezo ya kina kuhusu *TVT,* inazimika zimika nafikiri mitambo ile ina mashaka au mafundi hawakuishauri vizuri Serikali juu ya uagizaji na uwekaji wa mitambo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Spika, kwa maoni yangu naomba sana Mheshimiwa Pius Msekwa, aendelee kugombea ili tuingie naye jengo jipya. Hii ni kutokana na kwamba, Waziri Mkuu kwa mujibu wa kauli yake atakuwa mpya, kwa hali hiyo, Spika naye akiwa mpya Bunge litakosa busara zenu tutazikosa wote kwa mpigo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba umshauri Spika agombee ili msiondoke kwa mpigo, muombe ili abadilishe uamuzi kama naye alipanga kutogombea, siko tayari kupata mlipuko wa kuondoka viongozi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Makatibu Wakuu na Baraza la Mawaziri, natoa shukrani kwa Makatibu Wakuu wa Mikoa na Mawaziri wote kwa kazi nzuri katika kipindi chote hiki cha uhai wa kuwa katika nyadhifa zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Makao Makuu, hivi sasa tunapoandaa mipango ya kuhamia Dodoma, je, hivi sasa Makao Makuu ya Tanzania ni wapi, Dar es Salaam, Dodoma au Arusha? Naomba kipindi hiki cha mpito Makao Makuu yasiwepo hadi hapo tutakapohama na kuhamia.

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima naomba kuunga mkono hoja hii moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu ruzuku ya mbolea. Utaratibu huu wa kutoa ruzuku kwenye mbolea ni mzuri na muhimu sana. Hata hivyo, naomba nishauri marekebisho ya msingi katika utaratibu huo hasa kwa Mkoa wa Iringa hususan Jimbo la Kalenga. Mbolea ambazo zinapewa ruzuku kwa asilimia 50 hivi ni mbolea aina ya *DAP* au *Urea.* Lakini mbolea aina ya *CAN* inapewa tu ruzuku ya usafirishaji, hivyo bei yake bado inabaki ya juu sana kwa mkulima wa kawaida. Kuna maeneo yaliyo na mwinuko sana ambayo *Urea* inafaa sana. Lakini sehemu nyingine *(lowlands)* ukitumia *Urea* mahindi yanakua na kurefuka mno bila

kubeba mahindi ya kutosha yaani punje ndogo sana na chache sana. Maeneo hayo hufaa kupandia mbolea aina ya *DAP* na kukuzia na mbolea aina ya *CAN.*

Hivyo ikiwa ndivyo nashauri kuwa kiasi hicho cha fedha za ruzuku kwa Mkoa wa Iringa Serikali irekebishe uwiano wa ruzuku kwa kupunguza ruzuku kidogo katika mbolea ya *Urea* na kiasi hicho cha ruzuku kiwekwe kwenye mbolea aina ya *CAN* ili nayo bei ipungue kwa kiasi fulani ambayo ina unafuu kwa mnunuzi yaani mkulima.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine linahusu mishahara ya Waheshimiwa Madiwani. Suala hili ni muhimu sana lipatiwe ufumbuzi mapema iwezekanavyo. Kazi za Mbunge haziwezi kuwa na mafanikio bila kushirikiana kwa karibu sana na Waheshimiwa Madiwani walioko kwenye Kata za Jimbo. Ni muhimu sana wawe na vyombo vya kufanyia kazi yaani Ofisi Makao Makuu ya Kata na chombo cha usafiri walau pikipiki wapewe mikopo. Wakati huo huo wawe na mshahara unaoeleweka. Sasa hivi tumetambua umuhimu wa Maafisa Watendaji wa Vijiji wanapewa mishahara ili Serikali za Vijiji zitengemae, sembuse Waheshimiwa Madiwani. Hata shughuli za Chama (CCM) Makatibu wa Kata na Matawi watapata baiskeli. Haya ni mambo mema. Sasa tufanye maamuzi ya dhati kuhakikisha kuwa Waheshimiwa Madiwani wetu wanapewa mafao yafaayo.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nitamke kuwa naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge 2005/2006 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, pamoja na Serikali kuanzisha maeneo machache mapya ya utawala, kupeleka huduma kwa wananchi, kurahisisha utendaji na kuboresha utawala bora, zoezi lilikuwa *isolated and piecemeal.* Baada ya sensa ya idadi ya watu na makazi ya mwaka 2002, Watanzania wengi tulitarajia Serikali ingezitumia takwimu za zoezi hilo ambalo hufanyika mara moja baada ya miaka 10 vyema kwa gharama kubwa, kuboresha mipango ya maendeleo ya wananchi kwa kutumia takwimu za sensa ya mwaka 2002, Serikali ingefanya mapitio mahsusi ya maeneo ya utawala na uwakilishi kwa lengo hilo la kusogeza huduma kwa wananchi, kurahisisha utendaji, kuboresha uwakilishi na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, zoezi hilo ni muhimu kufanyika ili kuleta mgawanyo sawa wa rasilimali na maendeleo sawia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuanzisha programu mbalimbali kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa uzalishaji katika sekta ya kilimo, kazi kubwa bado kufanyika. Ili kweli uwezo wa sekta ya kilimo utumike kikamilifu kwa faida ya wananchi, Taifa haliwezi kukwepa kuanzishaji wa programu mahsusi za kilimo cha

umwagiliaji. Hicho ndicho kilimo cha uhakika. Vinginevyo kuendelea kutegemea kilimo cha mvua kwa sehemu kubwa ya maisha ya wananchi ni kujidanganya.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyorejewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika aya ya 26 ya hotuba yake kuhusu ongezeko la hekta zilizoendelezwa chini ya mpango kabambe wa kilimo cha umwagiliaji hayaridhishi hata kidogo. Nchi hii kubwa, inayojivunia zaidi ya hekta milioni 6 za ardhi inayofaa kwa kilimo *(arable land),* ongezeko la hekta 107,573 tu za kilimo cha umwagiliaji hadi hekta 250,573 ni mzaha katika Taifa hili ambamo pamoja na jitihada zote za wananchi, wanakabiliwa na njaa mara kwa mara kutokana na kutegemea kilimo cha mvua ambapo mara nyingi ukame hutokea.

Mheshimiwa Spika, lazima tuanzishe kilimo cha umwagiliaji kama jawabu la pekee la kukifanya kilimo kuwa kweli uti wa mgongo wa uchumi wetu, kuleta mapinduzi katika maendeleo ya Watanzania na kuwaondolea umaskini.

Mheshimiwa Spika, zipo ishara chanya katika kufanikisha hili. Baadhi ya ishara hizo ni pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali hivi karibuni kuanzisha *Warehouse Receipt System* na *Rural Energy Fund.* Hatua hizi hata hivyo, lazima zitengewe fedha za kutosha kutoka kwenye bajeti ya Serikali; sio kutegemea wawekezaji binafsi.

Aidha, sambamba na hatua hizo, barabara za vijijini lazima zitengenezwe kwa kiwango cha kupitika mwaka mzima ili kufungua maeneo ya uzalishaji na kuwapatia masoko ya uhakika kwa mazao yao wazalishaji ambao wengi wao wako vijijini.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, lazima Taifa liwekeze kikamilifu katika miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji. Pawepo programu mahsusi za uchimbaji mabawawa, uvunaji wa maji na utumiaji wa maji ya mito. Programu hizo ziwe na malengo yanayopanuka na yanayotekelezeka kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya marehemu Abu Kiwanga na wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kifo cha ndugu na kiongozi wao. Mwenyezi Mungu apumzishe roho yake kwa amani. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Ofisi hiyo kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa miaka 10 ya Awamu ya Tatu ya uongozi wa nchi yetu. Kazi yao imepafanya Tanzania pawe mahali pazuri zaidi kuishi.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza kuona upinzani unabeza kazi ambayo imefanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu. Huu ni ushahidi tosha kuwa upinzani katika Tanzania hawajui maana ya upinzani na kuwa hawawezi kuchukua uongozi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inajitosheleza na inajibu maswali yote ambayo nilikuwa nayo. Hata hivyo, naomba nitoe mawazo yangu juu ya mambo machache.

La kwanza, vita dhidi ya rushwa. Pamoja na kwamba rushwa husababishwa na mambo mengi sana kubwa likiwa sababu ya kiuchumi, ni lazima jitihada kubwa zaidi zifanyike katika kukubaliana nayo.

Mheshimiwa Spika, rushwa katika Mahakama zetu sasa imekithiri. Mahakama za Mwanzo na za Wilaya ndiyo zinaongoza. Nadiriki kusema kuwa haki sasa kwa kiasi kikubwa inauzwa. Polisi wanaohudumia Mahakama, waendesha Mashtaka, Makarani, Wazee wa Baraza na Mahakimu wanashirikiana kwa karibu katika biashara hii ya haki.

Nashauri sera yetu ya ajira za watumishi wa Mahakama na Polisi iangaliwe upya. Ni jambo la kushangaza kwa Hakimu kuahirisha uamuzi juu ya dhamana ya mshtakiwa kwa wiki mbili wakati zamani lilikuwa ni jambo la kuamua papo hapo. Kwa nini raia wa kawaida asifikirie kuwa hii ni jitihada ya baadhi ya watumishi wa Mahakama kutaka rushwa?

Mheshimiwa Spika, pia, utaratibu wa kutaka barua za utambulisho wa wadhamini ni mwanya mwingine wa rushwa. Polisi na Mwendesha Mashtaka wanakuwa ndio wanaoamua ni nani akubalike kuwa mdhamini au la. Pia, kuna mtindo wa kuwapeleka washtakiwa rumande na kuwaita kudhaminiwa kwa *removal orders.* Nimeona wananchi waliosotea hizi *removal orders* kwa wiki mbili kwa kubabaishwa na Waendesha Mashtaka na Makarani. Naomba Serikali ilirekebishe jambo hili.

Pili, Wazee wa Baraza la Mahakama za Mwanzo. Nashauri umuhimu wao uangaliwe upya. Natoa rai kuwa wao ni sehemu kubwa sana katika upotoshaji wa haki. Tume ya Kurekebisha Sheria imetoa wazo kuwa Mabaraza ya Kata hayajafanya kwa kiwango kilichotegemewa. Ni rai yangu kuwa haya Mabaraza yamebobea katika uuzaji na upotoshaji wa haki. Tatu, Uboreshaji wa Huduma za Mahakama, naipongeza Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa majengo ya Mahakama za Mwanzo, Wilaya na Mahakama Kuu Kanda na Mahakama ya Biashara.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, inashangaza kuona Mahakama ya Ardhi inaendesha shughuli zake katika jengo ambalo halistahili kuwa Mahakama lililoko Upanga, Dar es Salaam. Nimearifiwa kuwa jengo hilo linalipiwa kodi ya shilingi milioni 18 kwa mwaka, fedha ya kodi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Mheshimiwa Rais asishauriwe kutumia madaraka yake ya kutwaa ardhi na kutwaa moja kati ya majengo ya Shirika la Nyumba la Taifa ambayo hayafai *(condemned)* na kujenga jengo la Mahakama ya Ardhi lenye hadhi ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa miongoni mwa wajumbe walioshughulikia shughuli za Mheshimiwa Waziri katika Kamati, kwa hiyo, mchango wangu mkubwa ulikuwa katika Kamati. Kwa hiyo, nilikuwa na nyongeza ya machache, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri sana na kubwa aliyoifanya Serikalini na Bungeni kwa kipindi chote cha miaka 10. Pia naomba kumpongeza kwa hotuba nzuri aliyoitoa ambayo imetoa picha ya kazi nzuri ya utekelezaji wa kazi za Serikali, ambayo imeonyesha mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo machache ambayo ningependa kugusia katika kuboresha utendaji katika maeneo hayo.

Moja, uhuru wa vyombo vya habari. Baadhi ya vyombo hivyo hasa magazeti yanajiingiza katika kupotosha habari na kuleta migongano katika jamii. Magazeti mengine yanapotosha hata habari zinazoandikwa au kuzungumzwa na viongozi wakuu wa nchi. Nashauri kuwepo na sheria na chombo kitakachofuatilia vyombo vya habari vinavyopotosha na kutoa kejeli kwa jamii kisha kuwachukulia hatua za kisheria.

Pili, Vyama vya Siasa. Sheria ya Vyama vya Siasa inaweka wazi uhuru wa vyama hivyo kufanya kazi huru kulingana na taratibu na sheria. Lakini hali inayojitokeza hivi sasa ya viongozi wa vyama vya siasa kutumia fedha ya umma (ruzuku) kwa kuvuruga amani na utulivu ni muhimu idhibitiwe. Kwa kuwa ruzuku ni fedha ya umma, sheria iseme wazi kuwa fedha hiyo ikaguliwe kuona matumizi halali ya fedha hiyo. Utaratibu uwekwe wa kukagua na kuitolea taarifa kwa umma.

Tatu, Uanzishaji wa Vituo vya Utangazaji Mikoani. Nashauri Vituo vya Umma *(RTD* na *TVT)* visambazwe nchi nzima. Miji ambayo imesahauliwa kwa matangazo kama hayo na wanahitaji kujua maendeleo yanayofanywa na Serikali yao kwa usahihi na maendeleo wanayojiletea wenyewe yatangazwe mara kwa mara, ni vizuri vyombo hivi vya Kiserikali vianzishwe katika Mikoa hiyo, mfano kama Mkoa wa Kilimanjaro. Maombi hayo yalikwishapelekwa Ofisi ya Waziri Mkuu (Habari) bado halijatekelezwa.

Nne, kuhusu utalii napenda kutoa pongezi kwa Serikali kwa kuandaa Mpango Kabambe wa Utalii wa kuendeleza vivutio asilia vya utalii na kubaini vipya. Ningependa kuishauri Serikali kupitia Wizara inayohusika kuelekeza wawekezaji katika mwambao wa Ziwa Nyasa ambako Milima ya *Livingstone* inaleta mvuto mkubwa kwa utalii *Eco-Tourism,* utalii ambao ungeweza kuliingizia Taifa letu fedha nyingi. Milima ya *Livingstone* pia ni maarufu sana kwa madini mengi, hivyo ni vyema pia Wizara ya Nishati na Madini ijitahidi kufanya utafiti wa kina kujua ni kwa kiwango gani au aina gani ya madini yaliyopo kwa faida ya nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo mfupi, naunga mkono asilimia mia kwa mia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Frederick Sumaye, Mbunge, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania kwa vipindi viwili mfululizo vya jumla ya miaka 10. Amejenga uzoefu mkubwa na unadhihirika katika hotuba yake hii ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2005/2006 inayotafsiri kazi za miaka 10 Kitaifa. Nawapongeza pia Watendaji wake kwa kumpa msaada mkubwa. Katika hotuba hii nitaelekeza ushauri na mapendekezo katika maeneo mawili kama ifuatavyo:-

Moja, matumizi ya tafsiri za takwimu. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inaonyesha wastani wa takwimu za miaka 10, mwaka 1995 - 2004/2005. Lakini katika hotuba za Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni za tofauti ya miaka miwili 2003/2004 au 2004/2005. Tofauti ya tafsiri ya takwimu kwa mfumo huo umeleta matokeo tofauti kwa mfano katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji ukurasa wa 9 sehemu (10) inasema: “Ukuaji katika Sekta ya Madini umeshuka.”

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 22 sehemu (30) inasema: “Sekta ya Madini imekua kutoka asilimia 9.7 mwaka 1996 hadi asilimia 15.6 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, hotuba hizi mbili zikisomwa na wawekezaji wawili tofauti, watapata picha tofauti katika sekta ya madini. Inahitaji uelewa wa juu kutafsiri vizuri hotuba hizo hasa katika ngazi ya uelewa wa wananchi wetu. Ni vyema tukaainisha hotuba kabla ya kuzitoa.

Pili, miradi ya *TASAF One.* Mfuko wa *TASAF* umefanya kazi nzuri katika Wilaya zote za majaribio *TASAF* moja. Hata hivyo, miradi mingi haikukamilika na fedha za kukamilisha hazikupelekwa kutokana na muda wa mradi kwisha. Madarasa ya shule za msingi, sekondari na miradi ya maji, haikukamilika. Katika Wilaya ya Muheza, madarasa katika shule tatu za sekondari, Shebomeza, Kisiwani Nkumba na Chifu Mang’enya, pia madarasa ya shule za msingi Kwatango na Mwarimba na mradi wa Maji Kigombe haikukamilika. Hali kama hii ipo katika Wilaya nyingine kama ilivyoelezwa wakati wa semina ya *TASAF* kwa Waheshimiwa Wabunge katika Mkutano wa 19.

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya miradi, wananchi walikamilisha michango yao. Kwa upande mwingine matatizo yalitokana na mapungufu kwa upande wa watendaji wawakilishi wa *TASAF* katika Halmashauri. *TASAF* haikuwa na uwezo wa kuwadhibiti watendaji hao kwa kuwa ni waajiriwa wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo wasimamizi wakuu wa kanuni za matumizi ya fedha za *TASAF* toka Benki ya Dunia ni *TASAF* kwa niaba ya Serikali na kama kumetokea mapungufu basi Serikali isikwepe lawama kuwaachia wananchi maskini wa vijijini. Kama msimamizi wa Wizara zote na shughuli za Serikali ingekuwa vyema

Ofisi ya Waziri Mkuu ikajenga hoja na kuishauri Serikali kutoa fedha kwa Mpango Maalum ili kumalizia kazi (viporo) vya *TASAF One.*

Mheshimiwa Spika, miradi hiyo iliyokwama imesimama na wananchi bado wanangojea fedha kwa Mkataba wa *TASAF One.* Hali hii inaiweka *TASAF One* katika jina baya katika maeneo yenye viporo. Hivi ni lazima tuongoje fedha za *World Bank* tu ndio tujenge mdarasa na miradi hiyo muhimu katika jamii yetu? Kuongoja fedha za *TASAF Two* ili zianze kwa kumaliza miradi ya *TASAF One* hakuongezi tija katika kuhamasisha nguvu za wananchi katika kuanzisha na kuendeleza miradi mipya.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ijenge hoja ya kupata fedha ili miradi hiyo ikamilike na wananchi waanzishe miradi mipya kwa mpango wa *TASAF Two.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo, naipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa hotuba ndefu na nzuri na ninaunga mkono hoja.

**MHE. MWANAMKUU MAKAME KOMBO:** Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono mia kwa mia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri nilipata nafasi ya kuongea kwa mdomo. Nashukuru sana. Lakini nilipozungumza juu ya kupatiwa soko la matunda, nilikusudia pia kwamba inawezekana masoko yapo nje lakini matunda yetu hayako katika hali ya kuweza kuingia kwenye ushindani wa soko, kwa maana ya kuwa hayako kwenye viwango vinavyotakiwa na pia wananchi wetu hawana ujuzi wa kuhifadhi biashara hii ya matunda na kuyafungasha kwa kuyasafirisha.

Kwa hiyo basi, naiomba Serikali iwe na namna maalum au mpango maalum wa kuwafundisha wakulima kwa kuanzia namna ya kuyalima mazao yao kwa kupewa mbegu bora za miti ya matunda mpaka kufikia hatua ya kuyavuna na kuyafungasha kwa kuyasafirisha nje.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, mimi naanza kwa kuunga mkono asilimia mia moja hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na hotuba yenye mwelekeo wa maendeleo ya nchi yetu. Nampongeza sana kwa kazi nzuri aliyokuwa anaifanya kwa takribani miaka 10.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nizungumzie suala la hospitali ya Temeke. Naipongeza Serikali kwa jitihada zake zinazofanywa za kuikarabati hospitali ya Temeke. Pamoja na kazi hii nzuri, bado mimi nilikuwa na ombi, Wilaya ya Temeke inaendelea kupanuka kama inavyoonyesha katika taarifa ya sensa kuwa Temeke ni ya pili kwa wingi wa watu. Hivyo, kutokana na ongezeko hilo tunahitaji kuwa na zahanati angalau kila Kata ili kupunguza msongamano wa wagonjwa kwenye hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, pia liko tatizo la upatikanaji wa dawa kwani mapato ya Manispaa yetu hayatoshelezi kufanya hayo na hasa baada ya kuondoa kodi mbalimbali. Kutokana na hilo Halmashauri zinashindwa kutosheleza mahitaji ya wakazi wake.

Mheshimiwa Spika, narudia kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu kwa hoja hii nitauelekeza kwenye masuala machache muhimu. Kabla sijaanza kwenye masuala ninayotarajia kufafanua. Nichukue nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ya kusisimua na iliyojaa uwazi na ukweli mtupu kuhusu hali halisi ya mwenendo na mafanikio ya maendeleo kiuchumi, kijamii, kiutawala na kiteknolojia katika Taifa letu kwa kipindi 2003/2004 na 2004/2005.

Moja, suala la njaa na upungufu wa chakula. Tatizo hili la njaa au upungufu wa chakula linalowagusa wananchi mara kwa mara sasa lazima lipatiwe ufumbuzi wa kudumu na kwa kufanya hivyo suala hili litazamwe katika marekebisho ya sera za kilimo kwa kulenga mbali na sio ufumbuzi wa papo kwa papo *(long-term planning and programming in agricultural policy transformation).* Nasema hivyo kwa sababu, sasa Serikali inaonekana kama imechukulia kama kukubali kuwa matukio ya njaa au upungufu wa chakula ni sehemu ya maisha ya jamii ya wananchi wetu. Kwa sasa Serikali inachofanya ni kungojea njaa itokee na halafu ichukue hatua ya kutafuta msaada wa chakula au fedha za kununulia chakula na kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya mavuno ya chakula katika Wilaya nyingi hapa nchini imekuwa siyo ya kuridhisha takriban kwa miaka mitatu au minne mfululizo tangu miaka ya 2002, 2003, 2004 na hata mwaka huu 2005. Serikali haijajitokeza na sera ya uhakika kujaribu kujihami na janga hili la njaa mabalo linadhalilisha jamii.

Kwa mfano, katika Wilaya ya Iramba, kata za Kidaru, Tulya, Ntwike, Shelui, Mtoa, Mtekente, na Urughu mwaka huu wa 2005 familia nyingi (kaya) hazitaweza kuvuna mazao ya chakula kufikia hata mahitaji yao ya 1/3 ukilinganisha na mavuno ya miaka miwili ya nyuma. Tatizo hili sio la Wilaya ya Iramba tu - Mkoa wa Kilimanjaro kwa miaka 3 mfululizo (2003, 2004, 2005) haujapata mvua na haujavuna mahindi, maharage na hata ndizi.

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wa tatizo hili la njaa au upungufu wa chakula katika nchi yetu upo ndani ya uwezo wa Taifa hili kama tu suala zima la kujenga mazingira ya kuleta mapinduzi/mageuzi muhimu kwenye sekta ya kilimo. Hivi kuendelea na kilimo cha kisasa cha kutegemea mvua pekee (msimu wa mvua kwa mwaka) ni sera ambayo inalielekeza Taifa hili kwenye maangamizi kwani tupende au tusipende mwelekeo wa miaka ijayo mvua zitaendelea kupungua na kutokutabirika kwa matumizi ya kilimo *(erratic and diminishing rainfall trends in the coming years).* Ulimwengu wote sasa unaelewa tatizo hili na nchi nyingi sasa zimeanzisha sera maalum za kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya kilimo huu ndiyo mkakati wa msingi kabisa wa mageuzi katika kuelekea kwenye kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu kwa kuendelea kufumbia macho suala zima la kuvuna maji ni kitendo kinachofanana na kulea njaa katika sehemu ya jamii yetu. Haitoshi kwa Serikali yetu kuongojea njaa itokee halafu ndio hatua zichukuliwe.

Kinachotakiwa sasa ni kukubali kuweka sawa na wazi sera ya kuvuna maji ambavyo kwa kufanya hivyo hatimaye njaa itatokomezwa kwa kiwango kikubwa katika miaka ijayo. Kama nchi za kwenye majangwa ambazo hazipati mvua hata kidogo kabisa nchi kama za Afrika ya Kaskazini (Marocco, Tunisia, Algeria na kadhalika) tatizo la njaa siyo tukio la mara kwa mara, njaa katika nchi hizi haitokei kabisa, je, itakuwaje nchi ya Tanzania yenye mvua nyingi kuliko hata nchi jirani za Zimbabwe, Zambia, Kenya na kadhalika na yenye ardhi nzuri ya rutuba kwa matumizi ya kilimo iendelee kukumbwa na njaa mara kwa mara na wakati mwingine kwa miaka 3 au 4 mfululizo?

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kushauri Ofisi ya Waziri Mkuu katika Bajeti ya mwaka 2005/2006 ilichukulie suala la matukio ya njaa ya mara kwa mara kuwa ni janga la Kitaifa, kero kwa wananchi na linachangia sana katika kupunguza juhudi za wananchi kupambana dhidi ya umaskini wa kipato cha umaskini wa akili. Kwa hiyo, nashauri kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu itoe mwongozo na maelekezo kwa Wizara ya Kilimo na Chakula kuwa suala la kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya kilimo liwekwe kwenye mikakati ya kujenga mazingira ya kuleta mapinduzi/mageuzi kwenye kilimo. Mikakati hii iwe kwa vitendo na siyo kutayarisha makablasha ya utafiti na ya kinadharia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuweka sera ya kuvuna maji wazi katika Wizara ya Kilimo na Chakuala suala la kuunda Idara ya kuvuna maji na umwagiliaji *(water harvest and irrigation Department)* iwe sehemu ya muundo wa Wizara ya Kilimo na Chakula. Serikali pia ipitie upya na kuona umuhimu wa kutenganisha maji kutoka kwenye Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kufanya hivyo utata wa suala la maji kwa matumizi ya kilimo utaondoka. Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa sasa inaelekeza nguvu zake nyingi kwa kuendeleza upatikanaji wa maji kwa matumizi ya mifugo na binadamu. Itakuwa sio sahihi kuiagiza Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ijenge/ichimbe mabwawa na pia ichimbe mifereji ya kupeleka maji mashambani kwa kumwagilia mimea, kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, ngombe zinaweza zikaswagwa na kupelekwa bwawani kunywa maji, binadamu anaweza kwenda kusimani au bwawani kuchota maji, lakini mkulima hawezi kuswaga mahindi/maharage/kunde/viazi kutoka mashambani kupeleka bwawani au mtoni kunywa maji. Mkulima ni jukumu lake kujenga miundombinu ya mifereji/umeme/pampu kupeleka maji mashambani kumwagilia, hili sio jukumu la Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa itoe tamko rasmi kuhusu sera ya kuvuna maji kwa matumizi ya kilimo na pia Serikali ione umuhimu wa kutenganisha maji kutoka kwenye Wizara ya sasa ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu janga la UKIMWI. Ofisi ya Waziri Mkuu imepewa jukumu la kulilinda Taifa letu na wananchi wake dhidi ya janga la UKIMWI. Kwa sasa misaada ya madawa na chakula ya kurefusha maisha kwa walengwa waathirika hasa vijijini haiwafikii kwa wingi na mahali pengine waathirika wameachwa hivi hivi bila misaada wowote. Tume ya Taifa *(TACAIDS)* inafanya kazi, lakini udhaifu mkubwa upo katika kutokuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na waathirika au vikundi vyao. Misaada mingi sasa inatumika kuendesha semina/warsha/mafunzo na kadhalika.

Pia kuna Mashirika mengi yasiyo ya Kiserikali ambayo yamejiingiza kwa ujanja kufaidika na misaada inayolengwa kwa waathirika wa UKIMWI. Kitendo cha kupitishia kwenye Halmashauri za Wilaya misaada kwa waathirika kitazamwe upya *(to be reviewed)* kwa sababu misaada hii hasa fedha zinazopitishiwa kwenye Halmashauri hatimaye hupangiwa matumizi mengine na sio kuwasaidia waathirika.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nadiriki kuweka wazi kuwa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uongozi wake ulio imara na wenye uadilifu mkubwa kama alivyouonyesha kwa muda wote wa uongozi wake wa nafasi hiyo, katika awamu zote mbili za Serikali ya Awamu ya Tatu ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 16/06/2005 imethibitisha haya. Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imekidhi matarajio ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na wasaidizi wake wote. Naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ni kweli kuwa katika kipindi cha miaka kumi ya Serikali ya Awamu ya Tatu, shughuli za kisiasa nchini zimeendelea kutekelezwa kwa amani na utulivu chini ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Mheshimiwa Spika, amani yetu na utulivu tuliyonayo siyo jambo zuri kubezwa na viongozi wa Vyama vya Upinzani pamoja na vyama vyao. Hatua hii ya maendeleo tuliyofikiwa na ambayo tunategemea kuyafikia hapo baadaye yanatokana na amani na utulivu wetu tulionao ambao misingi yake imejengwa na viongozi wetu waasisi wa Taifa letu hili la Tanzania, pamoja na Serikali zetu zilizopitwa yaani Awamu ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu chini ya vyama vyetu vya siasa vilivyotangulia vya *TANU* na *ASP* na hatimaye Chama cha Mapinduzi (CCM). Kwa kweli misingi hii iliyojengwa na waasisi wetu na sera nzuri za vyama vyetu vilivyotawala Taifa letu hili la Tanzania kuanzia mwaka 1961 hadi leo hii mwaka 2005, ndiyo mambo ya kuzingatia na tuondoe ubinafsi wetu sisi viongozi na vyama vyetu na wananchi wote wa Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tumeelezwa mafanikio yaliyopatikana kuhusiana na daftari la wapiga kura ambapo tunaelezwa kuwa watu 15,942,824 wameandikishwa. Naiomba Serikali pamoja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kuhakikisha kuwa idadi hii ya waliojiandikisha wanapiga kura kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Spika, kuna maneno kuwa idadi hii ya waliojiandikisha, wamejiandikisha kwa ajili ya kupata hivi vitambulisho tu. Kwa hiyo, mikakati iandaliwe ili watu hawa kwa asilimia kubwa wapige kura katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu wa 2005.

Mheshimiwa Spika, napenda nikiri kuwa Muungano wetu ni kweli unaimarika siku hadi siku. Naomba Serikali ya Muungano wa Tanzania kwa yale ambayo yanafanywa Zanzibar na Serikali ya Muungano yawekwe wazi kama vile zipelekwe fedha za *TASAF* kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar. Mambo kama haya yataondoka ile dhana kuwa Zanzibar hainufaiki na Muungano.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya uchumi wa Zanzibar pamoja na bandari ya Zanzibar pamoja na matatizo yanayofikiriwa, lakini kwa kweli suala la siasa linachangia kudhoofisha uchumi na maendeleo ya Zanzibar. Mivutano ya vyama vyetu Zanzibar, migogoro ya wananchi wa Zanzibar, wafanyabiashara wakubwa wenye uwezo wa kuagiza vitu (bidhaa) kutoka nje ambao wako katika upande wa Chama cha Upinzani, inaonyesha kupunguza kuagiza bidhaa kutoka nje wengine kuhamishia uingizaji wa bidhaa zao kupitia Tanga, Mombasa na maeneo mengine ya nchi yetu na nchi jirani na pia wapo ambao wamehamishia masuala yao ya kibiashara Tanzania bara badala ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika kulishughulikia suala hili ni vizuri tukaangalia maeneo haya na kukaa nayo pamoja na kuyashughulikia na kuyasawazisha. Zanzibar tunalazimika kuwa wakweli na kujenga umoja kwa kuondoa tofauti zetu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Napenda kuishauri Serikali kujenga misingi mizuri ya kiutendaji ndani ya vyombo vyake vikuu na muhimu viache kulumbana isivyo na msingi na kusababisha kuonekana kuwepo udhaifu wa Serikali. Kwa suala lililotokea hivi karibuni kuhusu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Haki za Binadamu kuhusu wananchi wa Serengeti. Ninaiomba Serikali kuondoa malumbano kwa vyombo vyake vikuu kama hivi ili kuondoa udhaifu ndani ya Serikali yetu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha programu ya mabadiliko katika Sekta ya Afya. Naipongeza sana Serikali, lakini naiomba Serikali kuhakikisha kuwa ile Mikoa ambayo haina Madaktari bingwa kupelekewa Madaktari hao ili kuwapatia huduma za matibabu yaliyo bora na ya mafanikio kwa jamii ya Watanzania wote. Pia ninaipongeza sana Serikali kwa kutilia mkazo huduma ya maji hapa nchini. Lakini juhudi hizi ninaomba ziendelezwe na kuimarishwa kwa nguvu zote hasa Vijijini ambako umbali wa upatikanaji wa maji uko mbali sana.

Mheshimiwa Spika, tunaelezwa kuwa Serikali itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji. Naipongeza sana Serikali kwa kulieleza hili na pia naomba Serikali katika uratibu wake huo ni vizuri kuvitaka vyombo vya habari na vya watu binafsi kuangalia ipasavyo baadhi ya vipindi vyao katika televisheni zao. Tunaangalia *TV* zao tukiwa pamoja na familia zetu wakiwemo wazazi na watoto wetu wa kuzaa na dada zetu.

Mheshimiwa Spika, pia ninaiomba Serikali kuharakisha ujenzi wa minara ya *TVT* ili wananchi wote wa Tanzania wafaidike na chombo chetu hicho cha Taifa. Vile vile maslahi ya Waandishi wa Habari wa *TVT* yaimarishwe kwa wote siyo kwa baadhi ya sehemu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Katibu Mkuu mama Rose Lugembe na watendaji wote kwa kuandaa hotuba nzuri ya Bajeti inayoeleweka. Hotuba hiyo pia ni majumuisho ya yote yaliyotekelezwa na Serikali ya CCM ya Awamu ya Tatu na matarajio yote yatakayoendelea kutekelezwa na Serikali ya CCM Awamu ya Nne.

Pamoja na kueleweka kwa hotuba hii naomba kuchangia mawazo katika maeneo kadhaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kudumisha amani na utulivu tulionao nchini. Suala hili limefafanuliwa vizuri kwenye hotuba, sasa ni wajibu wa viongozi wa vyama vyote vya siasa, mashabiki wa kisiasa na wananchi kwa ujumla kujihadhari na maneno na vitendo vitakavyoweza kusababisha uvunjifu wa amani kwa vile ni rahisi kuvunja amani kuliko kuijenga amani na mifano ya nchi jirani tunayo na madhara yake ni mengi.

Mheshimiwa Spika, huduma za jamii ni kweli kabisa Tanzania, tumepiga hatua kubwa katika uandikishaji wa wanafunzi kuanza darasa la kwanza toka 712,467 mwaka 1998 mpaka wanafunzi 1,376,467 mwaka 2005 kadhalika idadi ya Walimu imeongezeka. Hata hivyo, ieleweke kwamba idadi kubwa ya wanafunzi wenye ulemavu wa aina aina hawaandikishwi shule kutokana na ama wazazi kuwaficha, Walimu kukataa kuwaandikisha kutokana na kutokuwa na Walimu wa kuwahudumia wanafunzi wenye ulemavu. Kwa msingi huo, nashauri suala hili litazamwe kwa makini zaidi ili jamii hii ya wanafunzi waweze kupata haki yao ya msingi ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya, katika sekta hii pia kumekuwa na maendeleo ya utoaji na upanuzi wa huduma. Tatizo ni kwamba bado taratibu za kupata msamaha wa kupata huduma bure kwa wazee, walemavu, wagonjwa wasiojiweza, waathirika wa UKIMWI, wagonjwa wa kifua kikuu ni ndefu kiasi kwani zinazua kunyanyasika kwa wahusika badala ya kusaidiwa haraka. Hivyo, utaratibu wa utoaji misamaha uangaliwe upya kwani imekuwa ni usumbufu mkubwa kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wananchi kiuchumi, ingawa sera iko tayari juu ya suala hili, mikopo ya Kiserikali ya wanawake na vijana hutolewa kwa utaratibu uliopo sasa, lakini jamii ya watu wenye ulemavu bado wengi hawafaidiki na fursa hizi, kwanza kwa mfano mikopo niliyoitaja wengi wanaopewa ni wale waishio Mijini tu, mikopo hii haijawafikia wanajamii waishio Vijijini walemavu wakiwemo kwa hali hiyo kujikwamua katika dimbwi la umaskini ambalo walemavu wengi ndimo walimo inakuwa ni kama ndoto za alinacha.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iangalie upya taratibu za njia mbalimbali za uwezeshaji wananchi ili fursa hizo ziwafaidie walengwa walio wengi nchini wakiwemo walemavu.

Mheshimiwa Spika, suala la ulemavu linapaswa kuhusisha jamii nzima ya Watanzania na kwamba kila mpango na mkakati unapaswa kuzingatia mahitaji maalum ya jamii ya watu wenye ulemavu. Kwa msingi huo natoa rai kuwa masuala ya watu wenye ulemavu yawe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu au Ofisi ya Makamu wa Rais ili kila Wizara nyingine zishughulikie masuala yote ya walemavu yanayohusiana na Wizara husika kuliko ilivyo sasa kwamba kila kitu kiko chini ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ndani ya Idara ya Ustawi.

Mheshimiwa Spika, si rahisi Mheshimiwa Waziri mmoja kutoa maelekezo kwa Waziri mwenzake hivyo ndiyo maana nimependekeza kuwa masuala ya walemavu yawe chini ya uratibu wa Wizara/Ofisi nilizozitaja awali kwa vile Ofisi hizo zinaweza kabisa kutoa maagizo na maelekezo kwa Wizara zingine. Mfano wa pendekezo hili upo Tanzania Zanzibar na imesaidia Wizara zingine kuweka masuala ya walemavu ndani ya mipango yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake yote. Pamoja na shukrani hizo, napenda kutoa hoja zifuatazo:-

Moja, kwa vile mvua za mwaka huu zimekuwa za kukatika katika sana na hivyo watu katika vijiji vingi wamepanda zaidi ya mara tatu, kati ya vijiji 45 vya Wilaya ya Karatu, vijiji vya Gongali, Bashay, Qurus, Endashangwet, Endamaghang, Dumbechand, Matala, Mbuga Nyekundu, Oldeani, Mangola Juu, Gyehurum Arusha, Gyehurum Lambo, Bassodawish, Endamarariek, Qaru, Endadash, Kansay, Ayalabe, Iloma, Kilimanjaro na Chemichem vimeathirika sana. Ikizingatiwa kuwa sasa ni mwaka wa tatu kwa vijiji hivyo kukosa mazao kutokana na hali mbaya ya mvua. Je, ofisi ya Waziri Mkuu inatoa tamko gani kuokoa maisha ya wananchi hao ambayo yako hatarini kwani hawana tena mifugo ya kuuza na wala hawana fedha kutokana na ukame wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, hata vijiji vilivyobaki hali ya chakula si nzuri na hivyo, si vizuri kuzungumzia upungufu bali ni hali ya njaa inayoikabili Wilaya ya Karatu.

Pili, tangu Ofisi ya Waziri Mkuu ilipotoa sera ya maafa, inaelekea hakuna kilichofanyika kwa maelezo kuwa hakuna miongozo ya kiutekelezaji iliyopelekwa kwa vyombo husika Wilayani kwa kuwa miongozo hiyo haikupelekwa na hakuna vikao vya kamati za maafaa vilivyofanyika Wilayani Karatu. Je, Serikali inatoa kauli gani ili kamati hizo zianze rasmi na kunusuru maisha ya wananchi wengi wanaoweza kuathirika.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu sekta mbalimbali. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kulikuwa na mgogoro kati ya *CDA* na Manispaa ya Dodoma na mgogoro huo umesababisha mambo mengi kukwama katika kuendeleza Mji wa Dodoma ambao ni Makao Mkuu ya Chama Tawala CCM, Serikali na Bunge. Serikali imechukua hatua gani kusahihisho/kumaliza migogoro hiyo ili Mji wa Dodoma uweze kuendelezwa hasa kuhusu mawasiliano ya barabara za lami, mitaro ya maji machafu; na

(iii) Ujenzi wa nyumba za kisasa, kuongeza shule za msingi/sekondari ili Wizara nyingi zihamie Dodoma Makao Makuu na kupanua hospitali ya Mkoa kuwa ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na yote aliyoyasema ni ya msingi na yakitekelezwa vyema yatatupeleka mbali kiuchumi na kijamii kwa ujumla. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nimepokea simu sasa hivi toka kwa wapiga kura wangu wakinieleza nitoe shilingi katika hotuba ya Bajeti ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kama katika hotuba yake ya bajeti Mheshimiwa Waziri hatatamka lolote juu ya kuanzishwa kwa Manispaa ya Mtwara, maana tuliahidiwa kabla ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa hajaondoka tutapata Manispaa. Hivyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu umkumbushe Waziri wa TAMISEMI kama amesahau akumbuke.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na pia utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi. Nawapongeza Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib. Pia Katibu Mkuu wa Ofisi hii ndugu Rose Lugembe .

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia suala la watoto na wanafunzi wanaofaulu lakini wazazi na walezi hawana uwezo. Pamoja na juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali bado kuna walezi au watoto ambao wanajile wenyewe hawawezi kumudu kulipa ada ndogo ilyowekwa kwani ada inaonekana ndogo, lakini shule zenye hosteli kwa watoto wanaotoka mbali hawawezi kuzimudu. Ni vizuri Serikali iangalie upya jinsi ya kusaidia watoto hawa na kuhakikisha kwamba wanapata elimu kama watoto wengine. Pia kumekuwa na usumbufu kutoka kwa walimu kuhusu michango mbalimbali ya shule nje ya ada.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni umuhimu wa Serikali kutoa chakula cha mchana kwa watoto wote wa shule za msingi hasa kwenye Wilaya zenye matatizo au maafa. Hivyo, nashauri Serikali itoe chakula cha mchana kwa watoto wote Wilaya ya Makete ili kuwawezesha watoto kuondokana na adha ya kuingia ajira ya watoto na pia kuinua hali ya lishe miongoni mwa watoto. Hivyo, Idara ya Maafa ilitazame upya suala hili ingawaje *WFP* watatoa chakuala lakini siyo kwa watoto wote.

Mheshimiwa Spika, huduma za kujitolea ni vizuri ziangaliwe ili Serikali iweze kuweka utaratibu kwa wataalamu wa nchini kuweza kuchukuliwa na Serikali na kuwekea mikataba ya kufanya kazi kwa kujitolea ili kuziba mapengo kwenye Wilaya zenye upungufu mkubwa wa watumishi. Hawa ni pamoja na watumishi wastaafu ambao watakuwa tayari kwenda kufanya kazi na kulipwa posho ya kiwango kitakachowekwa na Serikali ili kujikimu. Hivyo, Serikali iliangalie suala hili kwa undani na kuona jinsi inavyoweza kulitekeleza.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Isimani, napenda kutoa pole na rambirambi zangu kwa ndugu, familia na wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kuondokewa na kipenzi chao, Mheshimiwa Abu Kiwanga. Mungu aiweke roho ya marehemu Kiwanga mahali pema peponi, *amin.*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba tena ya wananchi wa Jimbo hilo hilo la Isimani, natoa pongezi nyingi sana kwa Chama cha Mapinduzi kwa kukamilisha mchakato wa kuwapata wagombea wa Kitaifa kwa ufanisi na demokrasia iliyotukuka. Nampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kupewa jukumu la kubeba bendera kubwa ya CCM kama mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nawapongeza tena Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kugombea Urais wa Zanzibar. Nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kuwa mgombea mwenza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Kama nilivyosema, uteuzi na uchaguzi wao umekwenda kidemokrasia, sote tunajua ndani ya Bunge, nje ya Bunge, tumesikia pongezi zikitolewa hata kwa wenzetu wapinzani, wote wamepongeza uteuzi huu na hii inadhihirisha kwamba Watanzania wote wamefurahia uteuzi huu. Tunachosubiri sasa ni kuhitimisha ratiba ya uchaguzi ili tukamilishe furaha yetu, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuomba kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika maeneo yafuatayo:- kwanza nitachangia eneo la uratibu wa shughuli za Serikali, eneo la UKIMWI, udhibiti wa madawa ya kulevya, ustawishaji wa makao makuu, eneo la maafa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, nianze na eneo la makao makuu ya Serikali kuhamia Dodoma. Hoja hii imejitokeza na Waheshimiwa watano wameizungumzia nao ni hawa wafuatao:- kwanza imeanza kwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Margareth Bwana na Mheshimiwa Ireneus Ngwatura. Kamati imependekeza kwamba Serikali iweke ratiba ya kuhamia Dodoma lakini pia Mheshimiwa George Lubeleje ameulizia juu ya mgawanyo wa madaraka, ana mashaka juu ya mwingiliano wa madaraka kati ya *CDA* na Manispaa.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi, naomba niseme kwamba sisi sote hasa wana CCM tunajua kwamba suala la kuhamia Dodoma ni suala la Chama chetu, tumeliamua na tumeendelea kulisisitiza kupitia ilani zetu za uchaguzi kuanzia mwaka 1995 naamini mpaka hii inayokuja japo hatujaitoa rasmi. Tangu imetangazwa mpaka sasa muda mwingi sana umetumiwa na Serikali katika kuandaa mazingira ili kweli Dodoma iwe mji mkuu wa nchi.

Niwakumbushe tu yako mengi sana yamefanywa katika kuandaa mji huu ambao sote tunaujua ulivyokuwa kabla ya tangazo la kuhamia hapa. Katika kipindi hiki ndani ya mji wa Dodoma tumejenga barabara kuu za kilometa 14 zenye lami, tumejenga bomba kuu la maji katikati ya Dodoma zaidi ya kilomita 30 kwa kutumia *CDA,* tumejenga mifereji ya maji ya mvua zaidi ya kilometa 30, tumejenga bomba kuu la maji taka zaidi ya kilometa 24, tumejenga mabwawa ya maji taka hekta 16ambayo hivi karibuni tumeyakabidhi *DUWASA,* tumejenga shule za msingi tano, tumejenga soko kuu kubwa kabisa hapa, tumejenga kituo cha afya lakini pia tumejenga nyumba za makazi 600 ukiacha hizi mpya ambazo zinajengwa na Wizara ya Ujenzi zikikamilika hizi zitakuwa zaidi ya 800. Hayo ni sehemu ya maandalizi makubwa ambayo tumekwishayafanya pamoja na ujenzi wa ofisi kadhaa za Serikali ikiwemo ofisi ya TAMISEMI ambayo sasa ni mali ya Serikali na imekabidhiwa TAMISEMI, lakini maandalizi ya miundombinu hayajakamilika. Tumekamilisha eneo la mawasiliano, maji tumekamilisha. Mimi naamini hatua kwa hatua kulingana na uwezo utakaokuwepo, zoezi hilo la kukamilisha uhamishaji wa makao makuu kuja hapa litatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, najua Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, kwa upande wa Bunge Serikali imejitahidi kujibana ili angalau kwa eneo hili la Bunge kukamilisha mahitaji yote yanayostahili kuhamisha Bunge kuwa hapa Dodoma hasa kwa kuzingatia kwamba kwa mwaka huu wa fedha Serikali imeamua kujenga jengo la kudumu la Bunge hapa Dodoma. Kwa kufanya hivyo inahitimisha nia ya Wabunge wenyewe kupitia Bunge hili kwamba sisi tumeamua makao makuu ya Bunge ni Dodoma. Eneo moja hili Serikali imeshakamilisha na mengine najua yatafuata kulingana na uwezo utakavyokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo napenda nilizungumzie ni la udhibiti wa dawa za kulevya. Hili limezungumziwa kwa Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya na Mheshimiwa Mwanamkuu Kombo Makame. Waheshimiwa Wabunge wametoa hoja kwamba elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi kuhusu madhara ya dawa za kulevya na pili wamesema Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya irekebishwe kwani ilivyo sasa hivi haitoshelezi kudhibiti na kuwabana wanaojishughulisha na madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya, inatekeleza mpango kabambe wa Kitaifa wa Udhibiti wa Dawa za Kulevya ambao unalenga maeneo yafuatayo. Moja, ni kudhibiti uingizaji na uuzaji wa dawa za kulevya.

Pili ni kuelimisha jamii kuhusu madhara ya dawa za kulevya na tatu ni kutoa tiba na ushauri nasaha kwa waathirika wa dawa za kulevya. Tume inaelimisha kupitia vyombo vya habari na inaendesha semina kwa vikundi vya kijamii wakiwemo wanafunzi,

wasanii na vijana na aidha Tume imeanza kutoa semina kwa viongozi wa kijamii wakiwemo Makatibu Tarafa, Madiwani na viongozi wengine wa Mikoani. Hadi sasa Tume imeshafanya semina kwa viongozi hao katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Lengo ni kutoa elimu ya aina hii kwenye Mikoa yenye tatizo la dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na elimu hii na semina mbalimbali na elimu ambayo imetolewa, lakini pia Tume kwa kushirikisha vyombo kadhaa vya Serikali imefanya kazi kubwa sana na imekuwa inachukua hatua mbalimbali za kudhibiti uingizaji na uzalishaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya.

Kwa mfano kati ya mwaka 1997/2004 jumla ya kilo 3,146 za dawa za kulevya za viwandani kama vile *Heroine, Cocaine* na kadhalika, zilikamatwa na watuhumiwa 2,810 walitiwa hatiani. Aidha, jumla ya kilo milioni 257,868 za bangi na kilo 22,869 za mirungi zilikamatwa na watuhumiwa 39,569 walitiwa hatiani. Vilevile, mwaka 2004 peke yake ekari 2,815 za mashamba ya bangi ziliteketezwa na nyingi zinatoka Mkoa wa Mara.

Lakini ukiangalia takwimu hizi, zinaonyesha kwamba wengi wametiwa hatiani lakini wengi kwa sababu ya sheria na udhaifu wa sheria wengi walipigwa faini na wako nje na ndiyo maana tumeamua kama Serikali kuipitia upya Sheria Na. 9 ya mwaka 1995 ili kupendekeza adhabu ya faini kwa wasafirishaji, wazalishaji, wasambazaji na wauzaji ifutwe na badala yake iwepo adhabu ya kifungo, faini iwe ni nyongeza kwenye kifungo kwa sababu hivi sasa vijana wengi wanaokamatwa tunajua wanatumwa.

Baadhi ya watu wamekuwa wakihoji kila mara kwamba mbona vigogo hawakamatwi? Vigogo wote hawawezi kukamatwa kwa sababu wafanyabiashara wakubwa na wanaoitwa vigogo wanawatumia vijana wadogo ambao wanawapa ujira mdogo. Wanapokamatwa hawa kwa sababu sheria inawataka faini, wanawahakikishia kwamba msipotutaja sisi tutawalipia faini kwa sababu wakienda pale Mahakamani wanapigwa faini na mara moja wanalipiwa hizo fedha na wale waliowatuma.

Kwa hiyo, kwa sheria iliyopo hawafungiki. Si vigogo wala hawa wadogo, hawawezi kufungika ndiyo maana tunafikiri kwamba tubadilishe sheria ili adhabu iwe ni kifungo, lakini faini iwe inaambatana na kifungo pengine hawa wanaotumwa wataogopa kufungwa. Hivi sasa hawaogopi faini kwa sababu wanahakikishiwa na wale wanaowatuma kwamba mkikamatwa sisi tutawalipia faini. Kwa hiyo, haya ni baadhi ya maandalizi ya sheria ambayo tunafikiri tutaileta hapa Bungeni kwa wakati muafaka ili pengine itusaidie katika kuimarisha vita hii na mapambano dhidi ya madawa ya kulevya.

La tatu, naomba niseme kidogo juu ya hoja iliyoulizwa na Mheshimiwa Lwakatare na Mheshimiwa Salama Islam na Mheshimiwa Zahor Juma, kuhusu Ofisi ya Bunge. Mheshimiwa Lwakatare anasema, muundo wa Utumishi wa Ofisi ya Bunge urekebishwe ili watumishi wapate maslahi bora zaidi na Mheshimiwa Salama Islam ameulizia habari ya Ofisi ya Waheshimiwa Wabunge na Kamati za Bunge zipewe nafasi ya kutembelea Mikoa, lakini mwisho amependekeza kwamba muda wa wiki mbili kwa Kamati za Bunge kujadili Bajeti ya Wizara hautoshi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria Na.14 ya mwaka 1997 ambayo ndiyo iliyounda Tume ya Huduma za Bunge, kifungu cha 7(2) kinaelezea namna ya kupanga maslahi ya Watumishi wa Bunge. Tume imeelekezwa kuzingatia kuwa yanakuwa hayapishani sana na yale ya watumishi wengine katika Utumishi wa Umma, haya ni maelekezo ya jumla, kwa hiyo, Tume wakati inaangalia mambo haya na imekuwa inaangalia kila mara. Kwa sababu wote hawa ni Watumishi wa Umma na wote wanalipwa kutokana na fedha za Walipakodi, kwa hiyo, Tume inaangalia kwamba mafao haya ya Watumishi wa Bunge hayapishani sana na mafao ya watumishi wengine wa Umma.

Ingawa ni ukweli uliowazi kwamba kwa kweli Tume inawaangalia sana na inawajali Watumishi wa Ofisi ya Bunge. Sisi tunao watumishi kwenye Halmashauri, tunao watumishi kwenye Serikali Kuu hata ukiwalinganisha kwa macho tu unaweza ukawaona watumishi wetu hapa Ofisi ya Bunge wanawekwa vizuri zaidi kuliko watumishi wengine tunaowajua. Kwa hiyo, hilo jambo linatekelezwa vizuri sana na Ofisi yetu kupitia Tume yetu.

Kuhusu Ofisi za Wabunge, Serikali imeshatoa maelekezo kwa uongozi wa Wilaya na Mikoa yote kuhusu taratibu za kuwapatia Waheshimiwa Wabunge Ofisi zenye hadhi. Tulishatoa maelekezo muda mrefu na bahati nzuri kwa kiwango kikubwa sasa inatekelezwa. Ofisi zote za Waheshimiwa Wabunge zinatakiwa ziwe kwenye Majengo ya Serikali.

Tumewaelekeza Viongozi wa Mikoa na Wilaya wahakikishe kwamba Waheshimiwa Wabunge wanapewa Ofisi katika majengo ya Serikali katika Majimbo yao Wilayani na Mikoani. Hili jambo limeanza kutekelezwa na Serikali inaweka samani katika Ofisi hizo kupitia bajeti zinazowekwa na Katibu Tawala wa Mikoa. Ingawa kuanzia bajeti ya mwaka 2006/2007 tumeshakubaliana ndani ya Serikali kwamba sasa bajeti ya kuweka samani katika Ofisi, bajeti zinazohusu Ofisi za Wabunge zitasimamiwa na Katibu wa Bunge ambaye atashirikiana na Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya.

Kwa hiyo, kwa mwaka huu wa fedha bado bajeti ya samani au huduma za Wabunge mtaendelea kuziona kwenye bajeti za Ma - *RAC* lakini tumependekeza na tumeamua kuanzia mwaka 2006/2007 kazi hii ihame kutoka Mikoani, bajeti hii na pesa hizi apewe Katibu wa Bunge ambaye atazisimamia kwa kushirikiana na Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa.

Kuhusu Kamati za Bunge kupewa nafasi ya kutembelea Mikoa, muda wa wiki mbili Kamati za Bunge kujadili Bajeti ya Wizara hautoshi, napenda kujibu kwamba, hivi sasa Kamati zinakwenda Mikoani lakini kwa kawaida kwa mujibu wa utaratibu wetu hapa, Kamati ya Bunge tunawaita watu ambao tunahitaji kuwaona. Sisi tunao uwezo kwa mamlaka tuliyopewa ya kumwita mtu yeyote hapa kwenye Kamati iwe Dodoma au Dar es Salaam kumhoji au kutafuta maelezo yoyote ambayo tunafikiri yanafaa kwa mujibu wa uendeshaji bora wa shughuli zetu. Lakini pale inapobidi kwamba lazima Kamati iende Mikoani, Mwenyekiti wa Kamati anawasiliana na Spika na utaratibu

unafanywa, wanakwenda. Juzi hapa kulikuwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama imekwenda Mtwara na Lindi, imeshakwenda Mara. Kwa hiyo, suala hili linatekelezwa ili mradi lazima kuwe na sababu, lakini pia mawasiliano na Mwenyekiti wa shughuli za Bunge ambaye ni Mheshimiwa Spika.

Pia, wiki mbili zinatosha sana. Kwa hivi sasa kwa uzoefu tuliofanya kwa mujibu wa utaratibu wa kanuni tangu tumeanza Bunge hili mwaka 2000, kwa kweli wiki hizi mbili ni nzuri sana. Utaratibu wa wiki mbili unatusaidia sana kumaliza kazi zetu na kwa uzoefu tulioupata, nafikiri wengi wetu tunakubali kwamba kama Kamati ikijipangia vizuri majukumu yake kwa utaratibu mzuri, wiki mbili hizi tunafikiri kwa uzoefu tulioupata unatosha sana kutekeleza wajibu wetu vizuri.

Hoja ya nne inahusu Tume ya Huduma za Bunge. Muundo wa Tume urekebishwe ili Vyama vyote viwe na Wajumbe kwenye Tume. Hili limesemwa na Mheshimiwa Lwakatare. Mimi najua Mheshimiwa Lwakatare bahati mbaya hayupo. Anajua kabisa kwamba kwa utaratibu tulionao hapa Bungeni, sisi hatuna Vyama hapa, tuna Kambi ya Upinzani na tungesema kwamba tunataka viwe Vyama, basi hata huyo Mjumbe mmoja wasingempata kwenye Tume. Sasa tumerahisisha tukaweka Kambi ili angalau kwa umoja, wao waweze hata kuunda hata hicho kinachoitwa Baraza la Mawaziri Kivuli. Kama ingekuwa ni Vyama, hapa wasingeweza kuunda hata Wizara 10. Isingewezekana na sijui wangeelewanaje mpaka kugawana hizi Wizara, vinginevyo, ingekuwa Mawaziri watatu katika Wizara moja, kila mmoja angechagua Wizara anayoitaka. Kwa hiyo, sisi tumeamua hapa kwa pamoja kwamba tuwarahisishie kazi waunde kama Kambi ya Upinzani ili waweze kufanya kazi zao vizuri na ndiyo maana tumewapa hiyo nafasi moja.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Mheshimiwa Lwakatare ni kwa sababu huyu Mbunge tuliyemchagua, Mheshimiwa Ngede, nahisi ana uwezo mkubwa zaidi kuliko vile walivyofikiria ndiyo maana hawampendi. *(Makofi)*

Mimi niko kwenye Tume kwa niaba ya Serikali, najua uwezo wa Mheshimiwa Ngede na ndiyo maana kila mara hata wao wakisema hoja zote hapana, kwa sababu yeye ana busara zaidi, amekuwa anasema ndiyo, na ndiyo uwezo alionao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nampongeza sana Mheshimiwa Ngede na ninataka na Watanzania wajue kwamba unawawakilisha wenzako Wapinzani vizuri kwenye Tume. *(Makofi)*

Naomba niingie katika hoja za Vita Dhidi ya UKIMWI. Hoja hii imezungumzwa na Mheshimiwa Fatma Mchumo, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Leonard Shayo, Mheshimiwa Mng'ong'o, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo na Mheshimiwa Derefa. Wamezungumzia habari ya dawa za kurefusha maisha ARVs, wamezungumzia Asasi zisizo za Kiserikali zinazoshughulikia masuala ya UKIMWI kwamba hazifikishi huduma zao kwa walengwa kikamilifu na elimu ya UKIMWI wameshauri ifikishwe Vijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba kama tulivyosema kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mpango wa huduma ya matibabu unalenga kufikisha huduma ya upatikanaji wa dawa za kurefusha maisha nchi nzima kulingana na uwezo wa kitaalam na miundombinu inayohitajika katika kutoa dawa hizo. Utoaji wa dawa hizo, unaambatana na elimu kwa wagonjwa na wananchi kwa ujumla kuhusu matumizi bora ya dawa hizo.

Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya leo akijibu swali kwamba Serikali imeamua kutoa hizi dawa za kurefusha maisha bure, lakini kutokana na gharama kubwa, tunakwenda kwa awamu. Mpaka hivi sasa tumeweza kufikia wagonjwa 10,000 hivi sasa wanaweza kupata hizo dawa na wote tunajua kwamba bajeti ya mwaka 2003/2004 Serikali ilitenga Shilingi bilioni mbili na bajeti ya mwaka 2004/2005 Serikali ilitenga Shilingi bilioni 3.5 na wenzetu wa Canada wametusaidia Shilingi bilioni 3.5 na mwaka huu bajeti ya mwaka 2005/2006 Serikali imetenga Shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kununua hizo dawa.

Kwa hiyo, Serikali inayo nia njema ya kuhakikisha kwamba jambo hili linatekelezwa. Mheshimiwa Waziri wa Afya atalifafanua zaidi eneo hili la madawa maana wao ndiyo wanaolisimamia zaidi.

Tume ya Kudhibiti UKIMWI imeteua Mawakala watakaosaidiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kushirikiana na Sekta mbalimbali na Asasi zisizo za Kiserikali katika kuimarisha mwitikio wa wananchi dhidi ya UKIMWI, hii ni pamoja na kutoa na kuratibu raslimali ili kuhakikisha zinawafikia walengwa.

Ni kweli tumejitahidi sana kutumia mbinu mbalimbali, tumekuwa tunapeleka pesa kwenye Halmashauri, tunapeleka Mikoani, lakini baadaye tumejua pengine tunahitaji kuwa na watu wa kuratibu na kusimamia kwa ukaribu hizi fedha. Kwa hiyo, ndiyo maana uamuzi wa Serikali tumeufanya wa kuteua mawakala ambao watakuwa wanasimamia baadhi ya Mikoa na kuratibu shughuli ambazo zinahusiana na masuala haya ya UKIMWI.

Hawa wataratibu kupitia Halmashauri za Wilaya kwa sababu kwa mujibu wa Sera yetu *NGOs* na Taasisi zote zinazojihusisha na mambo ya UKIMWI zitasimamiwa na Halmashauri za Wilaya, lakini uwezo wa kifedha sasa tunaupeleka kwa hawa Mawakala ambao ndiyo watakuwa wanasimamia na ugawaji wa nyenzo na fedha kwa *NGOs* katika kila Halmashauri na Mikoa waliyopangiwa.

Mheshimiwa Spika, nimepokea ushauri hapa wa Mheshimiwa Makwetta nafikiri alimsikiliza vizuri Mheshimiwa Aziza alipokuwa anazungumzia dawa za kurefusha maisha ingawa hakuweka sahihi, lakini najua huu ni mwandiko wa Mheshimwa Makwetta. Nakubali ushauri wake, nataka niusome, amenisaidia kumpa majibu Mheshimiwa Aziza kwamba Wizara ya Afya imeagiza dawa za kurefusha maisha kwa watoto wadogo. *(Makofi)*

Dawa za kurefusha maisha kwa watoto zinatengenezwa kwa mchanganyiko tofauti na za watu wazima. Ni kweli na Waziri wa Afya amesema, hili ndiyo jibu na ni sahihi na hata utaratibu wa utoaji wa dawa hizi kwa watoto unatofautiana na ule utoaji wa dawa za watu wazima. Hili jibu nimelipata kwa msaada wa Mheshimiwa Makwetta ameniandikia hapa. *(Makofi)*

Nataka nizungumzie Hali ya Chakula. Hali ya Chakula imezungumzwa na Mheshimiwa Mgombelo, Mheshimiwa Dr. Slaa, Mheshimiwa Uledi, Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Ole Timan. Kwa ufupi wamezungumzia wasiwasi wa hali mbaya ya chakula unaojitokeza hivi sasa.

Nataka niseme kwa ufupi kwamba, Serikali inatambua kwamba kulikuwa na wasiwasi huo na ndiyo maana tulifanya tathmini ya awali ambayo ilitupa matokeo mwezi wa nne na kutokana na tathmini ile ya awali ilituonyesha kwamba maeneo fulani ya Mkoa wa Shinyanga, Ngorongoro na Monduli yana upungufu wa chakula na Serikali ilichukua hatua ikapeleka tani 1,913 katika maeneo hayo. Tani 1000 tullizipeleka Mkoa wa Shinyanga na ambazo ziligawanywa kama ifuatavyo:-

Wilaya ya Maswa ilipata tani 360, Bariadi walipata tani 340, Meatu walipata tani 240 na Kishapu walipata tani 60.

Mheshimiwa Spika, tulipeleka fedha kiasi cha Sh. 25,108,400/= kwa ajili ya kusambazia hiki chakula. Kwa hiyo, tulishaanza kuchukua hatua na pia tulipeleka Monduli tani 200 na Shilingi milioni 12 za kusambazia na pia tumepeleka Ngorongoro tani 300 lakini wenzetu wa *OXFARM* ndiyo walitusaidia kusambaza chakula hili. Kwa hiyo, kwa Awamu ya Kwanza ndiyo tumeshachukua hatua. Hivi sasa tumeelekeza tena nguvu zetu katika kufanya tathmini kubwa zaidi.

Nataka kuwahakikishieni kwamba Serikali itachukua hatua kwa mujibu wa matokeo ya tathmini itakayofanywa. Haya nimesema kwa jumla kwa majibu ya wote waliouliza na kutoa mashaka juu ya hali hii ya chakula.

Naomba nisemee kidogo juu ya masuala ya maafa. Hili jambo limezungumzwa na Mheshimiwa Salama Islam, kwamba Serikali ichunguze chanzo cha matukio ya moto kwenye majengo. Aidha, kiwepo kitengo maalum cha uokoaji katika Idara ya Maafa.

Mheshimiwa Spika, kila wakati matukio ya moto yalipotokea Serikali imechungunza vyanzo vya moto na kuchukua hatua zinazostahili. Aidha, Serikali imeagiza majengo yote ya umma na binafsi yaweke vifaa na vyombo vya kubaini na kuzuia au kuzima moto na hili ni agizo, ni lazima litekelezwe. Sera ya maafa imeelekeza kwamba kila anayehusika achukue tahadhari na kuwa na vifaa vya kutambua na kuzima moto.

Ofisi ya Waziri Mkuu ina mpango wa kuanzisha *Emergency Operation Centre.* Hii ni Ofisi ambayo itasaidia kuratibu majanga mbalimbali yanapotokea ili kuweza kupashana habari ndani ya Serikali na ndani ya Umma. Aidha, Serikali inaelekeza Sekta

binafsi nayo ichukue tahadhari ya kuweka vifaa na vyombo vya kubaini na kuzuia au kuzima moto kwenye majengo yao. Kwa hili kwa kweli naomba kwa dhati niipongeze Ofisi ya Bunge. Ofisi ya Bunge imetekeleza vizuri agizo hili la Serikali, kila mahali katika majengo ya Ofisi ya Bunge hapa tunavyo vyombo tayari maalum vimewekwa ambavyo vinatoa taarifa kama kuna uwezekano wa tukio lolote la moto na inatusaidia kujiandaa, kwa sababu vile ving'ora vikipiga, kwa vyovyote vile hakuna Mbunge au mfanyakazi atakayebaki hapa.

Kwa hiyo, itatupa nafasi kuanza kutafuta hata Zimamoto na kuwaarifu wenzetu ili waweze kutusaidia. Lakini pia tunaamini kwa tahadhari kama hizo, maisha ya watu hayatapotea kwa sababu kila mmoja atapata kusikia huo mlio wa tahadhari. Kwa hiyo, naomba Ofisi nyingine zote za Serikali ziige mfano wa Ofisi ya Bunge ambayo wao wameshatekeleza kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wote walioipongeza taarifa ya mafanikio ya Awamu ya Tatu ambayo imesomwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa wale Wajumbe wa Mkutano Mkuu ambao ni wa Chama cha Mapinduzi, taarifa ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu ya miaka 10 na taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya miaka mitano zilitolewa taarifa hizi tumezisambaza mpaka kwenye ngazi zote za Halmashauri ambako Dr. Slaa ni Mjumbe. Taarifa hizi zinafafanua kwa kina juu ya mafanikio na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Nataka kuwaomba Wabunge wote wenzangu hasa wa Chama cha Mapinduzi hii ndiyo silaha ya ushindi kwa sababu yote yaliyoahidiwa yametekelezwa vizuri sana na yameripotiwa katika taarifa hizi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu mmemshukuru sana na mimi namshukuru sana kwamba amejitahidi kutoa muhtasari wa mafanikio ya miaka 10 ya utekelezaji wa Shughuli za Serikali. Serikali itaendelea kutoa taarifa hizo. Hatuishii hapa tu, tumekubaliana ndani ya Serikali kwamba kila Waziri sasa baada ya Waziri Mkuu kutoa taarifa ya jumla ya Serikali. Kila Waziri atakapokuwa anasoma taarifa yake hapa, kwanza taarifa ya mafanikio itakuwa ndani ya kitabu ili iwe kumbukumbu katika *Hansard.*

Lakini baada ya kusoma na kuweka Mezani, kesho yake kila Waziri atatangaza Taarifa ya Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu ya miaka 10 katika magazeti ili na wananchi nao waweze kusoma.

Kwa hiyo, nawaomba wananchi wote wa Tanzania kuanzia sasa watapata taarifa na wataendelea kupata taarifa za kila Wizara kupitia Vyombo vya Habari hasa Magazeti. Tunataka wananchi lazima wajue jinsi Serikali yao ilivyotekeleza kwa ufanisi mkubwa sana kazi mbalimbali ambazo walikuwa wamewatuma kwa miaka hii 10.

Baada ya hapo, tukishamaliza Bunge wataingia wenzetu wa Mikoani kuanzia mwezi wa Nane, Mikoa nayo, wataendelea kutangaza mafanikio waliyoyapata katika Mikoa yao, Mkoa hadi Mkoa. Mikoa yote 21 wataendelea kutangaza mafanikio haya ya Serikali ya Awamu ya Tatu.

Kwa kweli nia ya Serikali ni kuwafanya wananchi waelewe na sisi kama Waheshimiwa Wabunge tutajitahidi wakati ukifika kufafanua zaidi yale ambayo yameelezwa kutokana na taarifa hizi. Taarifa hizi zinaweza kuwa ni fupi sana, sio rahisi kuandika yote, lakini sisi tutajitahidi sana. Nafikiri wakati wa kampeni kufafanua haya mazuri yote ambayo yamefanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu na pengine kutokana na mafanikio haya makubwa, tunaamini kwamba inaweza kutuwezesha Bunge lijalo tukawa na Viti vingi zaidi humu Bungeni kutokana na mafanikio tuliyoyapata katika vipindi hivi viwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimalizie kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa usimamizi thabiti katika utekelezaji wa Ilani zote mbili za Uchaguzi wa mwaka 1995 na mwaka 2000. Haya mafanikio yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wote mmeyapongeza humu ndani na ambayo yameendelea kupongezwa sana na raia wema wa nchi hii, yasingeweza kufikiwa bila usimamizi ulio imara wa Mheshimiwa Mkapa. Kwa hiyo, namalizia kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mkapa kwa usimamizi wake mzuri wa utekelezaji wake wa Ilani kwa kipindi hiki cha miaka 10.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi huo mdogo na mchango wangu, naomba na mimi kama walivyosema wenzangu, niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mia kwa mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hoja ya Waziri Mkuu na kabla sijasahau naomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Pia, naomba nitoe rambirambi zangu kwa wafiwa wote kwa vifo ambavyo vimetokea katika kipindi hiki cha Bunge.

Lakini pia ningependa niwashukuru sana Wapigakura wa Jimbo langu la Uzini kwa maelewano yetu, kwa mapenzi yetu, kwa ushirikiano wetu kwa muda wote wa miaka mitano. Ninaamini wale ambao wanaishi Jimbo la Uzini wanajua kwamba kipindi hiki tumefanya maendeleo makubwa sana katika Sekta ya Elimu, Afya, Maji, Barabara, Umeme na kadhalika.

Kwa hiyo, wakati ukifika nitakuja kwenu Waheshimiwa wa Jimbo la Uzini kuomba utumishi na ridhaa yenu kwa heshima, taadhima na adabu sana na ninaamini hamtaniangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningependa nitoe shukrani pia na pongezi kwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa ushindi mkubwa alioupata ndani ya Chama chake na pia ninaamini kabisa kwamba utatuletea ushindi wa kishindo katika kipindi kijacho cha uchaguzi.

Pia, nimpongeze sana Mheshimiwa Dr. Shein kwa kuteuliwa kuwa Mgombea mwenza na pia nimpongeze sana Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa. Naamini timu imetimia sana, vijana watatu hawa wazito kwelikweli, tutawafunga magoli mengi tu Wapinzani.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nimshukuru Bosi wangu , Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kufanya kazi naye katika kipindi kirefu. Mimi nafikiri ni Waziri pekee katika Wizara ya Nchi, nimefanya kazi naye muda mrefu zaidi kuliko wengine kwa sababu mara ya kwanza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, nikaenda Habari, nikaenda kwenye Kitimoto cha Mambo ya Ndani, nikarejea hapa hapa. Kwa hiyo, nafikiri nimefanya naye kazi sana.

Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kunifunza kazi, lakini namwomba anisamehe kwa mapungufu endapo nimemkera wakati wa utendaji kazi na ninamtakia kheri na baraka huko anakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo yangu yatakuwa mawili au matatu. La kwanza ni eneo la Habari ambalo waliochangia walikuwa ni Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Zahor Juma, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Anatori Choya, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Ester Nyawazwa, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo na Mheshimiwa Nyimbo.

La kwanza, wamezungumzia juu ya umuhimu wa maadili ya Waandishi wa Habari. Serikali inaahidi mbele yenu Waheshimiwa Wabunge kwamba itachukua hatua kali dhidi ya wale waandishi ambao hawafuati maadili ya Uandishi wa Habari. Lakini pia tutashirikiana nao Waandishi wa Habari na wamiliki wa vyombo katika kuwapa elimu na mafunzo Waandishi wa Habari ili wawe waandishi bora katika kipindi kijacho.

Pia, nafikiri kwa upande mwingine kwa wingi wa Vyombo vya Habari nchini mwetu, sisi tuna bahati hakuna msuguano mkubwa sana kati yao na Serikali, Chama Tawala na Vyombo vya Habari kwa sababu tuna majarida ya magazeti zaidi ya 489.

Tuna magazeti ya kila siku nchi nzima 42, tuna Vituo vya *TV* vikubwa, tuna Redio 32 nchi nzima, kuna *Cable TV* 63 na kuna Vituo vya Halmashauri 18.

Kwa hiyo, hivi ni vyombo vingi sana, lakini kwa sababu naamini kwamba Waandishi wa Habari na wamiliki wa Vyombo vya Habari ni wazalendo, watu ambao wameweka maslahi ya nchi mbele, nafikiri tumejitahidi sana kutokwaruzana hapa na pale na ningeomba kwamba watusaidie katika kuweka utawala bora na demokrasia.

Lakini wakumbuke kwamba wana wajibu mkubwa kuweka maslahi ya Taifa mbele. Ninaomba sana kipindi hiki cha uchaguzi watusaidie sana katika kuhimiza umoja na amani ndani ya nchi yetu kama wamiliki wa Vyombo vya Habari. Naamini kwamba kwa sababu wao ni wazalendo, wataweka mbele maslahi ya Taifa.

Lingine limeulizwa kuhusu taarifa ya Habari. Kwa nini inakuwa wakati mmoja katika baadhi ya Vyombo vya Habari? Tumeona kwamba sasa hivi kila mmoja ana uhuru wa kuweka vipindi vyake kwa mujibu wa anavyopenda mwenyewe, lakini pia Serikali ina mamlaka endapo ikiona kwamba taarifa ya habari ya vipindi fulani inaathiri umoja, amani na maslahi ya Taifa, basi Waziri mhusika anaweza akazuia akaweka wakati mwingine.

La msingi kuhusu habari, nafikiri kila chombo cha habari kijaribu kutoa habari ambazo anafikiri zinaweza kuvutia watu zaidi. Hiyo ndiyo misingi. Kwa hiyo, nafikiri ni ushindani huu tunataka pia wajitahidi kuweka mbele maslahi ya Taifa, lakini pia Vyombo vya Habari pamoja na Serikali vijaribu kuweka taarifa za habari zao zivutie zaidi ili ziweze kuvutia watu wasikilize.

Mheshimiwa Spika, lingine lililozungumziwa ni kwamba baadhi ya wakati *TV* inakatikakatika. Tumeambiwa kwamba kuna chombo kinachoitwa *Centre Contral* kiliharibika, Serikali imekwishakitengeneza.

Pia, tumeulizwa kwamba lini Serikali itajitahidi kuifanya TVT kuonekana nchi nzima? Tumejitahidi, sasa hivi tumejenga *Satelite* na sehemu kubwa ya nchi yetu inaonekana kwa kutumia nyungo. Lakini sasa hivi katika mwaka huu wa fedha tuna Vituo vya *Television* na vingi sana vitajengwa katika Mikoa yetu ikiwemo Mbeya, Tabora, Lindi, Mtwara, Tanga, Kagera, Kigoma na Mara. Nilifikiri Wabunge wa maeneo hayo watashangilia lakini hawashangili? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwamba kabla ya Oktoba mwaka huu 2005, basi maeneo yote haya tutaweza kuona Televisheni ya Taifa katika nchini yetu na kwenye Bajeti ijayo tutaweza kuongeza Mikoa mengine iliyobakia. Lakini nia yetu ni kwamba nchi zima ionekane kwa sababu ndiyo wajibu wa kwanza wa Serikali, kutoa habari kwa kila mtu.

Mheshimiwa Spika, lingine lililozungumzwa ni kuhusu maslahi ya wafanyakazi wa *TVT* na Redio. Tumesema kwamba tumejitahidi kufanya hivyo na maslahi sasa hivi yanaboreshwa. lingine, limeulizwa kuhusu uchunguzi wa miradi ya *TVT* hasa kuhusu malalamiko kwamba kuna ubadhirifu wa fedha katika ujenzi wa Kituo hiki. Nafikiri unajua kwamba katika Bunge hili tumepatiwa taarifa kwamba *PCB* na vyombo vingine vinafanya uchunguzi na kuna baadhi ya watu wameshahojiwa, tusubiri wakati ukifika mtapata taarifa hii ukizingatia Serikali hii ni ya uwazi na ukweli na haifichi jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine lililozungumzwa na Mheshimiwa Zubeir, ni kuhusu umuhimu wa Kiswahili. Nafikiri kuna haja ya Serikali kuwa na Sera maalum hasa ya Lugha ya Kiswahili. Mimi namuafiki sana kama mdau mkuu wa lugha hii, kwamba hasa kwa Tanzania. Sababu Kiswahili Tanzania ni nyumbani na sasa hivi Kiswahili kinazungumzwa na watu zaidi ya milioni 100 duniani kote na nchi nane za Afrika zinazungumza Kiswahili, ikiwemo Burundi, Kongo, Kenya, Visiwa vya Ngazija, Rwanda, Somalia, Tanzania na Uganda, lakini si hawa tu, kuna nchi za jirani pia kama

Malawi, Msumbiji na Zambia pia Kiswahili kinazungumzwa, lakini hata nchi za Uarabuni, Oman, Yemen na kadhalika.

Kwa hiyo, ni lugha ambayo ni muhimu sana na sisi Watanzania kama ndiyo Waasisi na wenyewe, basi kuna haja ya kuipa kipaumbele ili tuweze kufanikiwa jambo hili. Tuna taarifa kwamba hata wasomi maarufu duniani, hasa waandishi wa vitabu na mashairi, wakina Wole Soyinka na Ayi Kwei Armah walipendekeza zamani sana kwamba Kiswahili kinafaa kitumike katika nchi za Afrika na matokeo yake hivi karibuni tumepata bahati kwamba Kiswahili kimetumika katika Bunge la Afrika na pia katika Umoja wa Afrika. Mimi nafikiri sasa kuna haja ya nchi yetu pia tuonyeshe mfano wa kusaidia lugha hii.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi sana zinataka kutumia Kiswahili sana, lakini nazo pia hazina Sera. Lazima kuwe na Sera ambayo itaipa nafasi dhima ya Kiswahili ipewe hadhi yake na kujaribu kutoa kasumba iliyobaki katika mawazo yetu kwamba lugha ya Kiafrika haifai kufundishia na haifai kwa mambo mengine. Lakini wakati wa kuomba kura Kiswahili kinafaa, wakati wa kuhubiri Kiswahili kinafaa, lakini maslahi yake hakipati. Kwa hiyo, ningeomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane katika kukipa hadhi Kiswahili kipate hadhi yake. *(Kicheko/Mkofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna mahitaji makubwa ya Kiswahili Afrika na duniani. Tunatakiwa tupeleke Walimu wengi sana katika nchi ya Namibia, Libya, Burundi, Rwanda na Uganda, lakini Walimu wenyewe hawapo au hawana habari kabisa. Kwa hiyo, hii ni ajira kubwa sana, mimi nafikiri tutumie nafasi hii ili tuweze kwenda katika nchi hizo kupata ajira kama wengine wanavyoita lugha zao kama ni ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, eneo la siasa waliochangia ni Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Yahaya Kassim, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mheshimiwa Hilda Ngoye, Mheshimiwa Frank Maghoba na Mheshimiwa Danhi Makanga.

Mheshimiwa Spika, kuna swali kwamba,kuna watu ambao hawakupata nafasi kuhakiki majina yao wakati wa kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la Wapiga, lakini muda ulitolewa wa kutosha na ni muhimu kwenda. Kwa hiyo, je wale ambao hawakuhakiki watapiga kura? Nasema, Watapiga kura kama masahihisho hayakuwa makubwa, kama jina si lako kabisa na umri sio hawawezi kupiga kura hata kidogo. Kwa hiyo, nasema tutafanya makosa kwa wale ambao hawakuhakiki, lakini tutajitahidi, wale ambao wana makosa si makubwa watapiga kura kwa sababu ni haki yao.

Lingine limeulizwa kuhusu Wapigakura wale wa Zanzibar ambao idadi yao ni 15,977 ambao waliandikishwa na Tume yetu ya *NEC*. Hawa waliandikishwa tarehe 27 mpaka tarehe 10 mwezi Mei na walikuwa Unguja 14,216 na Pemba 1,761. Hawa hawakujiandikisha Zanzibar kwa sababu walikuwa hawana sifa ya kupiga kura kwa ajili ya chaguzi za Zanzibar, kumchagua Rais wa Zanzibar, Mbunge wa Zanzibar, Mwakilishi na Diwani wa Zanzibar. Hawa kwa lugha nyingine wanaitwa si "Wazanzibar", ni "Wazanzibara" kwa lugha ya Mitaani huko. Lakini mimi siiafiki lugha hiyo.

Wangesema hawa sio, hawana haki ya kupiga kura Zanzibar, lakini wana haki ya kupiga kura katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hawa watu ni wengi sana. Kama utaamua uwapeleke kwenye Jimbo langu la Uzini, basi sina shida, nitapita moja kwa moja. Kwa hiyo, ni muhimu kuhakikisha kwamba hawa kama hawana haki pale wasipige kura kwa sababu hawakai pale.

Mheshimiwa Spika, kwa Zanzibar mtu anashinda kwa kura 3,000 au 4,000 ama 7,000; ukimpa hizi 15,000 yuko mbali sana. Kwa hiyo, tumeamua kwamba hatuwezi kupandikiza watu ambao hawana haki ya kupiga kura Zanzibar. Hayo ndiyo madhumuni yake.

Mheshimiwa Spika, lingine Mheshimiwa Muttamwega ameuliza kwamba: Je, wagombea binafsi wanaruhusiwa? Tunasema hawaruhusiwi. Halafu tumeulizwa kwamba: Je, kutakuwa na ulinzi wa kutosha? Kutakuwepo ulinzi wa kutosha, kutakuwa na amani na utulivvu na tunatoa wito kwa wananchi wasiogope waende kupiga kura siku hiyo bila wasiwasi wowote. Pia, tumeulizwa: Je, kutakuwa na Vituo vya Uchaguzi vitakavyoongezwa? Vitawekwa kwa mujibu wa idadi ya watu na kila mmoja atapiga kura kwa wakati wake. Halafu pia tumeambiwa kwamba tuchukue hatua kali kwa matumizi mabaya ya ruzuku. Tumelisikia na tutachukua hatua kali kabisa.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa kwamba Vyama vya Siasa ambavyo havifuati Sheria na taratibu vifutwe. Vipo vilivyofutwa na vingine vitafutwa. Lingine limeulizwa na ndugu yangu, rafiki yangu Yahaya Kassim anashauri kwamba Mwezi wa Ramadhan Waislam wasipige kura kwa sababu wanafunga. Mimi nafikiri Sheria zetu na Katiba yetu inasema kwamba siku ya Jumapili ya mwisho wa mwezi wa Oktoba ni siku ya kupiga kura. Kwa hiyo, haya ni matakwa ya Katiba.

Lakini sio vizuri sana pia kuchanganya mambo ya dini na mambo ya Serikali kwa sababu wengine wangesema sisi Jumamosi hatupigi kura Wasabato, mwinge Jumapili nakwenda Kanisani, kwa hiyo, itakuwa balaa kubwa sana. Tungeomba kwamba ndugu zetu Waislam waende kupiga kura kwa sababu kupiga kura hufanyi dhambi wala saumu haifunguki bali unakuwa imara zaidi. Nimeuliza Masheikh wamesema kwamba, wakati wa vita vya Waisilamu vya Badri, Mtume Muhammad aliwaambia Waislam: "Fungeni mkapigane vita."

**MBUNGE FULANI:** Ni kweli!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Kweli! Kwa hiyo, vita na saumu ipi ngumu zaidi? Kwa hiyo, mimi nafikiri haina haja. Tufunge saumu tuswali, tujifanye kama sisi ni wapiganaji wa vita vya Badri, tunafunga na tunapiga kura ili CCM ishinde siku hiyo. Kwa hiyo, naomba Waislam kumbukeni mawazo ya Mtume Muhammad juu ya vita vya Badri, fungeni, salini na mkapige kura ili CCM ishinde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine la Mheshimiwa Lwakatare, naona hayupo hapa, nimepitia hotuba yake ile, anasema jambo usilolijua ni usiku wa giza. Sasa nimechukua

hii ndiyo *heading* yangu ya makala yangu kwamba: "Usilolijua ni usiku wa kiza." Ni dhahiri kwamba hotuba ile hakuandika yeye, imeandikwa Mtendeni Unguja na ushahidi ninao, kaletewa kwa *Fax* usiku hapa, kaja kaisoma. Kwa hiyo, huyu katumwa tu. *(Makofi)*

Zamani kulikuwa na santuri ile ya *gramophone*, hizi *Master's voice,* huu ni mwangwi tu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lwakatare achana nao, toka huko, si Chama chako hicho, wanakutumia tu wao. Yuko wapi Mapalala? Mapalala alikuwa Chama hicho hicho, yuko wapi? Hayupo leo, kafukuzwa. Yuko wapi Ramadhan Mzee? Hayupo, kafukuzwa! Yuko wapi Maghoba na wengi tu hawarudi hapa. Nimesikia mimi!! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pia ametuambia kwamba Chama chetu hakiwajazi mapesa watu mfukoni, sio Sera yake. CCM haijazi mapesa mfukoni kwa sababu ni unafiki, ni uongo haiwezekani, dunia gani itawajaza fedha mfukoni watu? Ametuambia Makanga juzi kwamba huyo mwenye Sera hiyo naye pia anadaiwa na nyumba imeuzwa. Sasa wasiwadanganye wananchi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwenye ukurasa wa sita, amesema kwamba CCM inafaa isifiwe, lakini imefanya mambo machache ya maendeleo. Mheshimiwa Lukuvi ametoa hapa vitabu viwili vinaeleza mafanikio yetu ya Chama cha Mapinduzi. Yako mengi sana, si machache. Lakini ni bahati mbaya wenzetu Wapinzani wana macho lakini hawaoni, wanamasikio lakini hawasikii.

**WABUNGE FULANI:** Hawasikii!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Nimepata aya moja kwenye Quran, tafsiri yake inasema hivi: "Wana macho lakini hawaoni, wanamasikio lakini hawasikii, wao ni kama wanyama bali wao wamepotea njia." Kwa hiyo, hiyo ndiyo hali ya wenzetu, hawayaoni haya yameandikwa. Katika hoja yake pia amejaribu kuleta kufuru hapa, kwa sababu Waislam wanatakiwa kabla ya kusoma Quran, watawadhe. Huyu bwana hakutawadha, sio safi kabisa, hana udhu! Halafu aya kaisema ndivyo sivyo, amekufuru, pia ana dhambi. *(Makofi)*

Sasa nimwambie namna ya kutamka, inatamkwa hivi: *"Inna lillah Waina illaih Rajiun"* kuna *aghain* hapa. Kwa hiyo, amekufuru huyu bwana. Bahati mbaya katika Uislam hakuna kuungama ya kitubio. Lakini ningemwomba aende akaungame kwenye kitubio ili asafike, la sivyo dhambi itamwandama. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, amezungumza pia kwamba, kwa mara ya kwanza Tanzania imetoa wakimbizi. Haijawahi hata siku moja, nchi yetu ni nchi ya amani utulivu, demokrasia na umoja, haikutokea na haitatokea. Wale walikuwa wahalifu wa Shimoni, kwa sababu walichinja Askari pale Wete. Walifanya maandamano haramu, walitaka kupora silaha katika Vituo vya Polisi. Kwa hiyo, walikuwa wahalifu wanakimbia kukamatwa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Watanzania wasijilinganishe wao hata kidogo na *ANC* au *SWAPO* au *ZANU.P.F,* hawalingani kabisa! Wao ni wahalifu, wenzao walipigania uhuru wale. Kwa hiyo, Chama hiki ni Chama cha Ugomvi, jina lake ni *CUF*; Chama cha Ugomvi na Fujo. *(Makofi, Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Chama chao pia kinawapa taabu sana, kwa sababu Waswahili wanasema kwamba jina zuri mpe mwanao. Sasa jina linawadhuru hawa, Chama cha Ugomvi na Fujo. Kwa hiyo, naomba wasiseme uongo kwamba wao wamekimbia kwa sababu ni wahalifu, Serikali imewasamehe, wao wanajua. Mimi nilikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, lakini wale ilikuwa tuwashitaki Mahakamani.

Lingine alichosema Mheshimiwa Lwakatare ni kwamba eti, akishinda, lakini Chama chake hakishindi, lakini anasema atashinda, nchi yake itakuwa ya haki na usawa huko Zanzibar. Lakini sisi Wazanzibar tunaowajua CUF, si kweli! Haki na usawa wa Zanziba umepatikana tarehe 12 Januari, 1964. Hapo ndipo haki na usawa wa kweli kweli ulipatikana, kwa sababu sasa hivi Zanzibar mtu hutawali kwa sababu baba yako alikuwa Mfalme au mama yako au dada au shangazi, siku hizi hamna hiyo. Unatawala kwa kura. Kwa sababu hii, haki imeletwa na *Afro- Shiraz Party. (Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Waambie!!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIBU):** Bila hivyo, tungekuwa mpaka leo tunatawaliwa na Mfalme tu Said Sayyid au Sayyid bin Abdalah, Said Khalifa. Kha! Kha! Sijui. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa nchi ya usawa, zamani kule Zanzibar kulikuwa kama *Pyramid* vile. Juu kabisa kule kuna Wazungu wachache tu, halafu wanafuatia Waarabu, wanafuatia Wahindi na huku chini ndiyo Waafrika tele huko, ni watwana huko, kuna wajakazi huko, makuli huko, wachukuzi huko chini huko. Sasa hivi *alhamdullillah* tuko sawa kabisa. Kwa hiyo, nasema haki ilifanyika mwaka 1964. Wazanzibar wanapata ardhi ya bure, wanapata elimu ya kisasa, afya, mashamba nakadhalika. Kwa hiyo, haki na usawa vimekwisha, hukuna lingine.
*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kwamba hawa wanasema haki na usawa katika Serikali. Ndani ya Chama chao haki hakuna. Nyinyi mnajua, wamewafukuza akina Mama Bozen na Ngede bure bure. Lakini Mahakama imesema hawa wana haki. Wamemfukuza Mapalala, Ramadhani Mzee hivi karibuni, wapo wengi watafukuzwa kati ya Waheshimiwa Wabunge hawa 17 maruhani wale, kiasi cha 10 hawarudi. Wameshinda kura za maoni, lakini wamewaengua kwa sababu wamewachukua marafiki zao na mashemeji zao. Hawa jamaa ni waonevu wakubwa sana! Waonevu kweli kweli! Tokeni huko *CUF*, njooni huku CCM.

Mnaona mfano kwa Lamwai! Yupo hapa! Alikuwa huko akakimbia, Makanga yupo! Tokeni huko si Chama hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni katika *speech* ya Mheshimiwa Lwakatare, namnukuu: "Kwa nini fedha hizo zisipelekwe kwa akina mama wanaougua saratani ya matiti wakati pale Rais wetu anachangisha fedha kwa ajili ya uchaguzi wa Mkoa wa Kirimanjaro?" Amesema hapa kwamba yeye anaona kwamba tumefanya makosa ya kumtaka Rais wetu ambaye ni Mwenyekiti wetu wa Chama, ana haki kabisa ya kuchangisha na fedha zile zingefaa zipelekwe kwa hawa watu wenye matatizo saratani ya matiti.

Mimi nafikiri si makosa na wao pia wafanye tu na nitawaelekeza wafanye nini. Ushauri wangu wa bure ni huu, wafanye hivi; Mwenyekiti wenu wa Taifa au Maalim Seif, nao hawakatazwi kuchangisha fedha na wakipata akachangie waathirika wa matende na mabusha. Wagonjwa wako wengi, wao wafanye kazi nyingine na sisi nyingine. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika nimalizie la mwisho kwamba, Lwakatare katuambia kwamba anashukuru sana ushirikiano wake na Wapinzani wenzake Bungeni hapa. Mimi nafikiri amewaburuza sana Wapinzani wenzake. *CUF* wamewaburuza sana wenzao ndani ya Bunge hapa kwa muda wa miaka mitano na juzi wametambua kwamba *alah*, kumbe tumeburuzwa! Matokeo yake ni yale ya kupiga kura ya kuwapinga wale wa *CUF* wenyewe kwamba Wapinzani wote wamekataa kuwaunga, wameunga mkono Bajeti ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Kwa hiyo, si kweli kwamba wameshirikiana, wametambua, mmewadanganya muda mrefu, wameamua sasa basi. Kwa hiyo, ningewaomba ndugu zangu wa Vyama vya Upinzani, *CUF* wanawatumieni nyinyi kujijenga wao, nyie hamjui. Sasa achaneni na hao, njooni katika Chama cha Mapinduzi. Ni kweli, "Jambo usilolijia ni kama usiku wa giza." *(Kicheko/Makofi)*

Mheashimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, naomba Watanzania wote kabisa kwamba Chama ambacho kinafaa kupigiwa kura ni Chama cha Mapinduzi, ni Chama chenye hazina ya Viongozi bora na wazuri kuliko Vyama vyote hapa nchini, Chama chenye Sera sahihi na nzuri kuliko zote nyingine nchini na ni Chama chenye kuheshimu Mapinduzi ya Zanzibar na Uhuru wa Tanganyika. Kwa hiyo, endapo Watanzania wanataka amani, utulivu, umoja na maendeleo, Chama cha Mapinduzi ndiyo Chama chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ratiba niliyoitangaza asubuhi inakwenda vizuri. Kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11:00 jioni tutakapomsikia mtoa hoja mwenyewe akihitimisha hoja yake. Ahsante.

*(Saa 06:49 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge Lilirudia)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi mchana huu ili niweze kuhitimisha hoja yangu ambayo niliitoa juzi siku ya Alhamisi. Kwa bahati mbaya sioni Wabunge wa upande wa Upinzani, lakini nafikiri haina tatizo tutaendelea na kumalizia hoja.

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao ambayo wameitoa katika hoja hii na nataka kuwaahidi kwamba Ofisi yangu pamoja na Serikali kwa ujumla tutazingatia sana yote ambayo mmetushauri. Yote ambayo mmechangia tutayaweka maanani katika kutekeleza bajeti hii na pia katika kutekeleza mipango mingine ya Serikali kwa sababu bajeti hii ilikuwa inazungumzia Serikali kwa ujumla. Yapo maeneo mengi sana ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumzia ambayo pia tutayafanyia kazi katika shughuli mbalimbali za Serikali.

Waheshimiwa Mawaziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mawaziri wa Nchi, wametoa ufafanuzi wa kutosha sana kwa maeneo karibu yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumzia. Kwa hiyo, kazi yangu itakuwa ni kujaziajazia pale ambapo labda nyama haikutosha au maeneo ambayo hawakugusia, lakini ni machache sana. Kwa hiyo, napenda niwashukuru sana Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakifanya ya kunisaidia katika kujibu hizi hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nishukuru Waheshimiwa Wabunge kwa sababu na wao pia wamenisaidia sana kujibu baadhi ya hoja hasa zile zilizotoka upande wa Upinzani hasa kwa Kiongozi wa Upinzani. Kwa kweli, amejibiwa na Waheshimiwa Wabunge na sio Wabunge wa Chama Tawala tu, hata Wabunge wa Upinzani pia wamemjibu. Kwa hiyo, nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamepata nafasi ya kuchangia katika hoja hii. Waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni ni arobaini na tatu. Ningependa niwataje, nao ni:-

Wa kwanza alikuwa ni Mheshimiwa Athumani Janguo -Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala akifuatiwa na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare - Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Thomas Nyimbo, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Salama Islam, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Kombo, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura na Mheshimiwa Dr. James Msekela. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Ali Karavina, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Mutamwega Mgaywa, Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Emmanuel Enock Kipole, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wale ambao hawakupata nafasi ya kusema lakini wameandika ni Waheshimiwa Wabunge thelathini na mbili na wao pia naomba niwataje. Nao ni Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Mussa Lupatu, Mheshimiwa Cythia Ngoye, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Khamis Awesu Abood, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Leonard Shango na Mheshimiwa Herbert Mntangi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Khadija Kusaga, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Kombo, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Abdillah Namkulala, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mheshimiwa Shaame Sijamin Mohammed, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Leonard Derefa na Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naamini nimewapata wote, lakini kama kuna ambaye labda jina lake limeachwa kwa bahati mbaya anaweza kunikumbusha.

Mheshimiwa Spika, katika kujibu hoja mbalimbali kama nilivyosema zipo ambazo zimeshajibiwa na zipo ambazo nitazijibu hapa na nyingine zitajibiwa na Mawaziri wa Sekta mbalimbali au wa Wizara mbalimbali kwa sababu kama nilivyosema hotuba yangu ilikuwa inahusu maeneo yote ya Serikali kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri Mkuu ndiye mratibu wa shughuli zote za Serikali. Kwa hiyo, majibu mengine yatatolewa na Wizara husika wakati wa bajeti zao au wakati mwingine wowote. Lakini Mawaziri wataelekezwa hasa yale maeneo ambayo yanahitaji majibu dhahiri waweze kuyajibu wakati wa bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nizungumzie maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza, Waheshimiwa Wabunge kadhaa wamezungumzia juu ya kuwa na uangalifu mkubwa katika kubinafsisha Mashirika ya huduma. Hili ni eneo ambalo wanayoyasema Waheshimiwa Wabunge ni ya kweli na kama mtakavyokumbuka, hata wakati tulipokuwa tunaelekea kwenye ubinafsishaji

tulisema ni eneo gumu na lazima Serikali ifanye ubinafsishaji katika eneo hili kwa uangalifu mkubwa.

Kama mtakumbuka, hata sasa katika Mashirika mengi ya aina hii tumekuwa tukitumia zaidi utaratibu wa ukodishaji badala ya ubinafsishaji moja kwa moja na hata wenyewe nao ni kwa uangalifu mkubwa. Kwa hiyo, nakubaliana na hoja ya Waheshimiwa Wabunge na nataka kuwaahidi kwamba Serikali imeliona hilo na hivi sasa Serikali imeunda timu ya wataalam wa kuangalia eneo hili kwamba twende nalo vizuri zaidi. Kwa hiyo ni eneo ambalo nakubaliana kabisa na ushauri waliotoa na tutaendelea kuzingatia na kama nilivyosema, tayari tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni bei kubwa ya mafuta. Ushauri ulitolewa kwamba kuwe na chombo cha kudhibiti bei kubwa ya mafuta. Nadhani tatizo katika eneo hili sio chombo, tatizo ni upandaji wa bei katika soko la dunia. Kama tunavyokumbuka si muda mrefu uliopita bei ya mafuta ilikuwa kwenye Dola 24 mpaka 26 kwa pipa katika Soko la Dunia, lakini ghafla katika kipindi cha muda mfupi bei hiyo ilipanda zaidi ya mara mbili na kufika kwenye Dola hamsini na wakati mwingine hamsini na zaidi. Sasa katika hali ile huwezi kudhibiti upandaji wa bei katika nchi ambayo huzalishi mafuta. Kwa hiyo, kazi kubwa kwa kweli tuliyonayo ni kuyatumia mafuta kwa uangalifu. Ni vyema shughuli hasa hizi za Umma zikatumia mafuta kwa uangalifu sana kwa sababu bei za mafuta bado zipo juu ingawa kuna matumaini kwamba labda zinaweza kupungua, lakini bado zipo juu na hatuna namna yoyote ya kuweza kushusha hizi bei.

Mheshimiwa Spika, kwa maana ya kudhibiti bei ndani ya nchi kama tunavyojua, tumefanya bei ya mafuta iwe ni huria na hii imesaidia sana Makampuni mbalimbali kushindana. Katika ule ushindani, kumekuwa na nafuu za kupata bei ndogo kwa sababu ukipandisha bei, wenzako wakiwa na bei ya chini, basi wewe hutopata biashara. Hili limesaidia lakini ni kwa kiwango kidogo sana katika soko la ndani. Kwa hiyo, tatizo letu kubwa ni bei ilivyo kubwa katika Soko la Dunia huko mafuta yanakochimbwa. Laiti tungepata mafuta yetu na ndio kazi kubwa ambayo Serikali itakuwa inaisimamia kuona kama tunaweza kupata mafuta ili tuweze kuondokana na tatizo hili katika muda mrefu. Kwa hiyo, hili ndio jibu la tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la tatu ambalo ningependa kulizungumzia ni la utawala bora na nitagusia vipengele viwili tu kwa sababu vingine vimekwishazungumzwa. Kipengele cha kwanza ni cha rushwa.

Nataka niseme kwamba tatizo la rushwa hakuna hata siku moja mtu alisema kwamba halipo, lakini tunachosema ni kwamba tumekuwa na mipango kadhaa ya kupambana na rushwa na kwa kweli mafanikio yapo ya kuridhisha sana, lakini bado mapambano haya yanatakiwa yaendelezwe kwa nguvu.

Napenda nishukuru sana wananchi wa nchi hii kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakiitika vita hivi dhidi ya rushwa. Kwa sehemu kubwa wananchi wameitika sana na ndiyo maana vita inaonyesha kuna mafanikio. Leo watu hawaogopi kusema habari ya rushwa na kama kuna Kiongozi au Mtendaji au nani anakula rushwa, watasema na bado

tumeendelea na utaratibu wa kuweza kuwatafuta kwa kupata maoni ya wananchi juu ya wala rushwa na kwa kweli haya yote yamesaidia na mimi nina hakika ndio maana hata katika tathmini za Kimataifa nchi yetu inaonekana ni mojawapo ambayo inapiga vita rushwa kwa dhati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata wawekezaji wetu nikizungumza nao ni tofauti sana na huko nyuma. Leo wanaridhika sana na hali ambayo wanakutana nayo wakati wanapotaka kuwekeza nchini. Mazingira na mawingu makubwa ya rushwa yameondoka. Kwa hiyo, mimi ninachotaka kuwaomba Watanzania ni kwamba tuendelee kupambana na rushwa, ni adui mbaya kwa ustawi wa jamii na ni adui mbaya kwa ustawi wa uchumi wetu. Kwa hiyo, tuendelee kupambana na rushwa na nina hakika tutafika pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili katika utawala bora ambalo ningependa nilizungumzie ni eneo ambalo Waheshimiwa Wabunge kadhaa wamelizungumzia la matumizi ya nguvu ya ziada na katika hili nina hakika wanamaanisha Polisi. Sasa ninaloweza kulisema ni kwamba, pale ambapo imebainika kwamba kwa kweli aliyehusika ametumia nguvu za ziada Viongozi wa juu yake wamemwadhibu au wamedhibiti jambo hilo. Pale ambapo itadhibitika hivyo lakini ni nani ambaye anasema haya, Viongozi wa Polisi wanajua pale ambapo nguvu kubwa imetumika, lakini pia wakati mwingine wananchi wanaweza kulalamika kwamba nguvu kubwa imetumika, lakini hawaelewi Polisi huyo alikuwa katika mazingira gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama Polisi alikuwa kwenye mazingira magumu, lazima atumie nguvu ambayo itahakikisha kwamba kile kitendo ambacho kingefanyika hakitafanyika. Polisi wetu wanafanya kazi kubwa sana katika kupambana na uhalifu na uhalifu mwingine upo katika mazingira ya hatari sana. Ukisema tu kwamba Polisi asitumie nguvu yoyote ndugu zangu ni sisi wenyewe hawa hawa tutakaolalamika.

Kwa hiyo, mimi nasema kama raia tukiwa watiifu, Polisi hawawezi kutumia nguvu ya ziada, hawana sababu, simama umesimama, kaa chini, upo chini ya ulinzi umekaa, kwa vyovyote Polisi hawezi kutumia nguvu ya ziada. Lakini simama umeshika mawe, unataka Polisi afanyeje? Kwa hiyo, ninachoomba, tusije kuwakwaza Polisi kwani wanafanya kazi hii kwa maslahi ya raia wema. Tusije kuwakwaza wakashindwa kutekeleza wajibu wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nakumbuka kuna wakati huko nyuma raia wa kawaida walikuwa wanalalamika kwamba Polisi gani sasa, Polisi anamwambia mhalifu ndugu tafadhali twende Kituoni. Halafu yule ndugu anakataa na Polisi hana la kufanya. Sasa ukimfikisha Polisi hapo, basi usalama utakuwa hatarini. Kwa hiyo, mimi nasema hatupendi Polisi watumie nguvu ya ziada na tukiachie chombo hicho kijidhibiti. Nina hakika wana uwezo mzuri sana wa kujidhibiti na wamekwishafanya hivyo. Pale ambapo wale wakubwa wanadhani aliyetumwa kazi ametumia nguvu ya ziada wamemwadhibu, mimi nadhani tuwaache wafanye kazi kwa jinsi ambavyo taaluma yao ya ulinzi inavyotaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la nne, kuna suala limekuwa likiulizwa, limeulizwa hapa pia wakati Wabunge wanachangia na mwaka jana liliwahi kuulizwa, nalo ni suala la mradi wa inayoitwa Nyumba ya Mafuta au Mafuta *House,* Dar es Salalam. Nyumba hii inayoitwa Mafuta *House* ilikuwa ni mradi wa pamoja kati ya *TPDC* na *National Housing. National Housing* asilimia ishirini na tano kwa maana ya wenye kiwanja na *TPDC* asilimia sabini na tano kwa maana ya wajengaji, yaani wenye kutoa fedha za kujengea. Mradi huo ulijengwa kuanzia nadhani mwaka 1995. Ujenzi huo ulipofikia hatua fulani ukakwama na mkandarasi akawa hajalipwa fedha zake za ujenzi alioufanya. Alikuwa anadai Shilingi bilioni 4.6.

Ilipofika mwaka 2004, mkandarasi baada ya kukaa kwenye eneo la kazi kwa muda mrefu bila kulipwa fedha zake kwa karibu miaka mitano, akasema sasa ninalazimika kuvunja Mkataba, akawa anadai Shilingi bilioni 4.2 za kuvunja Mkataba kwa sababu aliyemwajiri ameshindwa kumlipa fedha zake na ameshindwa kumfanya aendelee na kazi. Lakini tangu mwaka nadhani wa 1996, *TPDC* wakawa wanatafuta mtu wa kuingia naye ubia ili akamilishe jengo hilo. Jengo hilo kwa wakati huo lilikuwa linahitaji kukamilishwa kwa Shilingi bilioni 15. Wametafuta mtu kwa njia yoyote wameshindwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004, wakati sasa mkandarasi anataka kuondoka kwenye *site*, ametoa *notice* ya kuvunja Mkataba, mimi nikawaita wahusika, Viongozi wa *TPDC* na viongozi wa *National Housing*, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Fedha, watu wa *NSSF*, Wizara ya Kazi, tukakaa pamoja nikawauliza *TPDC* wana utaratibu gani wa kukamilisha hilo jengo? Wakasema wameshindwa kabisa kupata mbia. Kwa hiyo, hawana namna yoyote ya kukamilisha hilo jengo. Wakasema, wanachoomba ni Serikali iwape fedha hizo Shilingi bilioni 15 na zaidi ili waweze kukamilisha hilo jengo.

Waziri wa Fedha akasema hana hizo fedha hata kidogo. Lakini wakati huo kulikuwa na vifaa vya umeme, kulikuwa na makontena nadhani matano yameshakaa bandarini miaka mitano. *Contractor* akasema hizo *container* hata sasa ukienda kuzichukua, hivyo vifaa kwa vile ni vya umeme, ni vifaa vya *lift* na kadhalika vitakuwa vimeoza. Kwa hiyo, hiyo ni hasara nyingine. Lakini kulikuwa na vifaa vingine ambavyo vilikuwa kwenye sehemu ya chini ambayo wanaita *basement* na vyenyewe akasema vimeharibika kabisa, havina kazi. Kwa hiyo, ni hasara. Kwa hiyo, kitakachohitajika hakiwezi kuwa Shilingi bilioni 15 peke yake.

Kwa hiyo, tukajadiliana tufanye nini ili hilo jengo likamilike, wameshindwa kupata mbia yeyote, wao wenyewe wakasema kwa kweli tumeshindwa, tumejaribu kila namna haiwezekani. Walijaribu kuongea na Mashirika haya ya *NSSF* na *PPF* ili waingie nao ubia wakasema haiwezekani. Sababu walizoeleza ni kwamba, thamani ya jengo katika ujenzi huo iliyokuwa inahitajika ni zaidi ya Shilingi bilioni 15 na iliyotumika ni zaidi ya Shilingi bilioni 15, wakasema thamani iliyoingia hailingani na hiyo fedha. Kwa hiyo hakuna mtu anayetaka kuingia kwenye ubia huo. Lakini pia jengo limejengwa kizamani sana sio kisasa. Kwa hiyo, wakawa wamekataa kuingia ubia, lakini wakasema kama wao watapewa kama mradi waukamilishe kwa fedha zao wapo tayari.

Mheshimiwa Spika, tukawauliza wahusika na hiyo miradi *TPDC* na *National Housing* wakasema, wao watashukuru angalau hilo jengo likamilike. Kwa hiyo, tukakubaliana jengo hilo tuwape *NSSF* kwa masharti. Moja, walipe madeni yote anayodai *contractor* ambayo kwa madai ya kazi aliyomaliza yalikuwa ni Shilingi bilioni 4.6 lakini kulikuwa na fedha hizo za kukaa kwenye *site* bila kazi wakati ametoa *notice* ya kuvunja Mkataba ilikuwa ni Shilingi bilioni 4.2. Tukasema mkajadiliane kama anaweza kuwapunguzia hilo, lakini hivyo vifaa vilivyoko bandarini vinafaa, havifai mkavikomboe kwa gharama yenu.

Kwa hiyo, tukasema tukiwakabidhi hili msije mkadai *TPDC* chochote wala nyie msije kudaiwa. Lakini mkamilishe jengo na mlipe madeni yote. Tumelipa Shirika la Wafanyakazi, sasa watu wanauliza: Kwa nini imekuwa hivyo? Sasa mlitaka likae pale, zile sementi zikae pale miaka nenda rudi! Kwa hiyo, ndicho kilichofanyika na mimi nilidhani ni jambo la uzalendo sana limefanyika. Ingekuwa nimewapa Kampuni binafsi kweli ni haki kusema, lakini *NSSF* ya wafanyakazi wetu!

Jambo lingine ni biashara ya mazao. Nataka tu nizungumze kwa ujumla. Mazao yetu yote hasa haya ambayo tunayauza nje katika masoko ya dunia na hasa kwa hapa ndani lilizungumzwa sana zao la pamba na tumbaku.

Zao la pamba kama tunavyokumbuka mwaka jana 2004 lilileta tatizo sana wakati wa Bunge la Bajeti hivi hivi. Bei ya dira ilitangazwa ni Sh. 300/= kwa kilo, bei katika Soko la Dunia ikawa inashuka. Wakulima hawakuelewa, Waheshimiwa Wabunge hawakuelewa, ikabidi tuingilie kati kujaribu kutafuta fedha hapa na pale katika makato mbalimbali ili angalau kuongeza bei kidogo. Lakini nikatahadharisha kwamba mwelekeo ni kwamba bei ilikuwa inaendelea kushuka na ikiendelea kushuka hakuna mfanyabiashara atakayenunua zao kwa hasara. Haiwezekani kwamba anunue ili yeye atakapokwenda kuliuza apate hasara.

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni biashara ya Kimataifa, lakini hata biashara katika masoko yetu. Hata wanaouza ng’ombe kama kuna mchinjaji ananunua ng’ombe, hawezi kununua ng’ombe wako kwa Sh. 300,000/= kama yeye anajua akienda kumchinja bei ya nyama imeshuka atapata Sh.250,000/=. Hiyo ni kawaida katika biashara.

Kwa hiyo, tunapenda kusema kwamba, ni vyema wakulima wetu wakaelewa kwamba katika biashara yoyote kuna kupanda na kushuka na hili ndilo linalotokea katika mazao yetu. Sasa mwaka jana nilieleza hapa nikasema kwamba, mazao kama kahawa walikuwa pia wanatoa bei ya dira, ikawa inaleta matatizo hivyo hivyo, wakulima hawaelewi kwamba bei ya dira ni bei ya dira, wao wanajua ni bei ambayo Serikali imetangaza.

Kwa hiyo *Board* ya Kahawa na wanunuzi wa kahawa na wakulima wa kahawa wakaamua kuachana na utaratibnu huo wa kutangaza bei ya dira na mpaka leo husikii sokomoko tena.

Kwa upande wa kahawa, wameanza kujua namna ya kupata bei nzuri ya kahawa. Namna ya kupata bei nzuri ni kupandisha ubora wa zao. Leo kule Moshi na sehemu nyingine wanazolima kahawa, kuna watu ambao kwa kilo moja niliambiwa kuna watu kwa kilo moja wanapata Dola mbili mpaka tatu wakati mwingine.

Lakini wakati huo huo kuna watu ambao kwa kilo yake anapata Sh. 500/=. Ndivyo biashara inavyokwenda na ndiyo maana tunasisitiza sana ubora wa mazao. Hata pamba itakuwa hivyo hivyo. Wale ambao watalima pamba bora na watakaolima pamba nyingi kwa ekari wataendelea kupata faida na wale ambao wataendelea kulima pamba hafifu na mazao machache kwa ekari, wataendelea kupata hasara. Kwa hiyo, la msingi ni kubadili kilimo chetu, lazima tulime mazao yawe bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeambiwa kwamba mwaka huu wadau wa pamba nao wameamua wasitangaze bei ya dira naa wao wanaanza kuingia kwenye soko la Kimataifa, soko la ushindani, kwa sababu bei ya dira inapata tafsiri potofu. Lakini nataka niwahakikishieni tu kwamba pamoja na yote hayo, nilisikia Waheshimiwa Wabunge wakisema Serikali isiache tu soko huria peke yake.

Ni kweli, Serikali hainunui mazao lakini haitaacha pia soko likawa la kutafunana. Ni lazima Serikali ina maslahi na wananchi wake na ina maslahi na wakulima wake. Kwa hiyo, tutaendelea kusimamia kwa kadri inavyowezekana. Pale ambapo ni dhahiri tunaona kwamba hapa wajanja wanataka kupunja wakulima, tutaingilia kati. Kwa hiyo, hatutaachia sheria ya porini ifanye kazi, sheria ya pori kwamba mwenye nguvu anamla mnyonge, hapana. Ila Serikali haitakwenda kununua yenyewe moja kwa moja. *(Makofi)*

Kuhusu tumbaku, nashukuru sana kwa yale ambayo nimeyasikia jana, lakini lipo lile tatizo la kwamba wenye kununua ndio wanaotoa pembejeo. Hili jambo tumelizungumza sana, mimi mwenyewe nakumbuka nimelifanyia sana kazi lakini walinishinda nguvu wakulima, kwa sababu mimi nilitaka tuondokane na utaratibu wa utegemezi wa pembejeo kwa wanunuzi.

Lakini nakumbuka wakati ule nilipokwenda kule Tabora, nikaambiwa wakulima wamesema ndio huo utaratibu wanautaka. Basi, nikanyoosha mikono nikasema utaratibu huo uendelee, lakini nilijua utakuwa na matatizo. Lakini sasa, labda dawa siyo kuvunja huo utaratibu, dawa ni kuanzisha utaratibu unaokwenda sambamba na huo ambao uwe bora zaidi ili wakulima wajitoe huko taratibu na huo ni kwa kuimarisha Vyama vya Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiwa na Vyama vya Ushirika vilivyo imara, wala haya matatizo hayatakuwepo utaona tu yanakwisha yenyewe. Kwa hiyo, naomba sana tuimarishe Vyama vyetu vya Ushirika.

Jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la kufutiwa madeni ya vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, napenda Waheshimiwa Wabunge waelewe tafsiri ya hili ni nini. Tunaposema Serikali ifute madeni ya Vyama vya Ushirika, maana yake unachosema ni Serikali ichukue kodi ya mwananchi kwenda kulipia madeni ya watu ambao wamezembea. Serikali imwadhibu yule mtu ambaye ameendelea kufanya vizuri ili kulipa madeni ya yule ambaye amefanya vituko, ndiyo maana yake. Kwa sababu Serikali haina mahali tu ambapo itachota fedha kwenda kulipa madeni. Unaposema ifute au isamehe ni lazima yule aliyekopesha alipwe, hakuna kitu tu kinayeyuka hivi, ni lazima yule alipwe.

Lakini unajiuliza vyama vyetu vya Ushirika, zamani vilikuwa vinafanya biashara peke yao, vinajitetea. Tumefuta mara nyingi tu madeni ya Vyama vya Ushirika. Siku hizi wanafanya biashara sambamba na Kampuni binafsi. Sasa unajiuliza, hivi Kampuni binafsi inawezaje ikanunua zao kwa bei ile ile ambapo Chama cha Ushirika kinanunua? Chama cha Ushirika kimechukua mkopo wake, huyu amechukua mkopo wake au amepata sijui fedha wapi, yule akalipa wakulima wake alionunua kwao.

Chama cha Ushirika kinashindwa kulipa Benki kule kilikochukua mkopo, kinashindwa kulipa wakulima; huyu hadaiwi kokote, hadaiwi na wakulima, bei ni ile ile. Lazima tukubali kuna kasoro mahali. Sasa bila kurekebisha hiyo kasoro, haiwezekani ikawa ni dawa kufuta madeni. Tunafuta madeni, nani awe anayalipa? Kwa hiyo, dawa ni tusimamie vyema Vyama vya Ushirika ili viwe vinafanya biashara kama ambavyo inatakiwa, kwa sababu kodi hizo tunazihitaji. Tunahitaji tuboreshe elimu, tunahitaji tuboreshe afya, tuboreshe barabara, maji na huduma mbalimbali kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la biashara kati ya Zanzibar na Dar es salaam. Bandari ya Zanzibar na Dar es salaam na kwamba mapato ya Zanzibar yameshuka sana, mimi sina sababu ya kukatalia hilo kwa sababu takwimu naziona. Sasa jawabu lake linaweza likashughulikiwa na Kamati yetu ya fedha ya pamoja, ilishughulikie hilo kuona jawabu lake ni nini. Lakini jawabu la mwisho wa yote ni kukuza uchumi. Tukikuza uchumi, haya mambo yote yatakwisha. Kwa sababu soko la Zanzibar ni dogo, lazima tukubaliane na hilo.

Kwa hiyo, mfanyabiashara yeyote ataona afadhali ashushie bidhaa zake Dar es Salaam kwa sababu soko ni kubwa kuliko kushusha Zanzibar ambapo soko ni dogo. Kwa hiyo, ni misingi tu ya biahara ya kupata fedha na soko ndilo linayotawala, sio kwamba kuna upande mmoja unamwonea mwingine, hapana. Lakini mimi nasema tuache wataalam wetu walifanyie kazi, Kamati yetu ifanyie kazi, lakini mwisho wa yote ni lazima tujitahidi sana kufufua uchumi. Hii tu ndiyo itatupa jawabu la kudumu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni Baraza la Taifa la Ushauri. Namshukuru, nadhani alikuwa Dr. Msekella aliyelielezea, lakini alisema kwamba yeye hakutaka liwepo kwenye Katiba, lakini kama liwepo hivi hivi analipenda. Sasa hivi hivi, nalo ni tatizo. Jambo kuwa hivi hivi, ni tatizo. Hili ni jambo ni kubwa na ndiyo maana tulisema wakati ule mliposema la nini, la nini, tukasema labda halijaiva. Sasa nashukuru limeanza kuiva, mimi nina hakika kwa wale wanaokuja safari ijayo, bila shaka wataona sasa hili limeiva.

Kwa kweli ni jambo jema kwa namna yoyote ile, ndiyo maana tulikuwa tumelifikiria liwepo kwenye mabadiliko ya kumi na nne ya Katiba, lakini ili mradi halikuweza kuingia, basi mimi nina hakika wenzetu ambao mtakuwepo sasa limeanza kueleweka mtalishughulikia kwa haraka zaidi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kilimo. Mimi nimeshukuru sana Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia kilimo kwamba kipewe umuhimu wa kutosha. Nakubaliana na ushauri huo na nataka niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge, tumeanza kuutekeleza, labda tu hatujafikia kiwango kikubwa sana kwa sababu tu ya udogo wa Bajeti yetu. Lakini kwa kweli ndiyo mwelekeo wa Serikali na ndiyo mwelekeo wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Nami nina hakika Ilani inayokuja ya Chama Cha Mapinduzi itakuwa na mwelekeo zaidi juu ya jambo hili. Ilani nyingine siwezi kuzisemea, sijui, lakini naamini hii nyingine ya Chama Cha Mapinduzi ndiyo itakayotekelezwa. *(Makofi)*

Mimi naamini kabisa kwamba bila kilimo chetu kubadilika, tutapata tabu sana kupata ukuaji wa kuridhisha wa uchumi wetu. Kilimo ndicho kitakachoweza kubadili hali za wananchi. Hata huu umaskini wa mfukoni tunaousema bila ya kubadilisha kilimo, ni vigumu sana kuondoa umaskini wa fedha. Sasa tufanyeje? *(Makofi)*

Kuna maeneo ambayo lazima tuyatilie mkazo, nilikwishasema tena, lakini niyarudie tu kwa kifupi kabisa.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuwe na kilimo cha kisasa na cha kibiashara. Bado tunalima kilimo cha kujikimu *(subsistence farming)* hakitupeleki popote. Ni lazima sasa tufanye kilimo cha biashara. Mimi nasema, kama wako Watanzania ambao wanaweza kulima mashamba makubwa, wapewe fursa. Mimi nashukuru sana, wako Waheshimiwa Wabunge hapa wana mashamba mazuri tu makubwa na mimi ningependa wengine waige mfano huo. *(Makofi)*

Ni lazima tulime mazao ya faida. Habari ya kulima mazao ya mazoea lazima tuachane nayo. Kwamba umemkuta babu yako analima mahindi, basi wewe ni hayo hayo. Ni lazima tulime kilimo cha faida. Wataalam wetu wa masoko na wataalam wa kilimo wasaidie wananchi ni mazao gani ambayo sasa katika Soko la Dunia yana bei kubwa. *(Makofi)*

Labda niwachekeshe. Sijui ni kuchekesha, lakini mimi niliwahi kwenda kwenye Mkutano wa Pamba Mwanza. Nikapokea zile taarifa za Pamba. Mwaka ule, nadhani ilikuwa kwenye mwaka 2000/2001, nilipiga hesabu za haraka. Mkulima wa pamba Mwanza wakati ule kwa bei ya pamba iliyokuwepo, alikuwa anapata mapato ya jumla siyo faida,wastani wa Sh.83,000/= kwa ekari. Amezidi sana Sh.120,000/=. Hakuna namna yoyote utamfanya huyo mwananchi, ana watoto sita nyumbani, wengine labda wake wawili, watoto 12 utarajie kwamba ataondokana na umaskini.

Lakini kuna mazao ambayo mkulima kwa ekari ile ile, kwa juhudi tena labda pungufu ya ile ya pamba, anaweza akapata Sh.800,000/= mpaka Sh.1,000,000/=. Hiyo

ndiyo kazi tunayotakiwa tufanye wataalam pamoja na sisi wanasiasa. Tukifanya hiyo kazi, Mtanzania ataondokana na umaskini. Lakini kama ni ilimradi tu mahindi yanaonekana tu ni ya kijani shambani tunapiga makofi kwamba mwaka huu mazao mazuri, tutaendelea na umaskini miaka nenda miaka rudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji lazima kitiliwe mkazo. Yako maeneo mengi sana katika nchi hii ambayo yanaweza yakamwagiliwa bila hata kuhitaji gharama kubwa. Mengine yalikuwa yanamwagiliwa huko nyuma, mifereji ile imeharibika tu na kutengeneza hiyo mifereji inahitaji majembe ya mkono, lakini hatuyasimamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, usindikaji wa mazao, hili ni eneo lingine muhimu sana. Kama tutaendelea kuuza marobota ya pamba Ulaya, hatufiki popote. Kama tunabeba Korosho, tunapeleka na maganda yake India wakabangue wao, hatufiki popote. Kama tunauza Katani kama nyuzi, hatufiki popote. Ni lazima mazao yasindikwe na mwisho ni kuongeza mauzo nchi za nje, hapo ndipo tutakuwa tumeondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa nigusie, ni juu ya kuendeleza Vijana. Limegusiwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kwamba Vijana ni Jeshi ambalo tusipoliangalia lina hatari na mimi nakubaliana kabisa. Sasa, yako mengi ambayo yanafanyika, huku kuboresha elimu, kujitahidi vijana wengi wasome kadri inavyowezekana, wengi wafike Sekondari ni katika kuwaandaa. Jeshi la Kujenga Taifa kulirudisha ni katika juhudi hizo hizo. Mikakati kama MKURABITA, yote ina lengo la kuboresha mazingira ya kuweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Sasa tunalo tatizo la ajira, lakini kwa bahati mbaya sana hata sisi viongozi wakubwa wa siasa tunatoa tafsiri ya ajira ambayo si sahihi. Tunatoa tafsiri ya ajira kana kwamba kila mtoto wa Tanzania anayemaliza Darasa la Saba, anayemaliza Darasa la Kumi na Mbili, anayemaliza la Kumi na Nne na Chuo Kikuu na Vyuo mbali mbali ni lazima aajiriwe ili awe na mashahara mwisho wa mwezi. Hii ni tafsiri potofu ya ajira. Ni lazima tuwaeleze vijana wetu, tunamaanisha nini tunaposema tunawaandaa ili waweze kujitegemea. Mimi naamini tukiweza kuwaeleza vijana, watatuelewa. *(Makofi)*

Kama tukiboresha kilimo kama nilivyoeleza, katika ekari moja akawa na faida angalau Sh.500,000/= vijana hawatakuja Mjini, watabaki huko huko kwa sababu kuna faida ya kulima. Lakini kama faida katika ekari moja ni Sh. 60,000/=, Sh.70,000/=, Sh.80,000/=, kwa kweli watakuja Mjini. Kwa hiyo, ni lazima tuweke tafsiri sahihi. Lakini jawabu la yote haya ni kukuza uchumi. Tukikuza uchumi haya yote yatakwisha.

Mheshimiwa Spika, nigusie tu kidogo suala la amani na utulivu. Nimesema tuko kwenye kipindi cha uchaguzi, ni vyema kabisa wote tuwe waangalifu hasa sisi wanasiasa. Tuache maneno ambayo yanaonyesha uchochezi, maneno yanayoamsha jazba, maneno yanayoamsha dharau, maneno yanayoonyesha ati tunaweza kupambana tu na Serikali na tunatumia vijana ambao ni maskini, wanaweza wakaumia bila sababu. Sisi tulio Viongozi wa Vyama tuwe wadau wakubwa wa amani. Sisi tukishakuwa wadau wa amani, hawa vijana wetu hawana wala sababu ya kufanya fujo, hata wao hawapendi fujo. Lakini tukiwachemsha, wao ni damu inayochemka, watachemka. Lakini tusiwachemshe.

Namshukuru sana Mheshimiwa Magoba, alisema "lugha zenye vitisho majukwaani tuache." Akasema "Tushirikiane na Chama Tawala kuleta maendeleo" Namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la uwiano wa maendeleo Kimkoa. Hili jambo limezungumzwa sana na Waheshimiwa kadhaa na kwa kweli ukiliangalia kwa haraka linaleta matatizo hayo au mtazamo huo, lakini kama nilivyoeleza, hata mwaka jana nimelielezea vizuri sana na tumeendelea kufanya juhudi za kurekebisha hali hiyo.

Wizara yetu ya TAMISEMI ilifanya utafiti wa kina kuona ni namna gani tunaweza tukagawana hiki kidogo kilichoko na ndiyo wamekuja na *formula* ile ya kusema sasa wanangalia ukubwa wa eneo, idadi ya watu na hali ya umaskini na ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wameangalia takwimu zile za fedha za ndani wameridhika sana kwa sababu zenyewe zimejielekeza huko vizuri zaidi.

Sasa kwa upande wa fedha za nje, nazo zimejielekeza kwa huko, ila tu kuna maeneo ambayo yana sababu za tofauti. Kwa mfano kuna Miradi ambayo inaendelea, lazima ikamilishwe na ina fedha za nje, lazima Mkoa huo utaonekana umepata fedha nyingi. Lakini siyo hiyo tu, kuna miradi ambayo haiwezi kuanza kwa nchi nzima kwa mara moja. Mnajua kwamba kwa mfano hata *TASAF* ilikuwa kwenye Wilaya 45, ungeangalia Bajeti za zile Wilaya wakati ule, lazima ungeona Bajeti zao ni kubwa.

Kuna miradi ambayo haipo kwa nchi nzima. Kuna hii miradi ya maji sasa hivi ya Benki ya Dunia, ingawaje tumesema inachukua nchi nzima lakini haianzi yote kwa mara moja. Kuna sehemu inaanza kwa mfano Mkoa wa Pwani ambao ulitolewa mfano. Kilichosababisha fedha zikawa nyingi pale ni Mradi wa Maji wa Benki ya Dunia. Mradi wa namna hiyo pia uko Dodoma ingawaje siyo ule wa Benki ya Dunia, lakini ambao unafadhiliwa na Uingereza.

Kwa hiyo, kuna miradi maalum ambayo unakuta ama siyo ya nchi nzima, ni ya maeneo fulani fulani. Sasa lazima fedha zitakuwa tofauti lakini tumefanya juhudi sana ili kuweza kuweka hali ya usawa kadri inavyowezekana ili fedha kidogo zinazopatikana kwa maendeleo ziweze kuenea. Mengine yataonekana kwenye Wizara mbali mbali. Miradi ya barabara, miradi ya maji, mwingine kama ni mradi ambao ni maalum, utaonekana kwenye Wizara ya Maji. Sasa katika hali hiyo, lazima fedha zitatofautiana lakini tutafanya juhudi zote kuhakikisha kwamba uwiano unakuwepo kwa kadri inavyowezekana tunafanya kila jitihada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nigusie maeneo machache ambayo ameyasemea Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Sitaki kujibu yale ambayo ameyasemea kwa sababu yamejibiwa tangu Alhamisi, watu wamekuwa wakiyajibu. Hotuba yake yenyewe mliona ilivyofanana. Haifai kwa kweli hata kujibiwa lakini kuna maeneo yasipopata ufafanuzi watu wanaweza wakadhani yale aliyoyasema ni ya kweli. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa bahati mbaya, tangu alipotoa hotuba yake hakukaa tena hapa Bungeni, ingawaje yuko Dodoma. Sasa hili linaonyesha tu kwa mwanasiasa maana yake umesema maneno ambayo hutaki kusikia utakavyojibiwa. Sasa hili ni tatizo, maana mwanasiasa lazima uwe na nguvu. Ukiyaeleza mambo lazima uwe na nguvu ya kuyasikiliza majibu na kuyahimili. Husemi tu halafu ukakimbia, haisaidii. *(Makofi/Kicheko)*

Moja ambalo ni la jumla tu alilokuwa analaumu zaidi kwamba hakuna maendeleo, nadhani hotuba yangu nilieleza yaliyofanyika tangu mwaka 1995 mpaka mwaka 2005 na Waheshimiwa Mawaziri wameonyesha vile vitabu vyetu vya taarifa vina kila kitu. Lakini wananchi wa nchi hii wanaona sana. Sote tunatembea katika nchi yetu na tumeona jinsi wananchi ambavyo wanaridhika sana na kazi ambayo Serikali imefanya. *(Makofi)*

Chama Cha Mapinduzi kinaridhika sana na jinsi Serikali ilivyotekeleza ilani yake. Kwa hiyo, mimi nafikiri hilo halina tatizo hata kidogo. Lakini alichonishangaza alisema hata kile kidogo cha mafanikio kilichofanyika ni kwa msukumo wa Wapinzani. La! Hapo ndiyo sikumwelewa kwa sababu Sera na ilani inayotekelezwa ni ya Chama Cha Mapinduzi. Kama Wapinzani waliweka msukumo ili Serikali itekeleze Sera na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, sasa Vyama vyao ni vya nini?

Kama kazi yenu ni kusukuma ilani ya CCM itekelezwe, basi CCM itatawala milele tu. Lakini Mheshimiwa huyu nadhani huwa haangalii hata vile vitabu tunavyopewa vya orodha ya Wabunge. CCM sasa hivi hapa tuko 254, Wapinzani wako 34. Hivi hao ndiyo wa kusukuma mpaka tofauti itokee? Basi watakuwa wana nguvu ya ajabu, labda siyo ya kibinadamu. Kwa hiyo, haya yote yaliyotokea yanatokana sana sana na Waheshimiwa Wabunge wa CCM kuishauri na kuisimamia Serikali yao ikatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa amesema kama kawaida Ripoti ya Tume ya Dr. Kipokola juu ya madini imeendelea kuwa siri ya Serikali. Jamani! Hata kama tunasahau kwa haraka, Mkutano wa 19 tumefanya Semina hapa na taarifa hiyo tukaigawa na Waheshimiwa Wabunge mkasema mnahitaji Semina nyingine. Sasa huyu leo anasema ni siri ya Serikali! Nadhani tatizo ni lile la kutokuhudhuria Bungeni. Sasa hilo mimi siwezi kumsaidia.

Lingine, amesema Waziri wa Fedha amedanganya Bunge kwa kuelezea yale aliyosema Rais akiwa Songea. Waziri wa Fedha ameeleza sahihi kabisa yale aliyoyasema Rais akiwa Songea. Hata yeye mwenyewe aliponukuu hapa, ni yale yale, mimi namshangaa anampiga vita Waziri kwa sababu gani! Kwa sababu ni yale yale, hata yeye hakueleza kwamba Rais alisema watalipwa Shilingi bilioni 400. Rais alisema "Nitahakikisha mtaanza kulipwa kwa fedha ambayo imetengwa kwenye Bajeti." Ndicho alichosema Waziri wa Fedha. Akasema: "Tutajadiliana kuona kiwango ambacho mnadai kwa usahihi." Ndicho Waziri wa Fedha alichosema. Lakini anasema Waziri wa Fedha kadanganya Bunge. Sasa haya ndiyo matatizo mengine ya uelewa wa mambo. *(Makofi)*

Amesema, ubinafsishaji ni kupanda mchicha na kuvuna bangi. Pamoja na kwamba lugha zenyewe si za kibunge na si ya kiongozi, lakini kwa kweli kama mtu haoni faida ya

ubinafsishaji mpaka leo, Mbunge mzima tena kiongozi wa upande mzima wa Upinzani, basi kuna matatizo. Viwanda vyote vilivyobinafsishwa vinavyozalisha yeye haoni, basi kuna matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulifafanua ni kwamba Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi aliombwa na Mkoa wa Kilimanjaro akawa Mgeni rasmi kwenye hafla ya kuchangia Mfuko wa Chama Mkoa wa Kilimanjaro. Hayo yamefanyika na Viongozi wengi tu. Mimi nimefanya, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete amefanya, tena sehemu nyingine zimepatikana fedha nyingi kuliko hizo zilizopatikana za Mkoa wa Kilimanjaro. Ni nini hicho cha ajabu ambacho leo Kiongozi wa Upinzani anakuja kuelezea hapa? *(Makofi)*

Lakini nikawa najiuliza, hivi wao hawana Mwenyekiti wa Chama? Si wafanye? Lakini kama mmezidiwa kabisa mnaweza mkamwomba na Mwenyekiti wetu kama atakubali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa kabisa Vyama vya Siasa popote duniani vinachangiwa na wapenzi na wanachama wao na ndivyo Chama cha Mapinduzi kinavyofanya. Mimi nataka niwaulize hawa wenzetu wa *CUF* basi, maana yeye anatokea *CUF*, maana tunaona na wao wanafanya shughuli za Chama. Hizi fedha wanazipata wapi? Sisi fedha zetu zinachangishwa hadharani na zinatangazwa, ninyi zenu tunawaona tu mnafanya kazi, hizo hela mnapata wapi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, pia Kiongozi wa Upinzani, kwa kweli alimsingizia Rais, kwenye hotuba yake. Alisema: nataka ninukuu hiyo sehemu, amesema hivi: "Mbaya zaidi ni pale Rais Amirijeshi Mkuu, Mwenyekiti wa Chama Tawala, anapotamka hadharani kwamba atatumia nguvu zake zote na uwezo wake wote na vyombo vya dola kuhakikisha anaua Upinzani." Rais hajasema hili hata kidogo! Yaani ni uongo, sijawahi kuona kwamba kiongozi mzima anaweza akasimama hapa Bungeni kweli akasema hayo! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mimi nilikuwepo, Mheshimiwa Rais alichosema alikuwa anazungumzia uchaguzi kwamba lazima uwe wa amani. Akasema: "Wapo ambao wanatishia kuchukua madaraka kwa kutumia fujo na nguvu, akasema sitakubali, sitaruhusu. Ikifika hapo nitatumia nguvu ya dola kuhakikisha uchaguzi utakuwa wa huru na wa haki." Sasa huyu bwana anakuja kuleta maneno ya ajabu hapa! *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Apelekwe kwenye Tume ya Simpasa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kwa kweli maneno aliyoyazungumza/aliyotoa kwenye hotuba yake yalikuwa hayaweki hadhi ya Kiongozi wa Upinzani. Lakini mimi nimalizie hapo, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi ambavyo mmechangia hoja yangu, jinsi mlivyotoa ushauri na napenda kurudia tena kwa heshima kubwa kwamba ushauri wenu tunaupokea, tunaukubali na utafanyiwa kazi na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sehemu ya kwanza ya kushughulikia hoja hii, yaani Mjadala kuijadili sasa tumekamilisha, tunakwenda kwenye sehemu ya pili. Katibu hebu itamke hiyo sehemu ya pili.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**Matumizi ya Kawaida**

**Fungu 25 - Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 - *Administration and General*.. ... ... ... Sh.1,749,077,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 27 - Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kifungu 1001- *Administration and General*.. ... ... ... Sh. 9,738,274,500/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 - *Administration and General*. ... ... ..Sh. 1,986,695,500/=
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... Sh. 272,496,000/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... . Sh. 1,769,203,800/=
Kifungu 1004 - *Internal Audit* ... ... ... ... Sh. 197,846,200/=
Kifungu 2001 - *Civil Affairs and Contingencies* ... ...Sh. 434,833,800/=
Kifungu 2002 - *National Festivals* ... ... ... .Sh. 492,153,600/=
Kifungu 3001 - *Parliamentary and Political Affair*.. Sh. 354,957,200/=
Kifungu 5001 - *Coordination of Government Business* ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 495,636,300/=
Kifungu 7001 - *Government Printer* . ... ... ...Sh. 3,406,807,200/=
Kifungu 7003 - *Information Services* ... ... ... ... Sh. 7,903,894,800/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42 - Ofisi ya Spika**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... Sh. 3,910,664,000/=
Kifungu 2001 - *National Assembly* ... ... ... ... ...Sh. 25,729,213,200/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 61 - Tume ya Uchaguzi**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... ... ... Sh. 31,429,042,100/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91 - Tume ya Madawa ya Kulevya**

Kifungu 1001 - *Administration and General* . ... ... ... Sh.1,006,606,900/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92 - TACAIDS**

Kifungu 1001 - *Policy, Planning and National Response*..... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 292,670,000/=
Kifungu 1002 - *Finance, Admin and Resource Mobilization* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ..Sh. 2,556,544,600/=
Kifungu 1003 - *Monitoring, Evaluation, Research and Mis* ... ...... ... ... ... ... ... ... ... ... .....Sh. 553,380,000/=
Kifungu 1004 - *Advocacy Information Education and Comm.* ... ... ... ... ... ... Sh. 456,550,000/=
Kifungu 1005 - *District and Community Response* .. Sh. 709,850,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... Sh. 300,000,000/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... Sh. 400,000,000/=
Kifungu 5001 -*Coordination of Government Business* ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 11,457,683,800/=
Kifungu 7003 - *Information Services* ... ... ... ... ... Sh. 600,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42 - Ofisi ya Spika**

Kifungu 2001 - *National Assembly* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 950,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92 - TACAIDS**

Kifungu 1001 - *Policy, Planning and National Response*... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 757,580,000/=
Kifungu 1002 - *Finance, Admin and Resource Mobilization* ... ... ... ... ... ... ... ... ... .Sh. 14,478,630,000/=
Kifungu 1003 - *Monitoring, Evaluation, Research and Mis*.. ... ... ... ... ... ... ...Sh. 1,126,580,000/=
Kifungu 1004 - *Advocacy Information Education and Comm* . ... ... ... ... ... .Sh. 3,966,260,000/=
Kifungu 1005 - *District and Community Response* ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 12,339,463,400/=

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba baada ya Bunge lako Tukufu kuketi kama Kamati ya Bunge zima na kupitia kifungu kwa kifungu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2005/2006 kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizopo chini yake na yale ya Ofisi ya Bunge na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Naomba kutoa hoja kwamba Makadirio haya sasa yakubalike.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka 2005/2006 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hadi kufikia hapo ndiyo tumefika mwisho wa shughuli za leo. Kesho tutajadili hoja ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, sasa naahirisha Bunge hadi kesho asubuhi saa tatu.

*(Saa 12.17 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne tarehe 21 Juni, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*